TAARIFA YA KAMATI YA UANDISHI YA BUNGE MAALUM KUHUSU IBARA ZA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

(Imeandaliwa wwa mujibu wa Kanuni ya 35(6), 35(6A), 35(7) na 35(9) ya Kanuni za Bunge Maalum za Mwaka 2014)

1.0 UTANGULIZI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(9) ya Kanuni za Bunge Maalum za Mwaka 2014, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, Taarifa ya Kamati ya Uandishi ya Bunge Maalum kuhusu Ibara za Sura ya Kwanza mpaka ya Kumi na Sita za Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano zilizoandikwa upya pamoja na Ibara za Sura Mpya zilizopendekezwa wakati wa mijadala ya Rasimu ya Tume katika Kamati za Bunge Maalum na ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge Maalum kuhitimisha mjadala wa Sura ya Kwanza hadi Kumi na Sita pamoja na Sura Mpya, Kamati ya Uandishi ilielekezwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuyafanyia kazi maamuzi ya Bunge Maalum kwa mujibu wa Kanuni ya 35(6) ya Kanuni za Bunge Maalum. Kamati ya Uandishi ilikutana Dodoma katika ukumbi wa Pius Msekwa B kwa ajili ya kutekeleza maelekezo hayo kuhusu Ibara za Sura ya Kwanza hadi ya Kumi na Sita za Rasimu ya Katiba pamoja na Sura mpya.

1.1 MAJUKUMU YA KAMATI YA UANDISHI

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 35(7) ni kuandika upya Ibara za Sura za Rasimu ya Katiba zilizojadiliwa na Bunge Maalum na hatimaye kutoa taarifa kwa Mwenyekiti baada ya kukamilisha kazi hiyo. Hivyo, Kamati ya Uandishi ilikuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mapendekezo ya marekebisho, maboresho au mabadiliko katika Ibara za Sura ya Kwanza hadi ya Kumi na Sita pamoja na Sura mpya za Rasimu ya Katiba yanakidhi matakwa na masharti ya Kanuni za Bunge Maalum za Mwaka 2014.

1.2 MAMBO YALIYOZINGATIWA NA KAMATI YA UANDISHI

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi kama yalivyotamkwa katika Kanuni ya 35(7) ya Kanuni za Bunge Maalum za Mwaka 2014, Kamati ya Uandishi ilizingatia mambo yafuatayo:

(a) masharti ya Kanuni ya 35(6) ya Kanuni za Bunge Maalum yanayoitaka Kamati ya Uandishi kuzingatia taarifa za Kamati za Bunge Maalum;
(b) maoni na mapendekezo yanayotokana na mjadala ndani ya Bunge Maalum kuhusu taarifa za Kamati hizo;
(c) misingi ya uandishi wa sheria;
(d) marejeo ya Ibara za Rasimu ya Katiba;

(e) uwiano, mfanano, mpangilio wa Ibara na mtiririko wa kimaudhui wa Ibara za Rasimu ya Katiba;

(f) marejeo ya Ibara za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka, 1977 pale ilipohitajika;

(g) Sheria mbalimbali za nchi pale ilipohitajika;

(h) matumizi fasaha ya lugha ya kiswahili;

(i) tafiti mbalimbali katika Sheria na Katiba za Nchi nyingine; na

(j) hali na mazingira ya kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilizingatia mambo hayo ili kuhakikisha-

(a) Ibara za Sura ya Kwanza hadi ya Kumi na Sita pamoja na Sura mpya za Rasimu ya Katiba zimebeba maoni na mapendekezo ya Wajumbe katika Kamati mbalimbali;

(b) Ibara zinaeleweka bayana kwa msomaji pasipo utata au kukinzana katika maudhui yake;

(c) Ibara za Rasimu ya Katiba zina mpangilio na mtiririko mzuri kimaudhui; na

(d) Ibara za Rasimu ya Katiba zimeandikwa kwa kutumia Kiswahili fasaha.

1.3 UANDISHI WA IBARA ZA RASIMU YA KATIBA INAYOPENDEKEZWA

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuandika upya Ibara za Rasimu ya Tume, Kamati ya Uandishi ilitafakari na kuzingatia mapendekezo na maoni mbalimbali ya Kamati zote Kumi na Mbili za Bunge Maalum na maoni na mapendekezo yaliyotokana na mijadala ya taarifa za Kamati hizo katika Bunge Maalum kuhusu Sura ya Kwanza hadi ya Kumi na Sita pamoja na Sura Mpya za Rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ya kitaalamu haikuwa rahisi hasa ikizingatiwa kwamba Kamati mbalimbali zilitoa mapendekezo ya kuboresha maudhui ya Ibara za Rasimu yaliyotofautiana. Aidha, mapendekezo yaliyotolewa yaliambatishwa na Rasimu pamoja na Ibara mbalimbali kutoka kwenye Kamati za Bunge Maalum au Wajumbe wa Bunge Maalum. Katika mazingira haya, Kamati ya Uandishi ilifanya kazi ya kujumuisha, kuainisha na kuwianisha mapendekezo yote kwa kuzingatia maudhui yake ili kuandika upya Ibara ambazo zinajitosheleza. Mapendekezo mengine yaliilazimu Kamati ya Uandishi kujielekeza katika Ibara za Rasimu ya Katiba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Sheria za nchi, na Katiba za nchi nyingine ili kuandika Ibara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Ibara za Rasimu za Katiba zimebaki kama zilivyo kwa kuwa maudhui yake

yanajitosheleza. Ibara nyingine za Rasimu ya Katiba zimefutwa kwa kuwa:

(a) maudhui yake yamezingatiwa katika Ibara nyingine;

(b) maudhui yake yamebebwa katika mapendekezo mengine;

(c) maudhui yake yanapaswa kuzingatiwa katika sheria za nchi;

(d) maudhui ya Ibara nyingine yamehamishiwa kwenye Ibara nyingine ili kuweka pamoja maudhui yanayofanana; na

(e) maudhui mengine yamegawanywa katika Ibara ndogo tofauti kwa lengo la kuyaweka wazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura mbili mpya ambazo hazikuwemo katika Rasimu ya Tume zinapendekezwa katika Rasimu hii ya Katiba inayopendekezwa. Sura hizo ni ile inayohusu Ardhi, Maliasili na Mazingira na Sura inayohusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Aidha, Sura ya Pili ilikuwa na Sehemu Moja tu, sasa inapendekezwa kuwa na Sehemu Tano na pia Ibara nyingine mpya zimependekezwa katika Rasimu ya Katiba inayopendekezwa. Marekebisho haya yanalenga kupata Katiba bora, yenye maudhui yanayojitosheleza, itakayoeleweka na kutumika kwa urahisi na wananchi.

1.4 MAPENDEKEZO YA IBARA ZA RASIMU

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia Ibara za Rasimu ya Katiba iliyowasilishwa na Tume, Kamati ya Uandishi ilikutana na changamoto nyingi kutoka Kamati za Bunge Maalum. Mapendekezo mbalimbali ya Kamati na majadiliano Bungeni yaliazimia kufuta baadhi ya Ibara, ibara ndogo au aya na wakati mwingine kuziandika upya. Hali hii ililazimu kupanga upya Ibara, ibara ndogo au aya ili kuleta mtiririko mzuri wa kimaudhui na kimaandishi. Mtiririko huo wa kimaudhui na kiuandishi umesababisha kubadilika kwa maudhui ya Ibara uliofanya maudhui hayo yalotofautiana na yaliyomo kwenye Rasimu ya Mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara za Sura ya Kwanza hadi ya Kumi na Sita za Rasimu ya Katiba zilizoandikwa upya baada ya kufanyiwa maboresho, zisomeke kama zinavyoonekana katika Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba inayopendekezwa ambayo imewasilishwa katika Bunge Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya ufafanuzi wa Kamati ya Uandishi kwa kila Ibara au ibara ndogo iliyoandikwa upya ni kama ifuatavyo:

SURA YA KWANZA
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SEHEMU YA KWANZA
JINA, MIPAKA, ALAMA, LUGHA NA TUNU ZA TAIFA

2.0 IBARA YA 1: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii kulikuwa na mapendekezo mbalimbali kutoka katika Kamati na mijadala ndani ya Bunge Maalum. Aidha, mapendekezo hayo yalikuwa na lengo la kurekebisha ibara ndogo ya (1) na ya (2) kwa kufuta neno "Shirikisho", ambalo lilikuwa linaleta dhana ya Muundo wa Serikali Tatu. Neno hilo lilifutwa kwa kuwa mapendekezo yaliyotolewa na Wajumbe walio wengi ndani ya Kamati zote kumi na mbili za Bunge Maalum yalilenga kuwepo kwa Muundo wa Serikali Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilitafakari na kuainisha maudhui ya Ibara mbalimbali zilizopendekezwa na pia kufanya maboresho ya kiuandishi katika Ibara hii. Maboresho muhimu yalijumuisha kuongeza maneno yanayotaja tarehe na mwaka wa Hati ya Makubaliano ya Muungano katika Ibara hii kwa umuhimu wa Hati hiyo katika historia ya nchi yetu.

Katika ibara ndogo ya (2), Kamati ilifanya maboresho ya kiuandishi kuhusu matumizi ya neno **"kujitegemea"** ambalo lilionekana kuleta kasoro katika mtiririko fasaha katika Ibara hii

ndogo. Aidha, ibara ndogo ya (3) haikuwa na marekebisho kwa kuwa ilikuwa inajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 1 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

2.1 IBARA YA 2: Eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii, Kamati zote Kumi na Mbili zilipendekeza marekebisho ya kuainisha mipaka na eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mapendekezo hayo yalilenga kufafanua zaidi mipaka ya nchi kwa kuzingatia ardhi, anga, mito, maziwa, milima, bahari, bahari kuu, na kitanda cha bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutafakari mapendekezo haya, Kamati ya Uandishi ilizingatia pia Sheria ya Bahari ya Himaya na Ukanda Maalum wa Kiuchumi Baharini, Sura ya 238 *(The Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act, Cap. 238)* inayotawala masuala ya mipaka ya bahari. Katika kipengele cha pili cha Jedwali la sheria hiyo, imetamkwa kuwa eneo la bahari linajumuisha eneo la anga la bahari *(air space),* kitanda cha bahari *(sea bed),* na eneo la chini ya ardhi ya bahari *(sub soil)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kujiridhisha na masharti ya sheria hiyo, iliona kwamba hakuna umuhimu wa kuandika upya Ibara hii kwa kuainisha kila kipengele cha mipaka ya bahari kama ilivyopendekezwa na Kamati za Bunge, kwani yote hayo yanapaswa kuzingatiwa katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imechambua maudhui ya Ibara hii na kuona kwamba kuna umuhimu wa kumpa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kuigawa nchi katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengine kwa madhumuni ya kurahisisha shughuli za kiutawala ikiwemo kuweka masharti ya kumwezesha kukasimu mamlaka ya kuigawa nchi kwa upande wa Zanzibar kwa Rais wa Zanzibar, kama atakavyoona inafaa. Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi imeongeza Ibara ndogo mpya ya (2) inayofafanua masharti hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeongeza ibara ndogo mpya ya (3) kwa kutoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria itakayoainisha na kufafanua mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa suala la ubainishaji na uwekaji wa mipaka ni la kitaalam na utekelezaji wake unahitaji muda wa kutosha, hivyo haliwezi kujumuishwa kwenye Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia utafiti huu wa kisheria pamoja na maboresho mengine, Ibara hii imeandikwa upya na itakuwa na Ibara ndogo ya (1), (2) na ya (3) kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 2 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

2.2 IBARA YA 3: Alama na Sikukuu za Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii, Kamati sita kati ya Kamati Kumi na mbili zilipendekeza kufanya marekebisho kwenye Ibara ya (3)(1) kwa kuongeza aya mpya ya (d) kwa ajili ya kuongeza maneno "na maadhimisho" ili mbali na Sikukuu za Taifa zilizoainishwa katika Ibara hii, kuwepo pia na maadhimisho mengine ya kitaifa. Mapendekezo haya pia yalijitokeza katika mijadala ya Bunge Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilitafakari na kuzingatia maudhui ya Ibara hii na kuona kuwa maudhui ya Ibara hii yanahusu "Sikukuu za Taifa" na siyo "maadhimisho" ya kitaifa. Aidha, kwa sababu ibara ndogo ya (2) (d) imeweka utaratibu wa kutambua Sikukuu nyingine za kitaifa kama zitakavyoainishwa na sheria za nchi, Kamati inaona kwamba maadhimisho mengine yanayopendekezwa yanapaswa kuzingatiwa kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo**,** Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 3 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

2.3 IBARA YA 4: Lugha ya Taifa na Lugha za Alama

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii, Wajumbe wa Kamati zote walipendekeza kuandikwa kwa ibara ndogo mpya ya (3) ambayo itaruhusu lugha ya alama na lugha ya alama mguso kutumika kama lugha rasmi ya mawasiliano kwa viziwi na viziwi wasioona. Mapendekezo hayo yalilenga kuzitambua Kikatiba lugha hizo ili ziwe lugha rasmi za mawasiliano kwa watu wenye mahitaji hayo. Marekebisho hayo yalihusu kuongeza maneno "lugha za alama mguso" katika ibara ndogo ya (3) ili kuwianisha Ibara hiyo na Ibara ndogo mpya. Aidha, kwa mantiki hiyo, Kamati imeongeza ibara ndogo mpya ya (3) na iliyokuwa Ibara ndogo ya (3) itasomeka kama Ibara ndogo ya (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na marekebisho hayo, Kamati nyingi zilipendekeza lugha ya Kiswahili itumike kama lugha rasmi ya mawasiliano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuongeza maneno "**Bunge na Mahakama**".

Hata hivyo, baada ya kutafakari kwa makini suala hili na kwa kuzingatia utamaduni wa uandishi wa sheria, Kamati ya Uandishi iliona kwamba neno "**Kiserikali**" lililopo kwenye Rasimu

ya Katiba, linajumuisha Bunge na Mahakama. Kwa mantiki hiyo, hakuna haja ya kuongeza maneno hayo kwenye Ibara hii ndogo kwa kuwa kimsingi maudhui hayo yameshazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maboresho katika Ibara hii, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 4 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

2.4 IBARA YA 5: Tunu za Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zote kumi na mbili zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza Tunu nyingine. Miongoni mwa Tunu zilizoongezwa ni "**amani na utulivu**", "**haki na usawa wa binadamu**" na "**usawa wa jinsia**". Kamati hizo zilipendekeza "**lugha ya Taifa**" iliyoainishwa kama Tunu isomeke kama "**Lugha ya Kiswahili**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilijadili maudhui ya Ibara hii hususan matumizi ya neno "**Tunu**" ili kubaini kama mambo yaliyoorodheshwa katika Ibara hiyo yanakidhi kuwa Tunu za Taifa. Kamati ilitafiti zaidi kuhusu maana ya neno "Tunu" na kubaini kuwa sio kila jambo lililoorodheshwa katika Ibara hii lina hadhi ya kuwa Tunu. Mambo mengine kama vile, uwazi, uwajibikaji, uadilifu, demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi, utawala wa sheria, umoja wa kitaifa, uzalendo, haki

za binadamu na usawa wa kijinsia yanaonekana kuwa siyo Tunu bali misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tunu na misingi ya utawala bora ni mambo mawili tofauti, Kamati inapendekeza kuifuta Ibara ya 5 na kuiandika upya kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 5 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa. Aidha, kuongeza Ibara mpya ya 6 inayoweka masharti ya misingi ya utawala bora kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 6 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

2.5 IBARA YA 6: Mamlaka ya Wananchi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tisa kati ya Kamati kumi na mbili zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo. Kamati tatu zilipendekeza marekebisho katika aya ya (b) kwa kuongeza maneno "**wote bila ubaguzi**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge Maalum na kuona kuwa maudhui katika aya ya (b) yanajitosheleza. Hivyo, aya hiyo ni muhimu kubaki kama ilivyo. Hata hivyo, Kamati ya Uandishi iliifanyia Ibara hii maboresho ya kiuandishi kwa kuondoa maneno ya utangulizi ambayo yalionekana siyo ya lazima na kuipanga upya ili isomeke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine ya kutafakari Ibara hii, Kamati ililinganisha maudhui ya Ibara hii na yale ya Ibara ya 68(1) na kubaini kuwa Ibara zote mbili zina maudhui yanayofanana yanayohusu mamlaka ya wananchi. Kamati ya Uandishi katika kuifanyia kazi Ibara hii, imehamisha maudhui ya Ibara ya 68(1) na kuyaweka katika Ibara mpya ndogo ya (2) ya Ibara hii kwa lengo la kuwianisha maudhui ya Ibara hizo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maboresho hayo, Ibara hii ya 6 imeandikwa upya na itakuwa na Ibara ndogo za (1) na (2) kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 7 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

2.6 IBARA YA 7: Watu na Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Watu na Serikali. Kamati zote zilipendekeza marekebisho ya kimaudhui. Kwenye ibara ndogo ya (1) Wajumbe walipendekeza kufuta maneno "**Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano**" na badala yake kuweka maneno "**Mamlaka ya Nchi**" au neno "**Serikali**". Aidha, sababu ya kufuta maneno hayo ni kuwa maneno "**Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano**" hayaendani na maudhui ya Ibara hii kwa kuwa yanahusiana na wajibu na malengo ya Serikali na sio wajibu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ndogo ya (2) Kamati zilitoa mapendekezo mbalimbali ya marekebisho kama ifuatavyo:

(a) kufuta maneno "**kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine**" katika ibara ndogo ya (2)(c) na badala yake yaandikwe "**kuzuia unyonyaji wa aina yoyote**" au "**kuzuia dhuluma ya aina yoyote**";

(b) kuzingatia masuala ya umiliki na mgawanyo wa ardhi;

(c) kuongeza neno "**ulemavu**" katika Ibara ndogo ya (2)(g); na

(d) kuongeza maneno "ukatili na udhalilishaji" katika ibara ndogo ya (2)(h).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilitafakari mapendekezo ya Kamati zote na kuwianisha mapendekezo hayo kwa lengo la kufanya maboresho katika Ibara hiyo. Katika zoezi hilo, Kamati ya Uandishi ilifanya maboresho mengine ya kiuandishi katika Ibara ya 7(2) (b), (c), (d), na (j) kwa kufuta baadhi ya maneno katika aya hizo ili ziweze kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii, Kamati tano kati ya kumi na mbili zilipendekeza masuala ya umiliki na mgawanyo wa ardhi kwa uwiano yazingatiwe katika ibara ndogo ya (2). Aidha, wakati wa mjadala Wajumbe wengi walipendekeza kuongezwa kwa Sura mpya inayohusu ardhi kwenye Rasimu

ambayo itaweka misingi ya umiliki na utumiaji wa ardhi. Kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeongeza Sura mpya ya Tatu inayohusu Ardhi, Maliasili na Mazingira kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzingatia mapendekezo na maboresho yote katika ibara ndogo ya (1) na ya (2), Ibara hii imerekebishwa kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 8 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

2.7 IBARA YA 8: Ukuu na utii wa Katiba

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii, Kamati sita kati ya Kamati kumi na mbili zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati nyingine sita zilipendekeza marekebisho yafuatayo:

(a) kuongeza maneno katika Ibara ndogo ya (1) "kwa kadri yatakavyohusika na Mambo ya Muungano kama yalivyoorodheshwa katika Nyongeza ya Katiba hii" mwishoni mwa Ibara hii;

(b) kujumuisha Katiba ya Zanzibar katika masharti ya Ibara ndogo ya (2) inayohusu utii wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(c) kuongeza Ibara mpya ndogo ya (3) inayotambua ukuu wa Katiba ya Zanzibar katika mambo yasiyo ya Muungano kwa upande wa Zanzibar;

(d) kufutwa kwa Ibara ndogo ya (5) na kuiandika upya ili pamoja na mambo mengine kuweka wajibu kwa kila mwananchi kuifahamu Katiba;

(e) kuongeza Ibara ndogo mpya ya (6) inayohusu Katiba kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu; na

(f) kuongeza Ibara mpya ndogo ya (7) inayotoa haki ya kufungua shauri Mahakama Kuu endapo itatokea ukiukwaji wa Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilizingatia mapendekezo ya Kamati za Bunge Maalum na maoni yaliyotolewa kwenye mijadala kuhusu kuboresha maudhui ya Ibara hii. Baadhi ya mapendekezo yalionekana kuwa hayatekelezeki, yanamaudhui ya kiutawala zaidi na mengine yalionekana yanafaa kuzingatiwa kwenye Ibara nyingine.

Aidha, katika Ibara ndogo ya (2), Kamati za Bunge Maalum zilipendekeza Katiba ya Zanzibar ijumuishwe katika masharti ya kuzingatia na kutii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati ya Uandishi ilitafakari pendekezo hili na kuona kuwa, hakuna haja ya kuyachukua mapendekezo hayo kwa kuwa maudhui yaliyopo katika Ibara hii yanajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ndogo ya (3), Kamati mbalimbali zilikuwa na mapendekezo ya kuongeza Ibara ndogo mpya ya (3) na kuiboresha iliyokuwa Ibara ndogo ya (3) katika Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ili kuleta maudhui yanayokusudiwa. Kamati ya Uandishi ilitafakari pendekezo hili linalotaka kuongeza Ibara ndogo mpya ya (3) inayotambua ukuu wa Katiba ya Zanzibar na kuridhika kwamba Katiba ya Zanzibar inajitosheleza yenyewe. Aidha, Kamati ya Uandishi imeboresha maudhui ya Ibara ndogo ya (3) ya Rasimu na kuiandika upya kama inavyoonekana kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ndogo ya (4), Kamati ilitafakari na kujadili masharti ya vyombo vya uamuzi au mtu binafsi kufanya uamuzi kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii. Kamati ya Uandishi ina maoni kuwa Ibara ndogo ya (4) inahusu masharti ya vyombo vyenye mamlaka ya kutoa uamuzi na sio mtu binafsi. Aidha, masharti yanayomhusu mtu binafsi yamezingatiwa kwenye ibara ndogo ya (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ndogo ya (5) Kamati ilijadili na kufanya maboresho ya kiuandishi kwa kuongeza neno “hii” mwishoni mwa Ibara ndogo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ndogo mpya ya (6) Kamati zilipendekeza kuanzishwa kwa ibara ndogo mpya ya (6) inayompa mtu haki ya kufungua shauri Mahakamani endapo kutakuwa na ukiukwaji wa sharti lolote la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maboresho kama yalivyofafanuliwa kwa kila ibara ndogo hapo juu, Kamati ya Uandishi haikuzingatia mapendekezo yaliyotolewa isipokuwa imeyaelekeza maudhui hayo katika sehemu inayohusu haki za binadamu na imefanya maboresho ya kuiandishi na kuiandika upya kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 9 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

2.8 IBARA YA 9: Hifadhi ya Utawala wa Katiba

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zote kumi na mbili zimependekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo hayo na kuona kuwa hakuna haja ya kuifanyia marekebisho Ibara hii na hivyo kupendekeza isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 10 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA PILI

MALENGO MUHIMU, MISINGI YA MWENENDO WA SHUGHULI ZA SERIKALI NA SERA ZA KITAIFA

3.0 **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati ya Uandishi ilipokuwa inajadili mapendekezo ya Kamati mbalimbali, ilibaini kwamba Kamati hizo za Bunge Maalum pamoja na mjumbe mmoja mmoja walikuwa na mapendekezo mengi ya kuiboresha Sura hii. Mapendekezo hayo yalilenga kuongezwa kwa Ibara mpya zinazohusu malengo ya Taifa katika nyanja ya siasa, utamaduni, uchumi na jamii. Mapendekezo hayo pia yalilenga kuongezwa Ibara mpya zinazohusu utafiti na maendeleo, Dira ya Taifa ya Maendeleo na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyachambua kwa kina mapendekezo hayo, imeyaafiki mapendekezo hayo kwa kuwa ni ukweli usiopingika kwamba, roho ya nchi yoyote ile ni ustawi wa kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa wananchi wake. Mapendekezo hayo yanalenga kuweka msingi imara utakayowezesha jamii kustawi kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ya kuyaafiki mapendekezo hayo ni kuungwa mkono kwa mapendekezo hayo na Wajumbe wengi wakati wa mijadala ndani ya Bunge

Maalum. Takriban Wajumbe wote waliochangia Sura hii waliyaunga mkono mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Sura hii kama inavyosomeka kwenye Ibara za 11 hadi 21 za Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa. Sura hii kama ilivyoandikwa upya itakuwa na sehemu zifuatazo:

(a) Malengo makuu;
(b) Malengo ya kisiasa;
(c) Malengo kiutamaduni;
(d) Malengo ya kiuchumi na kijamii; na
(e) Utafiti, Dira ya maendeleo, mipango na utekelezaji wa malengo ya Taifa.

SURA MPYA

SURA YA TATU
ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mbalimbali za Bunge Maalum zilipendekeza Rasimu ya Tume ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza Sura mpya. Miongoni mwa Sura zilizopendekezwa kuongezwa ni Sura inayohusu Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyachambua mapendekezo hayo, imeridhia kuongezwa Sura mpya inayohusu ardhi, maliasili na mazingira. Sababu za kuridhia kuongeza sura hii ni umuhimu wa ardhi, maliasili na mazingira katika maendeleo ya nchi. Aidha, ni ukweli usiopingika kuwa, ardhi, maliasili na mazingira vinagusa maisha ya kila siku ya watanzania walio wengi wakiwemo wanawake na wanaume ambao ni wafugaji, wakulima, wavuvi na wachimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ambayo ardhi yake haisimamiwi vizuri, hukumbwa na migogoro ya mara kwa mara na wakati mwingine hupatwa na mauaji yatokanayo na migogoro. Kuwa na Sura hii mpya inayohusu ardhi itasaidia kuondoa migogoro ya ardhi kupitia sheria itakayotungwa na Bunge na kwa kutumia misingi ambayo inayowekwa katika Katiba na hivyo kuweka utaratibu mzuri wa Kisheria wa kusimamia ardhi kwa ajili ya maendeleo ya nchi na wananchi.

Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza uwepo kwa aya ya (d) katika Ibara ndogo ya (2) itakayolinda haki za kila mwanamke ili aweze kupata haki ya kumiliki, kutumia, kuendeleza na kusimamia ardhi kwa masharti yale yale kama ilivyo kwa wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura mpya inayohusu Ardhi, Maliasii na Mazingira inapendekezwa iwe Sura ya Tatu ya Rasimu ya Katiba inayopendekezwa na ina Ibara zinazohusu Ardhi katika Jamhuri ya Muungano, Matumizi bora ya Ardhi, Fidia, Maliasili na Mazingira. Aidha, Sura hiyo inasomeka kama inavyoonekana kwenye Ibara za 22 hadi 26 za Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA TATU
MAADILI NA MIIKO YA UONGOZI NA UTUMISHI WA UMMA

SEHEMU YA KWANZA
MAADILI YA UONGOZI NA UTUMISHI WA UMMA

4.0 IBARA YA 13: Dhamana ya Uongozi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Dhamana ya Uongozi wa Umma. Kamati kumi kimsingi zilikubaliana na maudhui ya Ibara hii na kupendekeza maboresho machache yakiwemo kurekebisha makosa ya kiuandishi katika aya ya (a) ya Ibara ndogo ya (1). Katika Ibara ya (2) kuweka maudhui yanayozingatia usawa wa kijinsia, kuondoa ubaguzi katika aya ndogo ya (c) na pendekezo lingine la kuifuta Ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya. Aidha, Kamati mbili kati ya kumi na mbili zilipendekeza Ibara hiyo ifutwe na kuandikwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo ya Kamati mbalimbali na Wajumbe katika mjadala, walipendekeza kwamba, ibara ndogo (2) ifutwe na kuandikwa upya ili kuhakikisha muktadha wa Ibara hii unaweka sharti la viongozi waliopewa dhamana ya uongozi wa umma kufanya maamuzi kwa kuzingatia Katiba ya nchi, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Aidha, Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho madogo ya kiuandishi katika Ibara ndogo ya (1) aya ya (a)(ii) ili kuleta mtiririko mzuri wa lugha.

Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo hayo, imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 27 Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

4.1 IBARA YA 14: Kanuni za Uongozi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kanuni za Uongozi wa Umma. Kamati nyingi zimependekeza marekebisho mbalimbali ikiwemo kuacha Ibara nyingine zibaki kama zilivyo kwenye Rasimu na kufanyiwa marekebisho madogo, kufuta na kuandika upya Ibara ndogo ya (2) na kufuta neno "**viongozi**" na badala yake kuweka neno "**Kiongozi**" na neno "**na**" lisomeke "**au**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo haya inaona kuna umuhimu wa kuifanya marekebisho Ibara hii ili maudhui yake yaweze kueleweka ipasavyo. Aidha, inapendekezwa aya (b) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe kwa kuwa sharti hilo linatakiwa kujumuishwa kwenye sheria. Kamati ya Uandishi imeona kuna haja yakujumuisha maudhui ya Ibara ya 15 hadi ya 20 zinazohusu zawadi katika utumishi wa umma, akaunti nje ya nchi na mikopo, wajibu wa kutangaza mali na madeni, masharti ya jumla kuhusu miiko na maadili ya viongozi wa umma, mgongano wa maslahi, matumizi ya mali ya umma, na utekelezaji wa masharti ya maadili zijumuishwe kwenye Ibara moja ili kuweza kuipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria juu ya

mambo hayo. Lengo la maboresho ni kuhamishia masuala haya kwenye sheria za nchi kutokana na ukweli kwamba yanabadilika mara kwa mara kutokana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo hayo, inapendekeza Ibara hii iandikwe upya kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 28 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SEHEMU YA PILI
MIIKO YA UONGOZI WA UMMA

4.2 IBARA YA 21: Utii wa Miiko ya Uongozi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Miiko ya Uongozi wa Umma. Kamati mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba, Kamati tano zimependekeza Ibara hii ifutwe kwa kuwa masuala yanayohusu miiko na maadili ya uongozi wa umma yanapaswa kuainishwa katika sheria za nchi badala ya kujumuishwa kwenye Katiba na Kamati tano zilizobaki zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kuongeza na kufuta baadhi ya maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo inaona kuna haja ya kuiandika upya Ibara hii ili maudhui ya miiko na maadili ya uongozi wa umma yaweze kueleweka kwa urahisi na masharti yake yaweze kuzingatiwa katika sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzingatia maoni na mapendekezo ya Kamati mbalimbali na mijadala ya Bungeni, Kamati ya Uandishi inapendekeza kufuta na kuiandika upya Ibara hii ili kubainisha miiko ya msingi katika uongozi wa umma na kuacha mambo mengine ya kiutendaji yazingatiwe katika Sheria itakayotungwa na Bunge. Sababu ya mapendekezo haya ni kuwa, maudhui ya Ibara hii ya Rasimu ya Tume, yanaelezea mambo mengi yakiutendaji na kiutawala ambayo ni muhimu yakaainishwa katika Sheria zitakazotungwa na Bunge ili kurahisisha utekelezaji pindi kunapotokea mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ufafanuzi huo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 29 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

4.3 IBARA YA 22: Marufuku baadhi ya vitendo

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Ibara hii inayohusu marufuku kwa baadhi ya vitendo, jumla ya Kamati tisa zilipendekeza Ibara hii ifutwe kwa kuwa maudhui yake yanapaswa kuzingatiwa katika sheria za nchi. Aidha, Kamati moja ilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Katiba, Kamati nyingine moja ilipendekeza Ibara hii ifutwe na iandikwe Ibara mpya inayohusu Tume ya Maadili na Viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo ya kujumuisha masharti kuhusu marufuku kwa baadhi ya vitendo ambavyo mtumishi wa umma hastahili kuvitenda pale anaposhika madaraka au kugombea nafasi ya madaraka ya aina yoyote kwenye chama cha siasa. Aidha, mapendekezo yaliyotolewa kuhusu kuundwa kwa Ibara mpya inayohusu Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ni maoni ya Kamati ya Uandishi kuwa maudhui ya masuala hayo yanapaswa kuzingatiwa kwenye Sura itakayozungumzia Taasisi za uwajibikaji.

Hivyo, Kamati inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza na itasomeka kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 30 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURAYA NNE
HAKI ZA BINADAMU, WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI

SEHEMU YA KWANZA
HAKI ZA BINADAMU

5.0 IBARA YA 23: Uhuru, utu na usawa wa binadamu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru, utu na usawa wa binadamu. Kamati tisa zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyopendekezwa kwenye Rasimu ya Tume kwa sababu maudhui yake yanajitosheleza. Kamati tatu zimetoa mapendekezo ya kuongeza maneno **"mbele ya sheria"** kwenye ibara ndogo ya (1) ili kuleta dhana ya usawa mbele ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inaona kuwa maudhui yaliyomo kwenye Ibara hii, kama ilivyopendekezwa kwenye Rasimu yanajitosheleza. Hivyo, inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 31 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.1 IBARA YA 24: Haki ya kuishi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya kuishi. Kamati saba zimependekeza Ibara hii ibaki kama inavyopendekezwa kwenye Rasimu ya Tume. Aidha, Kamati nne zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza Ibara ndogo mpya mbili kwa ajili ya kutoa wajibu wa kuhifadhi maiti na

nyingine kwa ajili ya kuweka muktadha wa haki ya kuishi kuanzia ujauzito wa siku ishirini tangu kutungwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na mijadala ndani ya Bunge na kuridhika kwamba maudhui yaliyomo katika Rasimu yanajitosheleza. Kamati ya Uandishi inaona kuwa mapendekezo ya kuongeza Ibara ndogo mpya inayohusu haki ya kuhifadhi maiti hayaendani na maudhui ya Ibara hii kwa kuwa Ibara hii inazungumzia haki ya mtu ambaye yupo hai. Aidha, Kamati ya Uandishi inaridhika kwamba maudhui ya Ibara hii yanamlinda mama pamoja na mtoto aliyemo tumboni mwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 32 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.2 IBARA YA 25: Marufuku kuhusu ubaguzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu marufuku kuhusu ubaguzi. Kamati tano zimependekeza Ibara hii ifutwe, Kamati moja imependekeza, Ibara hii isomeke kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Aidha, Kamati sita zimependekeza marekebisho mbalimbali yakiwemo kuyafuta na kuyaandika upya Maelezo ya Pembeni ili yasomeke "**haki ya kutobaguliwa**", kufuta maneno "**mbele ya sheria**" katika ibara

ndogo ya (1), kufuta ibara ndogo ya (3) mpaka ya (7) na kuongeza aya mpya ya (g) inayohusu utoaji huduma ya sheria kwa wasioweza kumudu gharama za uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo hayo na kuona kuwa Ibara hii inaainisha suala muhimu la haki ya kutokubaguliwa. Hivyo, imeona maudhui yaliyomo kwenye Ibara hii yanajitosheleza. Hata hivyo, imefanya marekebisho kwa kuyafuta na kuyaandika upya Maelezo ya Pembeni ili yasomeke "**haki ya kutobaguliwa**" kwa kuwa sehemu hii inazungumzia haki za binadamu. Pia, imeongeza maneno "**utu wake**" kwenye ibara ndogo ya (7) mwishoni mwa aya ya (f) ili kuboresha maudhui ya aya hiyo. Aidha, Kamati imefanya maboresho madogo ya kiuandishi kwenye Ibara hii kwa ujumla ili kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi na kimaudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mapendekezo hayo, Kamati inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 33 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.3 IBARA YA 26: Haki ya kutokuwa mtumwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maudhui ya Ibara hii yanalenga kukomesha biashara ya binadamu na utumwa pamoja na vitendo vyovyote vinavyoendana na biashara hiyo. Kamati Saba hazikutoa mapendekezo yoyote, Kamati tano

zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali na kuandika upya ibara ndogo ya (1), kuunganisha ibara ndogo ya (1) na ya (2) pamoja na kuongeza ibara ndogo ya (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inaona kuwa maudhui yaliyomo katika Ibara hii yanajitosheleza na inakubaliana na marekebisho madogo kwa ajili ya kuboresha maudhui yanayotolewa. Marekebisho hayo ni kufuta aya ya (b) katika ibara ndogo ya (1) na kubadili mpangilio kwa kuifanya aya ya (c) kuwa (b) na kufanya marekebisho ya kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 34 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.4 IBARA YA 27: Uhuru wa mtu binafsi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru wa mtu binafsi. Kamati zote kumi na mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwa sababu maudhui yake yanajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo ya Kamati zote za Bunge na inapendekeza ibaki kama ilivyo kwenye Ibara ya 35 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.5 IBARA YA 28: Haki ya faragha na usalama wa mtu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya faragha na usalama wa mtu. Kamati nane zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Aidha, Kamati nne zimependekeza kufanya marekebisho mbalimbali kwa kufuta maneno "**kutoteswa au kudhalilishwa**" na kuongeza maneno "**kwa kuzingatia sheria za nchi**" katika ibara ndogo ya (1) pamoja na mapendekezo ya kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuifuta Ibara hii yote na kuiandika upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo imefanya marekebisho ya kimaudhui kwenye ibara ndogo ya (1) kwa kufuta maneno "**nyumbani kwake**" na badala yake kuweka maneno "**unyumba wake**" na kufuta maneno "**kutoteswa au kudhalilishwa**" kutokana na kwamba maudhui ya maneno haya yamezingatiwa katika Ibara nyingine.

Vile vile, katika Ibara ndogo ya (2), Kamati imeongeza maneno "**kwa mujibu wa Ibara hii**" baada ya neno "**mtu**" lililopo kwenye mstari wa kwanza na hivyo kuiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 36 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.6 IBARA YA 29: Uhuru wa mtu kwenda anakotaka

Mheshimiwa mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru wa mtu kwenda anakotaka. Kamati nane zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, Kamati nne zimetoa mapendekezo kwa ajili ya kuboresha maudhui ya Ibara hii, ikiwemo kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) ambayo itakayoweka maudhui ya itazingatia mila chanya na desturi za sehemu husika na sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya kuongeza ibara ndogo ya (3) kuhusu uzingatiaji wa mila chanya na desturi za sehemu husika na kuona kuwa maudhui ya Ibara hiyo ndogo mpya inayopendekezwa hayaendani na maudhui ya Ibara hii ambayo yanahusu uhuru wa mtu kwenda anapotaka. Hivyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke kama Ibara ya 37 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.7 IBARA YA 30: Uhuru wa Maoni

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru wa maoni. Kamati mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati kumi zimetoa mapendekezo mbalimbali ya kiuandishi ya kuongeza na kupunguza baadhi ya maneno yanayohusu masuala yanayohatarisha usalama

wa nchi na uhujumu uchumi, na makosa yanayotendeka kwa njia ya mtandao na ilipendekezwa yawekwe kwenye aya (c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilitafakari mapendekezo hayo, na imeona hakuna haja ya kuongeza aya mpya ya (c) kwa kuwa, aya hii inazungumzia masuala yanayohatarisha usalama wa nchi, uhujumu uchumi na makosa yanayotendeka kwa njia ya mtandao na kuona kuwa kimsingi Ibara hii inatoa uhuru na haki ya maoni kwa kila mtu na haizungumzii masuala yanayohusu usalama wa nchi. Hivyo, si vyema kuyajumuisha masuala hayo katika Ibara hii. Vile vile, maneno "**propaganda kuhusu"** yabadilishwe na badala yake yaandikwe "**kuchochea**" na kufuta neno "**ushawishi"** na badala yake kuandika neno "**kuchochea"** katika ibara ndogo ya (2) aya ya (b).

Kwa mantiki, hiyo Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 38 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.8 IBARA YA 31: Uhuru wa habari na vyombo vya habari

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru wa habari na vyombo vya habari. Katika Ibara ya 31, Kamati moja ilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu na Kamati kumi na moja zimependekeza marekebisho kwenye

maeneo mbalimbali kwa kuongeza aya mpya na maneno ambayo Kamati hizo na mijadala iliona kuna haja ya kupanua dhana na uhuru wa habari na vyombo vya habari, kuweka mipaka ya uhuru huo kwa kuzingatia sheria za nchi na kufuta na kuandika upya Ibara hii ili kuliwezesha Bunge kutunga sheria kwa ajili ya kutekeleza wajibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati nyingine zilipendekeza nyongeza ya maneno ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mifumo rafiki inayokidhi mahitaji ya mawasiliano kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imezingatia pendekezo la kuwapa wajibu waandishi wa habari na vyombo vya habari kutoa kwa umma habari na taarifa sahihi na za kweli, kuweka mfumo unaokidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu ikiwemo kuzingatia miiko ya taaluma ya uandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara ndogo ya (3) ifutwe kwa kuwa wajibu wa Serikali, asasi za kiraia, taasisi za dini na watu binafsi wa kutoa habari sahihi kwa umma, umeshazingatiwa katika ibara ndogo ya (4) ya Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, kwenye Ibara ndogo ya (4), Kamati ya Uandishi imeifanyia marekebisho kwa kulipa mamlaka ya Bunge ya kutunga sheria kwa ajili ya kusimamia na kulinda haki, wajibu, uhuru wa vyombo vya habari na waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haijazingatia hoja ya kuongeza aya mpya ya (c) na (d) kuhusu usimamiaji na upatikanaji wa habari na wajibu wa vyombo vya habari na wanahabari, kwa sababu masuala hayo yamezingatiwa katika Ibara hii. Hivyo basi, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 39 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.9 IBARA YA 32: Uhuru wa imani ya dini

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru wa imani ya dini. Kamati tano zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Katiba na Kamati saba zimependekeza marekebisho ya kuongeza maneno na kufuta baadhi ya maneno, kufuta na kuandika upya Ibara ndogo ya (1) na kuongeza Ibara ndogo mpya za (8) na (9) ili kuweza kuweka mazingira ya upatikanaji na utekelezaji wa sheria mbalimbali kuhusu kuanzisha na kuendesha Jumuiya na taasisi za kidini. Aidha, mapendekezo mengine yalilenga kuweka katazo la kutumia uhuru wa imani ya dini kukashifu imani au dini ya mtu

mwingine na katazo la watu kutumia dini kudhalilisha utu wa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kutafakari mapendekezo hayo imeona kwamba, kuna haja ya kubadilisha neno 'anao" kuwa "ana" kwenye Ibara ndogo ya (1) ili kuboresha maudhui kuhusiana na uhuru wa imani ya dini.

Aidha, maudhui ya ibara ndogo (5) yanazuia mtu au kikundi cha watu kukashfu dini ya mtu au watu wengine. Vile vile, suala la Bunge kutunga sheria ya utekelezaji na upatikanaji wa sheria mbalimbali za dini nalo limeshazingatiwa katika Ibara ndogo ya (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 40 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.10 IBARA YA 33: Uhuru wa mtu kujumuika na kushirikiana na wengine

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru wa mtu kujumuika na kushirikiana na watu wengine. Kamati zote kumi na mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu. Hata hivyo, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari pendekezo hilo, imeona kuna haja ya kufanya marekebisho

madogo ya kiuandishi ya kufuta maneno "**na hasa zaidi**" na kuongeza maneno **"na kwa ajili hiyo"** ili kuboresha maudhui ya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 41 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.11 IBARA YA 34: Uhuru wa kushiriki shughuli za umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru wa kushiriki shughuli za umma. Kamati zote zilipendekeza Ibara ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Katiba kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza.

Kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati zote, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara hii ifanyiwe marekebisho madogo na isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 42 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.12 IBARA YA 35: Haki ya kufanya kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya kufanya kazi. Kamati tano zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu. Kamati saba zimependekeza marekebisho mbalimbali ya kimaudhui na kiuandishi kwa kuongeza maneno na kufuta baadhi ya maneno. Aidha Ibara ndogo ya (2) ilipendekezwa ifutwe na kuandikwa upya kwa lengo la kuzuia

raia wa kigeni kushika nafasi za umma ambazo ni mahususi kwa ajili ya raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekeo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuna haja ya kufanya marekebisho kwenye Ibara ndogo ya (1) kwa kuongeza maneno na "kupata ujira anaostahili" na kwenye Ibara ndogo ya (2) kwa kufuta neno "mtu" na badala yake kuweka neno "raia" ili kutoa fursa sawa na haki kwa raia kushika nafasi yoyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi.

Kwa mantiki hiyo Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 43 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.13 IBARA YA 36: Haki za Wafanyakazi na Waajiri

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki za wafanyakazi na waajiri. Kamati mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu. Kamati nyingine kumi zimependekeza kuifanyia marekebisho mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Ibara hii. Miongoni mwa mapendekezo hayo ilikuwa ni kuongeza aya mpya katika ibara ndogo ya (1) inayolenga kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vitendo vya udhalilishaji, kupata maelezo sahihi kuhusiana na kazi zao, na kupata mafao stahiki. Aidha, baadhi ya Kamati zilipendekeza kuwepo kwa haki ya kugoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Kamati zilipendekeza kutenganisha haki za wafanyakazi na waajiri kwa kuanzisha Ibara mpya inayohusu haki za waajiri, kwa kuwa haki na wajibu za wafanyakazi na waajiri zinatofautiana. Aidha, Kamati zilipendekeza kuanzishwa kwa Ibara mpya inayohusu haki za wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo kama ilivyo kwa makundi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyatafakari mapendekezo hayo na imekubaliana na mapendekezo ya Kamati za Bunge zinazohusu haki ya mkulima, mvuvi, mfugaji na mchimbaji mdogo. Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza kujumuishwa katika Ibara moja, haki za wafanyakazi na waajiri kwa kuwa kwa kiasi kikubwa zinafanana.

Aidha, katika Ibara ya 36 inayohusu haki za wafanyakazi Kamati imefanya maboresho kidogo kwa kuongeza aya mpya ya (e) kwenye ibara ndogo ya (1) inayowapa wafanyakazi hifadhi ya afya na usalama wao mahala pa kazi. Kutokana na mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 44 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.14 IBARA YA 37: Haki ya Kumiliki mali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya kumiliki mali. Kamati Tisa zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekibisho kwa kufuta na kuandika upya ibara ndogo za (1) na (2). Aidha, Kamati mbili zimependekeza kuongeza Ibara mpya ya 37A ambayo itatoa haki ya haki miliki bunifu kwa ajili ya kulinda kazi zinazotokana na utafiti, ugunduzi na ubunifu. Vile vile baadhi ya Kamati zilipendekeza kuongeza Ibara itakayohusu haki za wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo.

Baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo ya kuboresha Ibara ndogo ya (2) kwa madhumuni ya kutilia mkazo suala la kumiliki mali na ulipaji wa fidia inayolingana na thamani halisi ya soko. Aidha Kamati inaona kwamba suala la kuongeza Ibara mpya ya 37A itakayotoa haki ya haki miliki bunifu limezingatiwa kwenye Ibara ndogo ya (1) ya Ibara ya 37 ya Rasimu ya Katiba, kwa sababu kumiliki mali inajumuisha mali isiyoshikika na isiyohamishika. Hata hivyo, Kamati ya Uandishi imezingatia maoni ya kuwepo kwa ibara inayolinda hakimiliki bunifu na ugunduzi kwa kuongeza Ibara mpya ya 56.

Kwa msingi wa hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 45 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.15 IBARA YA 38: Haki ya uraia

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya uraia. Baadhi ya Kamati zilitoa mapendekezo ya kufanya maboresho katika Ibara hii kwa kufuta baadhi ya maneno na kuongeza Ibara ndogo mpya ya (2) kwa ajili ya kutoa haki ya kupata hati ya kusafiria kwa kila mtu.

Baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inaona kwamba maudhui yaliyomo katika Ibara hii yanahusu masuala ya Uraia na yanafanana na maudhui yaliyopo katika Sura inayohusu masuala ya Uraia. Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi, imeifuta Ibara hii na maudhui yake yamepelekwa kwenye sura ya sita.

5.16 IBARA YA 39: Haki ya mtuhumiwa na mfungwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya mtuhumiwa na mfungwa. Kamati Tisa zimependekeza marekebisho mbalimbali kwa ajili ya kuboresha maudhui ya Ibara hii ambayo yamelenga kutofautisha haki za mtu aliyewekwa chini ya ulinzi na haki za mtu anayetumikia kifungo, kuongeza lugha ya alama mguso na kuweka mazingira ya kuwatendea haki watu wa makundi mbalimbali walio chini ya ulinzi au kifungoni.

Baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi ilifanya maboresho ya kiuandishi kwa kuongeza Ibara ndogo mpya ya (3) na (4) kwa kuainisha haki anazostahili mtu anayetumikia kifungo ili kuendana na maelezo ya pembeni ya Ibara hii na kuzipa wajibu mamlaka za nchi kuzingatia masharti ya Ibara ya 25(7)(e) ya Rasimu wakati wa kutekeleza haki hizo. Ibara ndogo ya (3) imefanyiwa marekebisho kwa kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria badala ya mamlaka za nchi. Kutokana na marekebisho hayo, iliyokuwa Ibara ndogo ya (2) inapendekezwa kupangwa upya hivyo, itasomeka kama Ibara ndogo (3).

Aidha, kuhusu pendekezo la kuongeza matumizi ya lugha ya alama au alama mguso, halijazingatiwa kwa sababu lugha inayozungumzwa kwenye aya ya (a) inajumuisha lugha ya alama na alama mguso, kama zilivyozingatiwa kwenye Ibara nyingine za Rasimu ya Tume.

Kwa mantiki hiyo, Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 46 ya Rasimu hii.

5.17 IBARA YA 40: Haki ya watu waliyo chini ya ulinzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya mtu aliye chini ya ulinzi. Baadhi ya Kamati zilitoa mapendekezo ya kiuandishi kuhusu mpangilio wa maneno ili kukidhi maudhui ya

kuhusisha mikataba ya kimataifa. Aidha, ilipendekezwa kubadilisha maneno ya pembeni kwa kuyafuta na kuyaandika upya ili yasomeke "**haki za mtu aliye katika kizuizi**"

Kamati ya Uandishi, ilitafakari na kuzingatia mapendekezo ya maboresho ya maneno ya pembeni ili yaakisi maudhui ya Ibara hii. Kamati imeyafuta na kuyaandika upya maelezo ya pembeni ili yasomeke '**haki ya mtu aliye chini ya ulinzi au kizuizi**'. Aidha, Kamati inaona kwamba maudhui yaliyomo kwenye Ibarahii yanajitosheleza kwa sababu inahusu haki ya mtu aliye chini ya ulinzi au kizuizi. Vile vile, mpangilio wa maneno unajitosheleza kwa kuwa umeainisha masuala ya Mikataba ya kimataifa.

Kutokana na maelezo hayo, Kamati inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu na itasomeka kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 47 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.18 IBARA YA 41: Uhuru na haki ya mazingira safi na salama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uhuru na haki ya mazingira safi na salama. Kamati zote za Bunge zilikuwa na mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha maudhui ya Ibara hii, mapendekezo hayo yalilenga kuongeza maneno, kufuta ibara ndogo na kuandika upya ibara ndogo ya (2) na kuongeza ibara ndogo mpya za (4) na (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati pamoja na mijadala ya Bunge, Kamati ya Uandishi imejiridhisha kwamba ni muhimu iwepo ibara ndogo ya (4) ili kuliwezesha Bunge kutunga sheria kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya kuhifadhi mazingira, ushirikishwaji, udhibiti, ulinzi na usimamizi wake. Hata hivyo, maudhui kuhusu Ibara hii yameainishwa katika Ibara ya 64 inayohusu Bunge kutunga Sheria kuhusu utekelezaji wa haki, uhuru na wajibu ulioainishwa katika Sura hii. Kwa msingi huo hakuna haja yakuwepo kwa ibara ndogo ya (4).

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 48 ya Rasimu hii.

5.19 IBARA YA 42: Haki ya elimu na kujifunza

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya elimu na kujifunza. Kamati moja imependekeza Ibara ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu na Kamati kumi na moja zimependekeza marekebisho mbalimbali kwa kuongeza ibara ndogo ya (1)(e), Ibara ndogo ya (3) inayohusu miundo mbinu kwa ajili ya watu wenye ulemavu, kuongeza Ibara mpya zinazohusu uhuru, taaluma, ubunifu na ugunduzi haki, haki ya afya na haki ya afya chakula na lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imechambua mapendekezo hayo, na kuona kwamba ni muhimu iongezwe ibara ndogo mpya ya (4) itakayoweka masharti kwa Serikali ili kuhakikisha kunakuwepo mfumo wa elimu unaozingatia uwezo na mahitaji ya Taifa. Aidha, mfumo huo uwe unaotoa haki ya kupata elimu itakayomtayarisha mwanafunzi kikamilifu kwa ajili ya kuendelea na elimu kwa ngazi inayofuata au kumwezesha kujitegemea. Vile vile, mfumo huo utoe haki ya mtu kuchagua taaluma anayoitaka au anayoipenda kwa mujibu wa elimu na ujuzi alionao.

Aidha, mapendekezo kuhusu utoaji wa elimu bure, Kamati ya Uandishi ilikuwa na maoni kuwa suala hili linahusu utekelezaji zaidi wa sheria kwa kuwa Ibara hii inahusu haki ya elimu na kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 49 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.20 IBARA YA 43: Haki ya Mtoto

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya mtoto. Kamati mbili zimependekeza Ibara ibaki kama ilivyo katika Rasimu na Kamati kumi zimependekeza marekebisho mbalimbali yakiwemo kuongeza Ibara mpya inayohusu haki ya

afya, kufuta na kuandika upya na kuongeza Ibara ndogo mpya itakayotoa ufafanuzi wa umri wa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati pamoja na mijadala ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imekubaliana na baadhi ya mapendekezo kuhusiana na kuongeza na kufuta baadhi ya maneno. Kamati inapendekeza maneno yanayohakikisha haki ya ulinzi kwa mtoto dhidi ya utumikishwaji na mila potofu yaongezwe katika ibara ndogo ya (1) aya (b). Vile vile, kumuhakikishia mtoto haki ya kuwekewa mazingira bora kwa ajili ya kucheza na kupata elimu kwenye aya (c), kuongeza maneno yanayohakikisha mtoto anapata lishe bora, huduma ya afya, makazi na mazingira yatakayomjenga kiakili katika aya ya (e), kuongeza neno "**jamii**" kwa ajili ya kumuwezesha mtoto kupata haki ya malezi na ulinzi kutoka kwa jamii. Aidha, Kamati inapendekeza kuandikwa kwa ibara ndogo ya (3) itakayotoa tafsiri ya neno "**mtoto**" ambaye ni mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 50 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.21 IBARA YA 44: Haki na wajibu wa vijana

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu wajibu wa vijana. Kamati zote kumi na mbili zimependekeza marekebisho

mbalimbali ikiwemo kufuta maneno "**Serikali za Nchi Washirika**". Kamati hizo zinapendekeza ili haki hizi zitambuliwe kikatiba, ni vyema kuwe na chombo huru cha vijana, kitakachosimamia masuala ya haki na wajibu kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo inaona kuwa kuna haja ya kufuta maneno "**Nchi Washirika**" kwa sababu yanaashiria Muundo wa Serikali Tatu tofauti na muundo wa Serikali Mbili unaopendekezwa kwa sasa. Baada ya mapendekezo haya, Kamati ya Uandishi inaona ni vyema Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwani maudhui yaki yanajitosheleza.

Kwa kuzingatia maoni ya Kamati zote kumi na mbili, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 51 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.22 IBARA YA 45: Haki za watu wenye ulemavu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki za watu wenye ulemavu. Kamati tatu zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Katiba na Kamati tisa zilipendekeza marekebisho yaliyolenga kutoa haki mbalimbali kwa watu wenye ulemavu, zitakazowawezesha kuwa na haki ya kutumia lugha ya alama mguso, kupata huduma bora za afya, elimu, kulindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu na mila potofu, kutambuliwa na kushiriki na kushirikishwa katika masuala ya

uchaguzi. Baada ya uchambuzi wa mapendekezo ya Kamati na majadiliano Bungeni, Kamati ya Uandishi imeridhika kwamba upo umuhimu wa kutambua haki mbalimbali ambazo watu wenye ulemavu wanastahili.Kamati ya Uandishi inapendekeza kuongezwa maneno **"kulindwa dhidi ya vitendo vinavyoshusha utu wake**", kuongeza maneno katika ibara ndogo ya (1) aya ya (c) ili kuwawekea miundo mbinu na mazingira yanayofaa ya kuwawezesha kwenda wanapotakana Ibara ndogo ya (1) aya ya (d) kuongeza maneno "**alama ya mguso**" ili kuwawezesha kupata haki ya mawasiliano.

Kwa msingi wa hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza kufuta baadhi ya vifungu na kuboresha vingine na Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 52 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.23 IBARA YA 46:Haki za makundi madogo katika jamii

Mhehsimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki za makundi madogo katika jamii. Kamati nane zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu na Kamati moja imependekeza ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza ibara ndogo ya (4) inayotaja haki za wakulima, wafugaji na wavuvi. Kamati hiyo pia imependekeza iongezwe Ibara mpya inayoainisha haki za mtumiaji wa huduma. Aidha, Kamati

nyingine zilizobaki zimependekeza maboresho madogo ya kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekitim, baada ya kuyapitia mapendekezo yaliyowasilishwa na Kamati za Bunge Maalum pamoja na mijadala ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi imeboresha Ibara hii kwa kuongeza neno "**ya**" na neno "**maji**" katika ibara ndogo ya (2) ili kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi. Aidha imeona kwamba haki za wakulima, wafugaji na wavuvi ni muhimu kutambuliwa katika Katiba kama ambavyo imefafanuliwa katika lengo la Taifa la Kiuchumi.

Aidha, Kamati imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali kuhusiana na haki za mlaji ili kumlinda dhidi ya bidhaa na huduma ambazo hazina kiwango na ubora unaotakiwa pamoja na ulipwaji wa fidia kutokana na madhara anayoweza kupata kutokana na matumizi ya bidhaa zisizokidhi kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mapendekezo hayo Kamati inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 53 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.24 IBARA YA 47: Haki za wanawake

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki za wanawake. Kamati zote kumi na mbili zimependekeza Ibara hii iboreshwe kwa kuongeza haki za wanawake kupata afya ya uzazi

salama, kulindwa dhidi ya udhalilishaji, dhuluma, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia, mila potofu na kushiriki na kushirikishwa katika masuala ya uchaguzi na ngazi mbalimbali za maamuzi kwa uwiano ulio sawa na wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia maoni yaliyotolewa na Kamati mbalimbali za Bunge pamoja na mjadala Bungeni ikiwemo kuunda Ibara mpya itakayotambua haki za wanaume. Baada ya kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inaona ni muhimu kutambua haki za wanawake kwa ajili ya kuwalinda dhidi ya unyanyasaji wa aina zote ikiwemo mfumo dume na mila potofu zinazowakandamiza wanawake. Hivyo Kamati ya Uandishi imeboresha ibara ndogo ya (1) katika aya ya (a) kwa kuongeza maneno "**kuthaminiwa**" na "**kutambuliwa**", kuandika upya aya ya (b) na kuifuta aya ya (e) kwa madhumuni ya kulinda, kuheshimu, kuthamini na kutambua utu wa mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati haikukubaliana na mapendekezo ya kuongeza Ibara mpya inayoainisha haki za wanaumekwakuwa kwa sasa kundi hili si moja ya makundi ambayo yanakosa haki katika jamii. Kwa mantiki hii, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 54 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.25 IBARA YA 48: Haki za wazee

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki za wazee. Kamati tatu zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati tisa zimetoa mapendekezo mbalimbali yenye lengo la kuboresha haki za wazee. Marekebisho hayo ni kufuta baadhi ya maneno na kuyaandika upya, kuongeza aya za (e) na (f) katika ibara ndogo ya (1) na kuongeza Ibara mpya inayohusu mafao ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali na maoni ya Wajumbe wakati wa mjadala, Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho ya kimaudhui kwenye Ibara hiyo kwa kuyafuta maelezo ya pembeni na kuyaandika upya ili yasomeke "**stahiki za wazee**". Aidha, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kimaudhui katika aya za (a), (b), (c) na (d) kwa kuweka sharti kwa mamlaka ya nchi kuweka utaratibu utakaowezesha wazee kushiriki katika shughuli za kimaendeleo na kijamii na kupata huduma za matibabu pia kutoa ulinzi kwa wazee dhidi ya unyonyaji vitendo vya ukatili ikiwemo mateso na mauaji.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 55 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.26 IBARA YA 48A: Uhuru wa taaluma, ubunifu na ugunduzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati nyingi za Bunge zimependekeza kuanzishwa kwa Ibara mpya inayohusu uhuru wa taaluma, ubunifu na ugunduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imekubaliana na pendekezo hilo na imeanzisha Ibara mpya ya 48A inayohusu uhuru wa taaluma, ubunifu na ugunduzi ili kutoa fursa ya mtu kujifunza, kufundisha, kutafiti na kueneza matumizi ya matokeo ya utafiti kulingana na Kanuni za kitaaluma na za kiutafiti. Aidha, Serikali imepewa mamlaka ya kulinda haki miliki za ugunduzi na ubunifu ikiwa ni pamoja na haki za wabunifu na watafiti nchini kwa manufaa ya Taifa. Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuongezwa kwa aya mpya ya (f) inayoweka masharti kwa Serikali kukuza na kuendeleza utafiti inayoeleza **"mambo mengine yanayohusu ubunifu, ugunduzi na utafiti**"

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii mpya isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 56 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SEHEMU YA PILI
WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI NA MIPAKA YA HAKI ZA BINADAMU

5.27 IBARA YA 49: Wajibu wa Raia

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu wajibu wa raia. Kamati zote kumi na mbili zinakubaliana na maudhui ya Ibara kama ilivyo kwenye Rasimu, hata hivyo zimependekeza marekebisho mbalimbali kwa ajili ya kuboresha maudhui hayo. Marekebisho hayo ni ya kuongeza baadhi ya maneno, kufuta maneno na kuongeza aya mpya ya (h) katika Ibara ndogo ya (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo, imeiboresha ibara ndogo ya (1) aya ya (c) ili kuweka sharti kwa raia kulipa kodi kwa mujibu wa sheria za nchi. Aidha, aya ya (e) imefanyiwa marekebisho kwa kutoa wajibu wa raia kuilinda Jamhuri ya Muungano, inapendekezwa kufutwa kwa aya (f) na (g) pamoja na ibara ndogo ya (2) ili sharti la Bunge kutunga sheria za kusimamia sehemu hii kuwekwa mwishoni.

Baada ya mapendekezo hayo Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 57 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

IBARA YA 50: Wajibu wa kushiriki kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu wajibu wa kushiriki kazi. Kamati sita zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati sita zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kufuta na kuandika upya maneno na kurekebisha namba za aya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui yaliyomo katika Ibara hii ni ya muhimu hivyo Kamati ya Uandishi imeyazingatia kwa kuyaboresha na kufanya marekebisho kwa kuongeza maneno "**kwa mujibu wa sheria**" katika ibara ndogo ya (1) aya ya (b), kuongeza neno "**au kikatili**" katika ibara ndogo ya (2), kufuta maneno "**katiba hii**" katika ibara ndogo ya (3) na badala yake kuweka maneno "**Ibara ndogo ya (2)**" pamoja na neno "**kikatili**". Lengo la marekebisho hayo ni kuboresha maudhui kwa kuweka msisitizo kuhusu raia kushiriki kazi kwa kuzingatia sheria na kutopewa kazi za kutweza, shuruti au kikatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mapendekezo hayo Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 58 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

IBARA YA 51: Ulinzi wa Mali ya Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu ulinzi wa mali ya umma. Kamati tisa zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati tatu zimetoa mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha maudhui ya Ibara hii. Mapendekezo hayo ni kuongeza ibara ndogo mpya za (4) na (5) ambazo zitatoa masharti na wajibu wa kila raia kulinda maliasili za Taifa, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Taifa kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii ili kutoa wajibu kwa kila raia kutoa taarifa juu ya hujuma zozote zinazoweza kutokea juu ya maliasili. Hivyo, Ibara ndogo ya (2) imefutwa wa sababu maudhui yake yameshazingatiwa kwenye ibara ndogo ya (1). Baada ya marekebisho hayo ibara ndogo ya (3) imekuwa ibara ndogo ya (2), Kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 59 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.28 IBARA YA 52: Haki na Wajibu Muhimu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki na wajibu muhimu. Kamati tisa zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo na Kamati tatu zimependekeza Ibara hii kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza maneno "**dini, kabila na jinsi**"

katika Ibara ndogo ya (3) na neno "**jinsi**" katika Ibara ndogo ya (4). Vile vile, kuongeza Ibara mpya ya 52A inayohusu wajibu wa mamlaka ya nchi katika uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezohayo, Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo ya kufanya marekebisho katika Ibara hii ili kuzuia mtu kupewa haki au cheo kwa kuzingatia vigezo hivyo. Aidha, pendekezo la kuongeza Ibara mpya ya 52A halikuzingatiwa katika sehemu hii kwa kuwa limezingatiwa katika Sura Mpya inayohusu masuala ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 60 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.29 IBARA YA 53: Hifadhi ya haki za binadamu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu hifadhi ya haki za binadamu. Kamati tisa zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Hata hivyo, Kamati tatu zimependekeza marekebisho ya kufuta ibara ndogo ya (3), kufuta neno "**zinao**" na badala yake kuweka neno "**zina**" kwenye ibara ndogo ya (1) na kuifanyia marekebisho ibara ndogo ya (3) kwa kuongeza maneno **"na kufanywa kuwa sehemu ya sheria za nchi**" baada ya neno "**imeridhia**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari maudhui ya Ibara ya 53, sanjari na mapendekezo ya Kamati zote na mijadala ya ndani ya Bunge, imeifanyia marekebisho, ibara ndogo ya (1) kwa kufuta maneno "**na mamlaka ya nchi**" ili kuweka mtiririko mzuri wa kiuandishi na ibara hii iweze kueleweka kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imekubaliana na pendekezo la kuifuta ibara ndogo ya (3) ili utaratibu unaotumika sasa wakuifanya Mikataba hiyo itumike ndani ya nchi kwa kuandaliwa Sheria mahsusi itakayotungwa na Bunge au kurekebisha sheria za nchi, uendelee, kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mkataba husika ndani ya nchi *(domestication)*.

Aidha Kamati imefanya maboresho ya kimaudhui kwenye ibara ndogo ya (1) na ya (2) kwa lengo la kuzingatia muktadha wa muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mapendekezo hayo Ibara ya 53 sasa isomeke kama inavyopendekezwa kwenye Ibara ya 61 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.30 IBARA YA 54: Usimamizi wa haki za binadamu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu usimamizi wa haki za binadamu. Kamati tano zimependekeza Ibara hii ibakikama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati saba zimependekeza

Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza ibara ndogo ya (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kiuandishi kwenye ibara ndogo ya (3) na ya (4). Aidha, Kamati imeongeza kwenye ibara ndogo ya (4), aya mpya ya (a) inayomtambua Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kama mmoja wapo wa watu wanaoweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu la kudai haki za kikatiba, kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii, kwa kuzingatia kwamba yeye ni mwangalizi wa maslahi ya umma. Kwa muktadha huu, aya ya (a) itasomeka kuwa aya ya (b) na aya zinazofuatia zitafuata mpangilio huu.

Aidha, Kamati imeunga mkono hoja ya kuongeza Ibara ndogo ya (5) ili kuipa fursa Serikali kurekebisha kasoro au hitilafu iliyopo katika sheria au hatua inayolalamikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara ya 54 isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 62 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

5.31 IBARA YA 55: Mipaka ya haki za binadamu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu mipaka ya haki za binadamu. Kamati kumi zimependekeza Ibara hii ibaki kama

ilivyopendekezwa kwenye Rasimu ya Tume. Kamati mbili zimetoa mapendekezo ya kuboresha Ibara hii kwa kuongeza ibara ndogo za (3), (4) na (5). Mapendekezo haya ya Kamati yanaweka masharti ya Mahakama kusikiliza kesi zinazohusu ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzingatia na kutafakari mapendekezo haya, Kamati ya Uandishi inaona kwamba Ibara ndogo zinazopendekezwa zinaweka utaratibu wa uendeshaji wa mashauri ya ukiukwaji wa haki za binadamu ambao unapaswa kuwekwa kwenye sheria ambayo itatungwa na Bunge.

Aidha, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kimaudhui kwa kulipa mamlaka Bunge kutunga sheria kwa ajili ya kusimamia matumizi na utekelezaji wa masharti ya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 63 ya Rasimu ya Katiba hii Inayopendekezwa.

SURA YA TANO

URAIA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

6.0 IBARA YA 56: Uraia wa Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uraia katika Jamhuri ya Muungano. Kamati saba zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati tano zimependekeza marekebisho ya kiuandishi katika ibara ndogo ya (2) na kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) inayoipa Bunge mamlaka ya kutunga Sheria kuhusu masuala ya uraia na kufanya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, ilitafakari mapendekezo ya Kamati pamoja na mijadala ya Bunge na kuona kwamba maudhui yake yanajitosheleza na hivyo kutohitaji marekebisho yoyote.

Kwa kuzingatia ufafanuzi huo, Kamati ya Uandishi imeandika Ibara hii kama ilivyo kwenye Ibara ya 65 ya Rasimu Katiba hii.

6.1 IBARA YA 56A: Haki za Uraia

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeongeza Ibara mpya ya 56A inayohusu haki ya Uraia ili kumwezesha raia kupata hati ya kuzaliwa, kitambulisho cha uraia wake bila ya

upendeleo na ubaguzi wa aina yoyote na pale inapohitajika kupatiwa nyaraka za kumwezesha kusafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia pendekezo hilo, Kamati ya Uandishi imeongeza Ibara mpya kwenye Sura hii kama ilivyo kwenye Ibara ya 66 ya Rasimu hii ya Katiba inayopendekezwa.

6.2 IBARA YA 57: Uraia wa kuzaliwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati moja imependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati kumi na moja zimependekeza kufanya marekebisho mbalimbali. Miongoni mwa marekebisho hayo ni; kufuta neno "Tanganyika" na kuweka neno "Tanzania Bara", kufuta neno "anayezaliwa" na kuweka neno "aliyezaliwa", kuongeza ibara ndogo ya (3) inayolipa mamlaka Bunge kutunga sheria itakayoweka taratibu za utoaji wa uraia na kupanga upya namba za ibara ndogo ya (3) kuwa ya (4) na zinazoendelea kufuata mpangilio huo. Aidha, kufuta ibara ndogo ya (4) na (5) na kuongeza ibara ndogo mpya ya (5), (6), (7) na (8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapitia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge na mijadala Bungeni, Kamati ya Uandishiimefanya maboresho madogo ya kimaudhui katika ibara ndogo ya (1)kwa kufuta neno "Tanganyika" na kuweka

badala yake maneno “Tanzania Bara”. Pia katika ibara ndogo ya (3) kwa kuongeza neno “wake” baada ya neno “wazazi” na pia kwa kufuta neno “kama” na kuweka neno “kana” yanayolenga kuweka matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili.

Aidha, Kamati ya Uandishi imezingatia pendekezo la kuongeza ibara ndogo ya (6) itakayolipa Bunge mamlaka kutunga sheria ambayo itaweka masharti ya jinsi ya kushughulikia masuala yote ya uraia wa kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia pendekezo hilo, Kamati ya Uandishi imeiboresha Ibara hiyo kama inavyosomeka katika Ibara ya 67 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

6.3 IBARA YA 58: Uraia wa kuandikishwa

Mheshimiwa Mwenyekiti,Ibara hii inahusu Uraia wa kuandikishwa. Kamati tatu zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba na Kamati tisa zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno **“tano”** katika ibara ndogo ya (2)(a), na badala yake kuweka neno **“saba”** na kuongeza Ibara mpya ya 58A inayoainisha masharti ya mtu kufutiwa uraia .

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari kwa kina mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeridhia mapendekezo ya Kamati na mijadala ndani ya Bunge ya kuongeza kipindi cha kuomba uraia wa kuandikishwa kwa mtu aliyefunga ndoa na raia wa Jamhuri ya Muungano kutoka miaka mitano hadi saba.

Lengo la kuongeza muda huu, ni kujua dhamira na matendo ya muombaji katika kuthibitisha uaminifu wake na nia njema ya kuhitaji uraia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, Kamati ya Uandishi haikuunga mkono hoja ya kuanzisha Ibara mpya inayohusu masharti ya mtu kufutiwa uraia wa kuzaliwa kwa sababu maudhui yake yamezingatiwa katika ibara ndogo ya (6) ya ibara ya 68 ambayo imeipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria, ambayo itasimamia masuala yanayohusu uraia wa Jamhuri ya Muungano ikiwemo masharti ya mtu kufutiwa uraia.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 68 Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

6.4 IBARA YA 59: Hadhi ya watu wenye asili au nasaba ya Tanzania

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu hadhi ya watu wenye asili au nasaba ya Tanzania. Kamati nane zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba. Kamati nne zimependekeza marekebisho yanayolenga kuboresha maudhui yaliyomo kwenye Ibara hii, kwa kupendekeza uraia wa nchi zaidi ya moja (uraia pacha) na hivyo kutoa fursa kwa raia wa Jamhuri ya Muungano aliyepata uraia wa nchi nyingine kuendelea kubaki na uraia wa Jamhuri ya Muungano.

Aidha, Kamati moja imependekeza kuongeza Ibara mpya itakayoipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria itakayosimamia masuala yanayohusiana na Sura hii ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyatafakari mapendekezo ya Kamati pamoja na maoni ya Wajumbe katika mijadala ya Bunge Maalum, inapendekeza marekebisho madogo kwenye Ibara hii kwa kuongeza neno **Maalum** mbele ya neno **"hadhi"** ili lisomeke **hadhi maalum**. Mapendekezo haya yanatokana na ukweli kwamba Ibara hii kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, inaweka msingi wa kuwapa hadhi maalum kwa sheria itakayotungwa na Bunge watu wenye asili au nasaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao wameacha kuwa raia wa Jamhuri ya

Muungano. Utaratibu wa kisheria unaopendekezwa hapa unatumika sehemu nyingine duniani kwa mafanikio makubwa na unatoa fursa mbalimbali kwa watu hao bila ya kupewa uraia pacha.

Kwa mantiki hiyo, fursa mbalimbali zinazofikiriwa kuwa zitapatikana kwa kuwepo kwa uraia pacha zinaweza pia kupatikana bila ya kuwepo kwa uraia pacha kwa misingi iliyowekwa katika Ibara hii.

Kwa msingi wa hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 69 ya Rasimu hii.

SURA YA SITA

MUUNDO WA JAMHURI YA MUUNGANO

7.0 IBARA YA 60: Muundo wa Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Muundo wa Muungano. Kamati zote zilipendekeza kuifuta Ibara hii na kuiandika upya ili iendane na muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi kwa kuzingatia mapendekezo hayo imeandika upya Ibara hii ili iweze kuendana na mfumo wa Serikali mbili kwa kuanzisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, Kamati ya Uandishi ina maoni kwamba vyombo vya utekelezaji vilivyopendekezwa na Kamati za Bunge na mijadala yake kuanishwa katika Ibara hii, sasa vihamishiwe katika Ibara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo ya Wajumbe walio wengi na pia maboresho ya kiuandishi Ibara hii imeandikwa upya kama inavyosomeka katika Ibara ya 70 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

7.1 IBARA YA 61: Vyombo vya Utendaji vya Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu vyombo vya utendaji vya Jamhuri ya Muungano**.** Kamati zote zilipendekeza kufutwa kwa Ibara ya 61 kwa kigezo kwamba maudhui yaliyotajwa katika Ibara hiyo yamezingatiwa katika Ibara ya 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge na mijadala Bungeni, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kufutwa kwa ibara hii na kuiandika upya ili kuviwezesha vyombo vya utendaji vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar viweze kutekeleza kwa ubora shughuli za umma na kuweka mgawanyo wa madaraka juu ya shughuli hizo, baina ya vyombo vilivyotajwa katika ibara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vinavyopendekezwa kuanzishwa ni vyombo vya utendaji vyenye mamlaka ya kutunga sheria, utoaji haki na kusimamia utendaji wa shughuli za umma katika muktadha wa Muundo wa Serikali mbili. Aidha, Ibara hii imeweka masharti ya utekelezaji wa majukumu ya vyombo vilivyoainishwa kwa mujibu wa Katiba hii na Katiba ya Zanzibar.

Kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara yenye maneno ya pembeni "utekelezaji wa shughuli za

mamlaka ya nchi". Ibara hii ni kama inavyosomeka katika Ibara ya 71 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

7.2 IBARA YA 62: Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano**.** Kamati zote kumi na mbili pamoja na mijadala ya Bunge Maalum zilipendekeza Ibara hii ifutwe na kuandikwa upya ili kubainisha mipaka ya mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kuongeza dhana ya utekelezaji wa Mambo yasiyokuwa ya Muungano yanayohusu Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hiyo ili kuipa mamlaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuweza kutekeleza Mambo ya Muungano na Mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara hii isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 72 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

7.3 IBARA YA 63: Mambo ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mambo ya Muungano na inaweka masharti kwa ajili ya utekelezaji bora

wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, na kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka juu ya shughuli hizo. Kamati ya Uandishi baada ya kupitia maudhui ya Ibara hii inapendekeza kuwa Ibara hii ifutwe na maudhui yake yamekwisha zingatiwa katika Ibara mpya ya 71(3) ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

7.4 IBARA YA 64: Nchi Washirika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Nchi Washirika, na kwa mujibu wa Rasimu ya Tume nchi washirika zimetajwa kuwa Tanganyika na Zanzibar. Ibara inaelezea kuhusu mamlaka juu ya mambo yote yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanganyika na hivyo hivyo kwa Zanzibar. Kamati nyingi zimependekeza Ibara hii ifutwe.

Kamati ya Uandishi imetafakari na kuifuta Ibara hii kwa kuwa maudhui yaliyomo kwenye Ibara hii yanahusu Muundo wa Serikali tatu, tofauti na Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa kwa sasa.

7.5 IBARA YA 65: Mamlaka ya Nchi Washirika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu mamlaka ya nchi washirika kama ilivyopendekezwa kwenye Rasimu. Kamati nyingi na mijadala ndani ya Bunge Maalum zilipendekeza Ibara hii ifutwe na kuandikwa upya. Hivyo, Ibara hii

inapendekezwa kuandikwa upya ili kuainisha mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya Mambo yasiyo ya Muungano kwa upande wa Zanzibar na pia kuipa uwezo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha uhusiano na ushirikiano na jumuiya na taasisi za kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo ya kufutwa kwa Ibara hii na kuiandika upya ili kuiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa na uhuru na uwezo wa kuanzisha uhusiano au ushirikiano na Jumuiya au Taasisi yoyote ya kikanda au kimataifa. Aidha, Katika kutekeleza mamlaka na majukumu yake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahitaji kupata ushirikiano kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kufanikisha uhusiano au ushirikiano huo.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi, imeandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 73 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

7.6 IBARA YA 66: Mahusiano kati ya Nchi Washirika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mahusiano kati ya nchi washirika kama ilivyopendekezwa kwenye Rasimu ya Tume. Katika Ibara hii, Kamati nyingi na mijadala ndani ya Bunge zilipendekeza Ibara hii ifutwe na kuandikwa upya ili

kuondoa dhana ya uwepo wa Nchi Washirika na badala yake Ibara hii izungumzie uhusiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilitafakari Ibara hii na kufanya maboresho kwa kuongeza maudhui yanayohusu makubaliano maalum kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu Zanzibar, kwa mujibu wa makubaliano hayo. Lengo la maboresho hayo ni kuimarisha mahusiano baina ya Serikali hizi mbili katika utekelezaji wa mambo yenye maslahi kwa pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapendekezo ya Kamati za Bunge Maalum pamoja na maboresho hayo, Ibara hiyo imeandikwa upya na sasa itakuwa na ibara ndogo ya (4) kama inavyosomeka katika Ibara ya 74 ya Rasimu hii ya Katiba inayopendekezwa.

7.7 IBARA YA 67: Mawaziri Wakaazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mawaziri Wakazi watakaoteuliwa na Nchi Washirika kuratibu na kusimamia masuala ya mahusiano baina ya Nchi Washirika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Bunge Maalum na Wajumbe wengi wakati wa mijadala ndani ya Bunge Maalum walipendekeza Ibara hii ifutwe ili kuondoa dhana ya kuwepo kwa Mawaziri ambao kimsingi waliwekwa kwa ajili ya muundo wa Serikali tatu. Hivyo, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hiyo ifutwe kwa kuwa muundo unaopendekezwa sasa ni wa Serikali mbili na siyo tatu.

7.8 IBARA YA 68: Mamlaka ya Wananchi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mamlaka ya Wananchi. Kamati nyingi za Bunge Maalum na wajumbe wengi wakati wa mijadala walipendekeza Ibara hii ifutwe na kuandikwa upya kwa sababu maudhui yake yalikusudia kuanzishwa kwa mfumo wa Serikali tatu. Hata hivyo, baadhi ya Wajumbe waliyo wachache walipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu kwa kuwa walikuwa wanaunga mkono muundo wa Serikali tatu uliyopendekezwa na Tume ya mabadiliko ya Katiba uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa mujibu wa mapendekezo hayo, suala la Serikali za Mitaa ambazo zilikuwa zikianzishwa na Serikali za Nchi Washirika kwa mujibu wa Rasimu ya Katiba, sasa zitaanzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Sheria zao. Aidha, kwa kuwa Serikali za Mitaa sio suala la Muungano,

Serikali hizo zitaanzishwa chini ya Katiba hii kwa upande wa Tanzania Bara na Katiba ya Zanzibar kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilitafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge Maalum na maoni wakati wa mijadala na kwakuwa hoja zilizotolewa zilikuwa ni za msingi, Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo hayo ya kuanzisha Serikali za mitaa na maudhui ya uanzishaji huo yamezingatiwa katika Sura ya Nane.

7.9 IBARA YA 69: Wajibu wa Kulinda Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Wajibu wa Kulinda Muungano. Kamati zote kumi na mbili zimependekeza ibara ndogo ya (1) na ya (3) zifanyiwe marekebisho kwa kuziboresha ili kuondoa dhana ya Muundo wa Serikali tatu unaopendekezwa na Rasimu na kuungwa mkono na wajumbe waliyo wachache kwa kuwa mfumo unaopendekezwa sasa ni wa Serikali mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilitafakari mapendekezo ya kufanyia maboresho Ibara hizi ndogo na kupendekeza maboresho ya kiuandishikatika ibara ndogo ya (2). Katika ibara ndogo ya (3), idadi ya viongozi imeongezwa na kuandikwa upya ili kuwajumuisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Kwanza wa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, Makamu Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Ibara hii imefanyiwa maboresho na kuandikwa upya kama ilivyo kwenye Ibara ya 75 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA SABA

SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

SEHEMU YA KWANZA

SERIKALI, RAIS, MAKAMU WA RAIS NA BARAZA LA MAWAZIRI

8.0 Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura ya Saba ya Rasimu ya Tume inahusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Sura hii imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni sehemu ya kwanza inayohusu Serikali, Rais, Makamu wa Rais na Baraza la Mawaziri. Sehemu ya pili inahusu Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pamoja na kwamba sehemu ya Kwanza ya Sura hii inajumjuisha Barazala Mawaziri, kimsingi maudhui yake hayajitokezi katika sehemu ya kwanza bali katika sehemu ya pili ya Sura hii. Kutokana na sababu hiyo Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho kwa kuondoa maneno 'Baraza la Mawaziri' kutoka sehemu ya kwanza ya Sura hii na kuyahamishia kwenye kichwa cha habari cha sehemu ya pili kwa kuwa ndipo mahali yalipokusudiwa kuwepo.

9.0 IBARA YA 70: Serikali ya Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kamati zote kumi na mbili zilipendekeza ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza maneno Rais, Makamu wa kwanza wa Rais na Makamu wa pili wa Rais, katika Ibara

ndogo ya (1). Aidha, Kamati sita zilipendekeza "Serikali ya Jamhuri ya Muungano iongozwe na Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Makamu wa Tatu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano". Kamati moja ilipendekeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano iongozwe na Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano. Vile vile, kulikuwa na pendekezo la kutaka Rais kukasimu madaraka yake kwa mtu mwenye madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au vyombo vyovyote vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati nyingine zilipendekeza ibara ndogo ya (2) ifutwe na kuandikwa upya ili kuitambua Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kuipa uwezo wa kutekeleza Mambo yote ambayo ni ya Muungano na yasiyo ya Muungano yanayoihusu Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ndogo ya (3) Kamati zilipendekeza madaraka ya Rais yakasimishwe kwa viongozi waliotajwa katika ibara ndogo ya (1). Sababu za mapendekezo haya ni kumwezesha Makamu wa Rais ambaye ni mgombea mwenza kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na kumtambua Rais wa Zanzibar kwa kumpa hadhi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kuheshimu makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964, yaliyomtambua Rais wa Zanzibar kama Makamu wa Rais. Pia kulikuwa na pendekezo la

kumfanya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kuwa Makamu wa Tatu wa Rais ili aweze kumsaidia Rais kutekeleza Mambo ya Muungano na Mambo yasiyo ya Muungano yanayoihusu Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo hayo imekubaliana na pendekezo la kumtambua Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kuwa Makamu wa Tatu wa Rais ili waweze kumsaidia Rais katika kutekeleza majukumu yake. Pia, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kuipa mamlaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili iweze kutekeleza Mambo yote ya Muungano na mambo yote yasiyo ya Muungano yanayoihusu Tanzania Bara. Kutokana na mapendekezo ya Kamati mbalimbali na majadiliano yaliyojitokeza Bungeni, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo hayo katika kuiandika Ibara hii na itasomeka katika Ibara ya 76 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.1 IBARA YA 71: Rais wa Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Rais wa Jamhuri ya Muungano, Kamati saba zilipendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati tano zilipendekeza marekebisho mbalimbali kwa kuongeza maneno "**ya Muungano"** baada ya neno "**Serikali''** katika Ibara ndogo ya

(2) na Kuboresha ibara ndogo ya (2)(c) kwa kuongeza maneno **"Muungano na**", baada ya neno **"kuhifadhi".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo ya Kamati na mijadala Bungeni na inakubaliana na mapendekezo ya kubainisha kuwa Serikali inayotajwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, Kamati inapendekeza ibara ndogo ya (2)(c) ifutwe kwakuwa inatoa majukumu kwa Rais ya kulinda, kukuza na kuhifadhi Muungano, dhana ambayo maudhui yake yanapaswa kuzingatiwa katika Ibara inayozungumzia madaraka na majukumu ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Ibara hii imerekebishwa na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 77 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.2 IBARA YA 72: Madaraka na majukumu ya Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Madaraka na majukumu ya Rais, Kamati moja imependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati kumi na moja zimependekeza marekebisho mbalimbali yakiwemo kuifuta na kuiandika upya ibara hii kwa lengo la kuainisha majukumu ya msingi ya Rais na kuyaacha mambo mengine yazingatiwe katika sheria za nchi. Aidha, kulikuwa na pendekezo linalomtaka Rais katika kutekeleza majukumu yake azingatie maadili na miiko iliyowekwa katika Katiba hii na pia kumpa

mamlaka Rais ya kuteua, kupandisha vyeo, kuanzisha na kufuta ofisi, kufukuza kazi na kumwezesha kuwa ndiye mwenye mamlaka ya nidhamu kwa watu anaowakabidhi madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapitia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi haioni haja ya kuainisha mamlaka ya Rais ya kuanzisha, kuteua, kupandisha vyeo, kufuta ofisi, kufukuza watu kazi na kumwezesha kuwa mamlaka ya nidhamu kwa watu anaowakabidhi madaraka. Aidha, Kamati ya Uandishi imezingatia pendekezo la kuainisha majukumu ya jumla ya Rais na kuyaacha majukumu mengine ya kawaida yaainishwe kwenye Sheria zitakazotungwa na Bunge. Ibara hii sasa itasomeka kama ilivyo kwenye Ibara ya 78 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.3 IBARA YA 73: Utekelezaji wa madaraka ya Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Utekelezaji wa madaraka ya Rais. Kamati tatu zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, Kamati tisa zimependekeza kufanya marekebisho mbalimbali ikiwemo kuifuta ibara ndogo ya (3) na kuiandika upya ili kuweka masharti kwamba Rais anapotekeleza madaraka yake ya uteuzi azingatie masharti kuhusu uthibitisho wa Bunge au mamlaka nyingine za ushauri. Aidha, ilipendekezwa kuifuta ibara ndogo ya (4) ili kuwezesha viongozi watakaoteuliwa na mamlaka nyingine kushika nafasi za madaraka katika Serikali ya

Jamhuri ya Muungano ambao sio viongozi Wakuu wala watendaji Wakuu yawe mikononi mwa mamlaka husika za nidhamu na uteuzi kwa mujibu wa Katiba hii na Sheria za nchi. Vile vile kulikuwa na pendekezo la kufuta neno "madaraka" na badala yake kuweka neno "**mamlaka**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapitia mapendekezo haya na michango katika mijadala mbalimbali Bungeni, Kamati ya Uandishi haikuona haja ya kumtaka Rais anapofanya uteuzi wa viongozi azingatie uthibitisho wa Bunge. Kamati inashauri kuwa ni vema Rais azingatie masharti ya Katiba na Sheria zitakazotungwa na Bunge. Aidha, ibara ndogo ya (4) imefanyiwa marekebisho ili kuipa mamlaka husika ya nidhamu na uteuzi iweze kufanya uteuzi na kudhibiti nidhamu kwa mujibu wa Katiba hii na sheria za nchi badala ya mamlaka hayo kuwekwa katika Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeboresha Ibara hii na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 79 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.4 IBARA YA 74: Rais kuzingatia ushauri

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Rais kuzingatia ushauri, Kamati mbili zilipendekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Aidha, Kamati mbili zilipendekeza kuwa Ibara hii ifutwe na Kamati nane zilizobakia zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali katika ibara

ndogo ya (1) ikiwa ni pamoja na kumtaka Rais kuzingatia ushauri anaopewa na mtu yeyote au mamlaka yoyote wakati Kamati nyingine zilipendekeza kuwa Rais asilazimike kuzingatia ushauri anaopewa na mtu yeyote au mamlaka yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi haikushawishika na pendekezo la kumtaka Rais kulazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu au mamlaka yeyote kwa kuwa Rais ndiye kiongozi Mkuu wa nchi hivyo ni vyema awe huru wakati wa kutekeleza Majukumu yake na kutokushurutishwa na mtu wala mamlaka nyingine, isipokuwa pale anapotakiwa na Katiba hii au sheria zitakazotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia mapendekezo na mijadala ya Kamati mbalimbali ndani ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imeifuta Ibara hii na kuiandika upya na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 80 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.5 IBARA YA 75: Rais kushindwa kumudu majukumu yake

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Rais kushindwa kumudu majukumu yake, Kamati nane zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Aidha, Kamati nne zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa Kuongeza maneno "**ya mwili au akili**" baada ya neno

"**maradhi**" lililopo katika ibara ndogo ya (1) na kuongeza Ibara ndogo mpya ya (3) itakayoweka masharti ya kuanzishwa kwa Kamati itakayofanya utafiti kuhusu afya ya Rais. Pia, kulikuwa na pendekezo la kuongeza idadi ya siku za kubatilisha hati ya uthibitisho wa Rais kuwa ameshindwa kumudu kazi zake kutoka siku saba kama ilivyopendekezwa katika Rasimu hadi siku kumi na nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo kuhusu kuongeza siku za nafasi ya Rais kuwa wazi kutokana na maradhi, Kamati ya Uandishi iliafiki mapendekezo ya Tume kwa kuwa muda wa siku saba unaopendekezwa unafaa hivyo hakuna haja ya kuongeza siku hizo kama zilivyopendekezwa na Kamati mbalimbali za Bunge Maalum. Pia, Kamati ya Uandishi, inapendekeza kufanya maboresho ya kiuandishi kwa kuondoa maneno "**ya madaraka**" katika ibara ndogo ya (3) na badala yake kuweka maneno "**kiti cha Rais**" ili kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia marekebisho hayo, Kamati ya Uandishi imerekebisha Ibara hii na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 81 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.6 IBARA YA 76: Utaratibu wa kujaza nafasi ya Rais kabla ya kumaliza muda wake

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Utaratibu wa kujaza nafasi ya Rais kabla ya kumaliza muda wake, Kamati mbili zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati kumi zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kufuta maneno "**Makamu wa Rais**" na badala yake kuweka maneno "**Makamu wa Kwanza wa Rais**" katika maneno ya kufungia *(closing clause)*ya ibara ndogo ya (1); kuweka dhana ya kuitisha uchaguzi ndani ya siku tisini baada ya Makamu wa kwanza wa Rais kuapishwa na kushika nafasi ya Rais ikiwa nafasi hiyo itakuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na pendekezo la kuweka utaratibu wa kufuata katika kujaza nafasi ya Makamu wa Rais baada ya nafasi ya Rais iliyokuwa wazi kuwa imejazwa. Endapo nafasi ya Rais iliyokuwa wazi itakuwa imejazwa na mtu aliyependekezwa na Chama cha Siasa basi mtu huyo atamteua Makamu wa Rais kwa kushauriana na chama chake cha Siasa na endapo mtu aliyejaza nafasi ya Rais alipatikana kwa njia ya Mgombea Huru basi mtu huyo atamteua Makamu wa Rais kwa kushauriana na Tume Huru ya Uchaguzi kisha kuwasilisha jina hilo Bungeni ili lithibitishwe na Bunge kwa kuungwa mkono kwa asilimia zaidi ya Hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo, imekubaliana na pendekezo la kumtaka Makamu wa Kwanza wa Rais aweze kuapishwa kushika nafasi ya madaraka ya Rais pale ambapo nafasi ya Rais inapokuwa wazi kutokana na kufariki dunia, kujiuzulu, kupoteza sifa za uchaguzi au kuondolewa katika madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la utaratibu wa kumteua Makamu wa Rais baada ya kujazwa kwa nafasi ya Rais iliyoachwa wazi, Kamati ya Uandishi ilikubaliana na pendekezo hilo la kujaza nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais baada ya kushauriana na chama cha siasa anachotoka endapo mtu aliyejaza nafasi ya Rais ametokana na chama cha siasa au Tume huru ya Uchaguzi kama ametokana na Mgombea Huru. Vile vile, Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho ya kiuandishi kwa kurekebisha jina la Makamu wa Rais na badala yake kuongeza maneno "**wa Kwanza**" ili kuweka bayana kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais ndiye anayehusika kwa mujibu wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali. Hivyo basi, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hiyo kama inavyoonekana katika Ibara ya 82 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.7 IBARA YA 77: Utekelezaji wa majukumu ya Rais akiwa hayupo

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inayohusu utekelezaji wa majukumu ya Rais akiwa hayupo, Kamati zilikuwa na mapendekezo mbalimbali mapendekezo hayo yanajumuisha:-

(a) kuwepo na-

(i) Makamu wa Pili wa Rais;

(ii) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano; na

(iii) Jaji Mkuu;

(b) kuwepo na -

(i) Makamuwa Kwanza wa Rais au kama nafasi yake ikowazi au kama naye hayupo au ni mgonjwa, basi;

(ii) Waziri Mkuu;au

(iii) kama Waziri Mkuu nafasi yake ikowazi au kama naye hayupo au ni mgonjwa, basi Spika;

(c) kuwepo na-

(i) Waziri Mkuu; au

(ii) Kama Waziri Mkuu nafasi yake iko wazi au kama naye hayupo au ni mgonjwa, Waziri mwingine yeyote atakayeteuliwa na Baraza la Mawaziri;

(d) kuwepo na -

(i) Makamu wa Kwanza wa Rais au kama nafasi yake iko wazi au kama naye hayupo au ni mgonjwa, basi Makamu wa Pili wa Rais; na

(ii) Waziri Mkuu, kama Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pilii wa Rais hawapo au ni wagonjwa;

(e) kuwepo na -

(i) Makamu wa Kwanza wa Rais;

(ii) Makamu wa Pili wa Rais;

(iii) Makamu wa Tatu wa Rais;

ama kama nafasi zao ziko wazi au nao kama hawapo, au ni wagonjwa, basi, Spika au Jaji Mkuu.

(f) kuwepo na -

(i) Rais wa Zanzibar na Makamu wa Pili wa Rais, kama Rais wa Zanzibar na Makamu wa Pili wa Rais naye hayupo au ni mgonjwa, basi Waziri Mkuu na Makamu wa Tatu wa Rais;

(g) kuwepo na -

(i) Waziri Mkuu;

(ii) Spika wa Bunge; au

(iii) Jaji Mkuu;

(h) kuwepo na Rais wa Zanzibar kama Waziri Mkuu nafasi yake iko wazi au kama naye hayupo, au ni mgonjwa, Waziri mwingine yeyote atakayeteuliwa na Baraza la Mawaziri;

(i) kuwepo na Makamu wa Kwanza wa Rais; au kama nafasi yake iko wazi au kama naye hayupo au ni mgonjwa basi, Makamu wa Pili wa Rais na kama Makamu wa Pili wa Rais nafasi yake iko wazi ama naye hayupo ama ni mgonjwa, basi Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo imeandika kwa kuzingatia muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa na wajumbe walio

wengi ambao ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Makamu wa Tatu wa Rais ambaye atakuwa Waziri Mkuu na Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na muundo huo, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa endapo ikitokea kuwa Rais hayupo atayemfuatia katika kutekeleza majukumu yake atakuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, na kama Makamu wa Kwanza wa Rais hayupo basi atakayefuata atakuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la Makamu wa Pili wa Rais, Kamati ya Uandishi imelizingatia, isipokuwa halikujumuishwa katika marekebisho ya Ibara hii kwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais anayependekezwa na Muundo wa Serikali mbili atakuwa ni Rais wa Zanzibar. Kwa kuzingatia majukumu aliyonayo Rais wa Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, 1984 itakuwa vigumu kumtwisha majukumu mengine ya Urais wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu pendekezo la kumuweka Jaji Mkuu au Spika wa Bunge kuweza kushika madaraka ya kutekeleza majukumu ya Rais akiwa hayupo, halikuzingatiwa kwani mhimili ya utendaji *(executive)* unatofautiana kwa kiasi na mihimili ya Mahakama na Bunge hivyo itakuwa vigumu kwa

watendaji wa mihimili hiyo kuweza kutekeleza majukumu ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mantiki hiyo na kwa kuzingatia Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hiyo kama inavyoonekana katika Ibara ya 83 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.8 IBARA YA 78: Uchaguzi wa Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inayohusu uchaguzi wa Rais, Kamati kumi zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati mbili zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa ajili ya kuleta mtiririko wa kiuandishi. Marekebisho hayo yalikuwa ni kufuta maneno "madaraka ya Rais" na badala yake kuweka neno "**Urais**" katika ibara ndogo ya (2), na kuongeza Ibara ndogo mpya ya (3) itakayoweka masharti ya muda wa kushika madaraka ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu pendekezo la kuongeza ibara ndogo ya (3), itakayoweka masharti ya muda ya kushika madaraka ya Rais, Kamati ya Uandishi haikuzingatia pendekezo hilo kwakuwa maudhui yake yameshazingatiwa katika Ibara nyingine za Rasimu ya Tume. Hivyo, Kamati ya Undishi inaona kuwa ni vyema Ibara hii ikabaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo inabaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 84 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.9 IBARA YA 79: Sifa za Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu sifa za Rais. Kamati tatu zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati tisa zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kuweka masharti ya kumtaka Mgombea Huru wa Urais kuwasilisha ilani yake ya uchaguzi inayoonyesha mipango yake ya uendeshaji wa nchi, vyanzo vyake vya mapato vya kugharamia kampeni zake za uchaguzi na timu yake ya kampeni.

Vile vile, mgombea huyo anatakiwa kuwasilisha kanuni, vigezo, na sifa atakazotumia kuwapata viongozi wa ngazi za juu wa kitaifa, orodha za mali zake, za mke au mume wake pamoja na watoto wake ambao wako chini ya umri wa miaka Kumi na nane (18) pamoja na madeni ambayo anadaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na pendekezo jingine la kumtaka mgombea ambaye ni mfanyabiashara, kuwasilisha taarifa zake za ulipaji kodi na tozo mbalimbali kwa kipindi cha miaka kumi ya nyuma. Aidha, baadhi ya Kamati zilipendekeza kuweka masharti kwa Mgombea urais kutokuwa na uraia wa nchi mbili au kutowahi kuwa raia wa nchi nyingine na pia

kuweka sharti la kutaka wazazi wote wawili wa mgombea au mmoja wa wazazi wake awe ni raia wa kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na pendekezo la kutaka sifa za mgombea urais kuwa amekaa nchini si chini ya miaka kumi, na awe na umri usiopungua miaka arobaini na tano na usiozidi miaka sabini, pia awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la kukwepa kodi au kosa la jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kuzingatia mapendekezo yote ya Kamati mbalimbali kuhusu masharti ya Mgombea Huru imeona kuwa hakuna haja ya kutenganisha masharti ya Mgombea Huru na masharti ya Mgombea anayetokana na Chama cha Siasa kwa kuwa sifa za Urais zinapaswa kuwa zinafanana bila ya kujali anatoka upande gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana pia na pendekezo la kuongeza sharti la kutaka sera za mgombea urais zisigawe Taifa kwa misingi ya ukanda, uzawa au kuwabagua walemavu. Aidha, pendekezo lililotolewa la kuweka sharti kwa mtu anayetaka kuwa Mgombea Urais awe amekaa nchini si chini ya miaka kumi halijazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mgombea urais kutowahi kutiwa hatiani, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo hilo na inaona kuwa ni vyema mtu yeyote anayetaka

kugombea urais awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai. Hii inatokana na unyeti wa nafasi ya urais na ukweli usiopingika kuwa, Rais ni taswira ya Taifa na kwamba anatakiwa awe ni mfano bora kwa jamii na itasaidia kuweza kujenga uaminifu kwa wananchi dhidi yake na kuweza kuiga mwenendo wake bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la kuongeza umri wa Mgombea urais kufikia miaka arobaini na tano na kuweka ukomo wa miaka sabini, Kamati imebaini kuwa umri wa miaka arobaini unatosha kuamini kuwa Mgombea huyo atakuwa amekomaa kifikra na kimatendo na pia utamuwezesha kutekeleza majukumu ya Urais. Kamati ya Uandishi inapendekeza kutokuweka ukomo wa umri wa kugombea nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati na mijadala mbalimbali ndani ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 85 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.10 IBARA YA 80: Utaratibu wa Uchaguzi wa Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Utaratibu wa Uchaguzi wa Rais. Kamati Sita zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu. Kamati Sita zimependekeza

marekebisho mbalimbali kwa kuongeza neno "**kilichosajiliwa**", mara baada ya neno "**chama cha siasa**" katika ibara ndogo ya (1) na kuweka masharti katika ibara ndogo ya (5) kuhusu siku ya kufanyika uchaguzi wa Rais. Aidha, kulikuwa na pendekezo la kuweka masharti ya kumtaka mgombea Urais atangazwe kuwa mshindi baada ya kupata kura nyingi zaidi halali kuliko mgombea mwingine yoyote. Pia kulikuwa na pendekezo la kumtaka mgombea Urais apate asilimia kumi ya kura zote halali kwa upande wa Zanzibar na angalau asilimia hamsini ya kura zote halali kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kuyatafakari mapendekezo hayo, ina maoni yafuatayo:

Kwanza, pendekezo la kuwa Rais achaguliwe kwa wingi wa kura yanafanana na sharti la Ibara ya 41(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977. Aidha, pendekezo la kumtaka Rais kuchaguliwa kwa wingi wa kura halikuzingatiwa kwakuwa kunaweza kufanya nchi kuongozwa na Rais ambaye watu wengi waliopiga kura hawajaridhia kuwa awe Rais.

Pili, sharti la kuwa Rais achaguliwe kwa kura zinazozidi asilimia hamsini kutoka Tanzania Bara na asilimia Kumi kutoka Tanzania Zanzibar ni la msingi ili kuonyesha kukubalika kwake na wananchi walio wengi lakini Kamati ya Uandishi inaona kuwa, kigezo cha kukubalika kwake kiwe Rais atangazwe mshindi kwa

kupata kura zaidi ya asilimia hamsini za kura zote bila kujali upande wa Jamhuri ya Muungano.

Tatu, pendekezo la kuongeza neno "**kilichosajiliwa**" ni la msingi ili kutoruhusu chama cha siasa ambacho hakijapata usajili kusimamisha mgombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti Kuhusu kuainisha siku ya kufanyika uchaguzi, Kamati ya Uandishi imelizingatia kwa kuweka sharti kuwa uchaguzi ufanyike siku ya Alhamisi ya mwisho ya mwaka wa uchaguzi ili kuheshimu imani na dini mbalimbali zinazotumia siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili kama siku za Ibada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia ufafanuzi huu, mapendekezo ya Kamati mbalimbali na mijadala ndani ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 86 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.11 IBARA YA 81: Malalamiko kuhusu uhalali wa Uchaguzi wa Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Malalamiko kuhusu uhalali wa uchaguzi wa Rais. Kamati sita zilipendekeza Ibara hii ifutwe na Kamati sita zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kwa kutaja muda wa siku ambazo mgombea wa nafasi ya Urais anatakiwa kuwasilisha malalamiko ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa Rais Mahakamani katika Ibara ndogo

ya (2). Aidha, kulikuwa na pendekezo la kutaja muda wa siku ambazo Mahakama ya Juu itatakiwa kuthibitisha juu ya uhalali wa mgombea endapo kuna pingamizi lililowasilishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali imekubaliana na hoja ya kutaja idadi ya siku ambazo mgombea yeyote wa nafasi ya Urais atatakiwa kupeleka malalamiko yake Mahakamani. Sababu ya Mapendekezo haya ni kutokana na ukweli kwamba Katiba ndio Sheria Kuu katika nchi, hivyo ni vyema siku hizo zikawekwa bayana katika Katiba badala ya kuziweka katika Sheria za nchi ili kumwezesha mtu yeyote aliyeshiriki kama Mgombea wa nafasi ya Rais ambaye hajaridhika na matokeo ya uchaguzi kuwasilisha malalamiko Mahakamani ili kuwapa wananchi fursa ya kujua uhalali wa matokeo ya mgombea wa Urais ndani ya muda uliopangwa.

Aidha, Kamati ya Uandishi imekubaliana na hoja ya kutaja siku ambazo Mahakama ya Juu inatakiwa kuthibitisha uhalali wa mgombea Urais endapo kutakuwa na pingamizi Mahakamani ili kuwezesha Mahakama kutoa uamuzi ndani ya muda uliopangwa.

Vile vile, kulikuwa na maboresho ya kiuandishi katika ibara ndogo ya (4) ili kuleta mtiririko mzuri wa kimaudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia ufafanuzi huu, mapendekezo ya Kamati mbalimbali na mijadala ndani ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imeifanyia marekebisho Ibara hii na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 87 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.12 IBARA YA 82: Kiapo cha Rais na muda wa kushika madaraka

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kiapo cha Rais na muda wa kushika madaraka. Kamati moja imependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati kumi na moja zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali katika ibara ndogo ya (1). Mapendekezo hayo yanajumuisha kutaja muda ambao Rais atatakiwa kushika madaraka baada ya kutangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Rais na Tume Huru ya Uchaguzi, kufuta maneno "**mapema iwezekanavyo**" na badala yake kuweka maneno "**ndani ya siku saba**", kuongeza maneno "**Naibu Jaji Mkuu au Jaji Mwandamizi**", ili nao waweze kuwa na fursa za kumwapisha Rais na pia kulikuwa na pendekezo la kufuta maneno "**siku ya kuthibitishwa na Mahakama ya Juu**" na badala yake kuweka maneno "**mara baada ya kuthibitishwa na Mahakama ya Juu**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo ya Kamati zote imeona kuwa ipo haja ya kutaja siku ambazo Rais Mteule atatakiwa kushika nafasi ya madaraka baada ya kutangazwa kwamba amechaguliwa

kuwa Rais. Hii itasaidia kutoa muda wa kutosha wa kuweza kukabidhiana madaraka kati ya Rais aliyetoka madarakani na Rais anayeingia madarakani. Aidha, pendekezo la kufuta maneno "**siku ya kuthibitishwa na Mahakama ya Juu**" na badala yake kuweka maneno "**mara baada ya kuthibitishwa na Mahakama ya Juu**", Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo hilo ili kutoa fursa kwa Rais Mteule aweze kutangazwa mara baada ya kutangazwa na Tume ya Uchaguzi au mara baada ya kuthibitiswa na Mahakama ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia ufafanuzi huo Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 88 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.13 IBARA YA 83: Haki ya Kuchaguliwa tena

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inayohusu haki ya kuchaguliwa tena. Kamati moja ilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo na Kamati Kumi na Moja zilipendekeza marekebisho mbalimbali kwa kufuta ibara ndogo ya (3) na kuandika upya ili kumwezesha mtu ambaye aliwahi kushika madaraka ya Urais wa Zanzibar aweze kugombea na kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na kurekebisha ibara ndogo ya (4) ili kumruhusu Makamu wa Rais kuweza kugombea nafasi ya madaraka ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kupitia mapendekezo kuhusu kumruhusu mtu aliyewahi kugombea au kuchaguliwa kushika madaraka ya Rais wa Zanzibar kuweza kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano, inaona kuwa hoja hiyo ni ya msingi na ipo haja ya kumruhusu aliyewahi kuwa Rais wa Zanzibar kugombea Urais wa Jamhuri ya Muungano kwani mtu aliyewahi kushika nafasi ya madaraka ya Rais wa Zanzibar au kuwahi kugombea nafasi hiyo anayohaki ya kushiriki katika uchaguzi wa nafasi ya madaraka ya Rais ya Jamhuri ya Muungano kwani Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vile vile, Kamati ya Uandishi ilipitia hoja ya kumruhusu Makamu wa Kwanza wa Rais kugombea nafasi ya madaraka ya Rais kwa vipindi viwili endapo atakuwa ameshika mdaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kipindi cha chini ya miaka mitatu baada ya kiti cha Rais kuwa wazi na kuona kuwa hoja hii ni ya msingi hivyo imekubaliana na pendekezo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivyo basi, Kamati ya Uandishi imeiandika Ibara hiyo mpya kama inavyosomeka katika Ibara ya 89 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.14 IBARA YA 84: Madaraka ya kutangaza vita

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Madaraka ya kutangaza vita**.** Kamati kumi zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati mbili zimependekeza ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza maneno **"la ndani au la kutoka nje ya nchi"** kati ya maneno **"lile"** na **"baada"** katika ibara ndogo ya (1), na kuongeza ibara ndogo ya (4) itakayomwezesha Rais kupeleka majeshi ya Tanzania nje ya nchi kwa ajili ya kulinda amani baada ya kupata idhini ya Bunge**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo haya Kamati ya Uandishi haikuafiki na pendekezo la kuongeza maneno **"la ndani au la kutoka nje ya nchi"** kwa sababu maneno yanayopendekezwa kuongezwa yatabadili maudhui ya Ibara hii. Aidha**,** kuhusu hoja ya kuongeza ibara ndogo ya (4) Kamati ya Uandishi imeona kuwa pendekezo hilo halihusiani na mamlaka ya Rais ya kutangaza vita, bali ni jambo ambalo lina utaratibu wake wa kufuata kwa mujibu wa Mikataba na sheria za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo haya inapendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Ibara ya 90 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.15 IBARA YA 85: Madaraka ya Rais kutangaza hali ya hatari

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Madaraka ya Rais kutangaza hali ya hatari. Kamati Kumi na moja zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati moja imependekeza marekebisho kwa Kufuta neno **"kimazingira"** lililopo katika aya ya (e) ya ibara ndogo ya (2), na badala yake kuweka neno **"asili"** na pia kufuta maneno **"kumi na nne"** katika ibara ndogo ya (3), na badala yake kuweka neno **"tano".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia mapendekezo haya Kamati ya Uandishi haikuafiki mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo kwa sababu maudhui ya Ibara hii yanajitosheleza. Aidha Kamati imefanya maboresho madogo ya kiuandishi katika aya ya (e) ya ibara ndogo ya (2) ili kuweza kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi na kupendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 91 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.16 IBARA YA 86: Mamlaka ya Rais kutoa msamaha

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mamlaka ya Rais kutoa msamaha. Kamati mbili zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati kumi, zilipendekeza marekebisho katika ibara ndogo ya (1)(a) na (b) ili kumuondolea Rais mamlaka ya kutoa msamaha na kubadilisha

adhabu ya kifo kuwa adhabu ya kifungo cha maisha kwa mtu aliyepatikana na hatia ya kuua. Pia kulikuwa na mapendekezo la kuifanyia marekebisho Ibara ndogo ya (3) kwa kuongeza maneno **"kwa kuzingatia uwiano wa pande mbili za Muungano"** pamoja na pendekezo la kufuta neno "**Tanganyika"** linalojitokeza katika Ibara ndogo ya (2) na badala yake kuweka maneno "**Tanzania Bara"**.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati zote, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kufuta neno "**Tanganyika"** katika Ibara ndogo ya (2) na badala yake kuweka maneno "**Tanzania Bara** ili kuweza kuendana na mfumo wa Serikali Mbili unaopendekezwa na Wajumbe walio wengi. Aidha, hoja ya kutaka Rais asiwe na mamlaka ya kutoa msamaha au kubadilisha adhabu ya kifo kuwa kifungo cha maisha haikuzingatiwa na Kamati kwa kuwa kazi ya kutoa msamaha ni miongoni mwa utekelezaji wa mamlaka ambayo Rais amepewa na Katiba na sio kuingilia uhuru wa Mahakama kama inavyodhaniwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la kutaka Kamati ya kumshauri Rais iwe na uwiano wa pande mbili za Muungano, Kamati ya Uandishi haikuzingatia pendekezo hilo kwa kuwa maudhui yake tayari yamezingaiwa katika Ibara ndogo ya (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo haya imeifanyia marekebisho Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 92 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.17 IBARA YA 87: Kinga ya mashtaka dhidi ya Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kinga ya mashtaka dhidi ya Rais. Kamati tisa zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati tatu zimependekeza marekebisho kwa kuongeza ibara ndogo mpya ya (4) itakayomruhusu mtu yeyote kufungua shauri la jinai au madai dhidi ya mtu aliyewahi kuwa Rais baada ya miaka miwili kupita tangu alipoacha wadhifa huo kwa kosa la ukiukwaji mkubwa wa masharti ya Katiba hii au makosa makubwa ya jinai.

Aidha, kulikuwa na pendekezo jingine la kuongeza Ibara ndogo nyingine ili kuliwezesha Bunge kutunga sheria itakayoainisha aina ya makosa ambayo mtu aliyewahi kuwa Rais anaweza kushitakiwa nayo baada ya kuacha madaraka ya Urais na utaratibu katika kumshtaki Rais aliyeacha madaraka yake. Vile vile kulikuwa na pendekezo la kumpa kinga Rais kutoshitakiwa kwa kosa la aina yoyote baada ya kuacha madaraka kutokana na kinga ya Katiba au sheria yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kutafakari mapendekezo haya, inapendekeza Ibara hii ibaki kama inavyopendekezwa kwenye Rasimu ya Tume. Suala la kumshitaki Rais baada ya muda wake wa madaraka kuisha halina uhalali kisheria kwakuwa tayari Katiba imeweka utaratibu wa kumuondoa Rais madarakani ikiwa atakiuka Katiba hii au kufanya kosa lolote lile hivyo hakuna haja ya kusubiri kumshitaki atakapomaliza muda wake wa kukaa madarakani. Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa Rais aendelee kuwa na kinga ya kutokushtakiwa ili aweze kutekeleza shughuli zake bila hofu wala woga wowote wa kushtakiwa kwa ajili ya maslahi ya taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 93 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.18 IBARA YA 88: Bunge kumshtaki Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii inayohusu Bunge kumshtaki Rais, Kamati moja ilipendekeza kuwa ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati kumi na moja zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali yakiwemo kufuta maneno **"nchi washirika"** katika aya ya (d) ya ibara ndogo ya (7) na badala yake kuweka maneno **"Jamhuri ya Muungano",** kufuta maneno **"Rais wa Tanganyika"** katika

ibara ndogo ya (14)(a), na badala yake kuweka maneno **"Rais wa Zanzibar na Makamu wa Kwanza wa Rais au Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais",** kufuta maneno **"ishirini na tano"** katika ibara ndogo ya (3)(b) na badala yake kuweka maneno **"sabini na tano",** kuandika upya ibara ndogo ya (7)(b) na (c), kufuta aya ya (d) na (e) za ibara ndogo ya (2), kuongeza aya mpya itakayo weka kigezo cha **kushindwa kutekeleza maazimio ya mihimili ya Bunge na Mahakama"ili Rais ashitakiwe,** kuongeza maneno **"kwa kuzingatia kanuni za Bunge na idadi sawa ya uwakilishi wa pande za Muungano",** kufuta aya (b) ya ibara ndogo ya (7) na badala yake kuweka maneno **"Jaji Kiongozi.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya uandishi imeyatafakari mapendekezo haya na imekubaliana na mapendekezo ya kuifanyia maboresho kwa lengo la kufanya maudhui ya Ibara hii yawiane na mfumo wa Serikali mbili unaopendekezwa na wajumbe wengi.

Aidha, Kamati ya Uandishi haikuafiki pendekezo la kumweka Jaji Kiongozi na badala yake imeifuta ibara ndogo ya (7) (b) kwa kuwa katika muundo unaopendekezwa hakutakuwa na Jaji Mkuu wa Tanganyika. Pia Kamati ya Uandishi inapendekezwa kubadili jina la Tume ya Uchunguzi iliyoundwa chini ya Ibara hii na badala yake kuiita Kamati Maalum ya Uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzingatiamapendekezo ya Kamati mbalimbali na mijadala ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imeifanyia maboresho ibara hiina itasomeka kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 94 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.19 IBARA YA 89: Maslahi ya Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Ibara hii inayohusu maslahi ya Rais, Kamati Saba zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu, Kamati tano zilipendekeza maboresho mbalimbali kwa kufuta na kuiandika upya ibara ndogo (1) ili kuwezesha mshahara na marupurupu mengine ya Rais kupangwa na Bodi ya Mishahara na kiinua mgongo, malipo ya uzeeni yalipwe kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kama itakavyoamuliwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na pendekezo la kuboresha ibara ndogo ya (2) ili kuzuia Rais kujiongezea Mshahara, marupurupu na malipo ya uzeeni akiwa madarakani. Aidha, kulikuwa na marekebisho madogo ya kiuandishi ikiwa ni pamoja na kuongeza Ibara ndogo mpya ya (3) ili kuhakikisha Rais anaendelea kupata huduma za ulinzi baada ya kumaliza kutumikia muda wake wa urais na Kamati nyingine zimependekeza Ibara hii iandikwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati mbalimbali likiwemo pendekezo la kuongeza ibara ndogo ya (3) itakayoweka masharti ya Rais kuendelea kupatiwa huduma ya ulinzi pale anapomaliza muda wake wa kushika madaraka. Hata hivyo, Kamati ya Uandishi haikuafiki pendekezo hilo kwa kuwa suala la ulinzi wa Rais mstaafu lina utaratibu wake na Ibara hii inahusu mshahara na maslahi ya Rais anapokuwa madarakani na mara baada ya kustaafu. Aidha, Kamati ya Uandishi imeongeza Ibara ndogo ya (3) inayolipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria kuhusu maslahi ya Rais akiwa madarakani na pale anapostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufuatia mapendekezo ya Kamati mbalimbali na mijadala ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imeifanyia maboresho ibara hii na itasomeka kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 95 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.20 IBARA YA 90: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Kamati za Bunge Maalum zilipendekeza Ibara hii inayohusu Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ifutwe na kuandikwa upya ili kuwezesha kuwepo kwa Makamu wa Rais wawili ambao ni Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu ambaye atakuwa Makamu wa Pili wa Rais. Vile vile, Kamati nyingine zilipendekeza kuwepo kwa Makamu Watatu wa Rais,

yaani Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye atachaguliwa pamoja na Rais kama Mgombea Mwenza, Makamu wa Pili wa Rais ambaye atakuwa Rais wa Zanzibar na Makamu wa Tatu wa Rais ambaye atakuwa ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kufanya uchambuzi wa kina imekubaliana na pendekezo la kuwa na Makamu Watatu wa Rais hivyo, Ibara hii kutokana na hoja za msingi za kumjumuisha na kumtambua Rais wa Zanzibar kama miongoni mwa viongozi wakuu wa Jamhuri ya Muungano. Sababu nyingine ni kuheshimu Hati ya Makubaliano ya Muungano ya Mwaka 1964 iliyomtambua Rais wa Zanzibar kama Makamu wa Rais. Aidha, mapendekezo haya yanalenga kumwezesha Rais kupata wasaidizi wakuu wa kumshauri katika kutekeleza majukumu yake aliyopewa kikatiba.

Hivyo, Makamu wa Kwanza wa Rais ni yule atakayekuwa Mgombea mwenza katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Pili atakuwa Rais wa Zanzibar na Makamu wa Tatu wa Rais atakuwa ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo Ibara hii imiandika upya na itasomeka kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 96 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.21 IBARA YA 91: Upatikanaji wa Makamu wa Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inayohusu upatikanaji wa Makamu wa Rais. Kamati nne zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati tisa zimependekeza ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno **"Makamu wa Rais"** na kuweka maneno "**Makamu wa Kwanza wa Rais"**. Aidha, kulikuwa na mapendekezo ya kufuta ibara ndogo ya (3) na kuandikwa upya ili kuweka masharti ya uwepo wa Rais wa Zanzibar kama Makamu wa Pili wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa Ibara hii inahusu upatikanaji wa Makamu wa Rais na kwa kuzingatia kwamba Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kuwepo wa Makamu wa Rais watatu, Ibara hii sasa itahusu upatikanaji wa Makamu wa Kwanza wa Rais. Aidha, Kamati ya Uandishi imeona kwamba Makamu wa Pili wa Rais na Makamu wa Tatu wa Rais watajwe katika Ibara tafauti. Vile vile, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuongezwa kwa ibara ndogo mpya ya (2) inayohusu masharti ya chama chochote au mtu yeyote anaekusudiwa kugombea nafasi ya madaraka ya Rais kutozuiwa kumpendekeza mtu yeyote kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais kwa sababu tu mtu huyo ameshika kiti cha Rais wa Zanzibar. Maudhui haya yamechukuliwa kutoka kwenye Ibara ya 92(2). Kwa mantiki hiyo Ibara hii itasomeka kama

inavyoonekana kwenye Ibara ya 97 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.22 IBARA YA 92: Sifa za Makamu wa Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Sifa za Makamu wa Rais. Kamati Nne zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo Katika Rasimu ya Tume na Kamati nane zilipendekeza kufanya marekebisho ya aina mbalimbali kwa kubadili jina la Makamu wa Rais kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na kufuta jina la Tanganyika ambalo limetumika sana katika Ibara hii. Aidha, kuna mapendekezo yaliyohitaji kufuta ibara ndogo ya (3) inayoweka masharti kuwa Makamu wa Pili wa Rais na Rais wa Zanzibar ataacha nafasi hiyo pindi anapoteuliwa au kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo, imeifuta ibara ndogo ya (2) na maudhui yake kuhamishiwa katika Ibara ya 91 ya Rasimu ya Katiba. Aidha, Kamati pia imeifuta, iliyokuwa Ibara ndogo ya (3) kwa sababu maudhui yake yamejikita katika muundo wa Serikali tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati na mijadala ndani ya Bunge Maalum, imezingatia sifa za mtu kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais na kuziweka chini ya Ibara ya

97(1). Kwa mantiki hiyo sifa za Makamu wa Rais zitasomeka kama zinavyooneka kwenye Ibara ya 97(1) ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Aidha, Kamati ya Uandishi imeanzisha Ibara mpya itakayohusu Majukumu ya Makamu wa Rais ambaye inasomka kama Ibara ya 98 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.23 IBARA YA 93: Kiapo cha Makamu wa Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kiapo cha Makamu wa Rais. Katika Ibara hii Kamati Mbili zilipendekeza kuwa ifutwe na kuandikwa upya ili kuweka masharti ya wakati gani Makamu wa Kwanza wa Rais ataapa kiapo cha uaminifu ambacho kitawekwa kwa mujibu wa sheria. Kamati sita zilipendekeza ibara hii isifanyiwe marekebisho kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza. Aidha, Kamati tano zilipendekeza kufanyiwa marekebisho madogo madogo kama vile ya kuweka jina la Makamu wa kwanza wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari inapendekeza kuwa Ibara hiyo ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza. Isipokuwa amaelezo ya pembeni yafutwe na kuandikwa upya ili yasomeke kiapo cha Makamu wa Kwanza wa Rais badala ya kiapo cha Makamu wa Rais. Hivyo, Ibara hii itasomeka kama Ibara 102 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.24 IBARA YA 94: Wakati wa Makamu wa Rais kushika madaraka

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Wakati wa Makamu wa Rais kushika madaraka. Kamati tatu zilipendekeza ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza na Kamati tisa zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kwa kuongeza maneno "**wa Kwanza**" "**au Makamu wa Pili wa Rais**", kuongeza ibara ndogo ya (3) itakayoweka masharti ya ukomo wa Makamu wa kwanza na Makamu wa Pili wa Rais kushika Madaraka yao kutokana na Rais kutengua uteuzi wao au Bunge kuwaondoa madarakani kwa kuwapigia kura ya kutokuwa na Imani. Kamati nyingine zilipendekeza Makamu wa Kwanza wa Rais kula kiapo kabla ya kushika madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo yaliyotolewa kwenye Kamati na Wakati wa Mijadala Bungeni na kuona kuwa ili kuwianisha muundo wa Uongozi unaopendekezwa wa kuwa na Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili na Makamu wa Tatu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 99 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.25 IBARA YA 95: Bunge kumshtaki Makamu wa Rais

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Bunge kumshtaki Makamu wa Rais. Kamati Moja imependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati kumi na moja zimependekeza kuifanyia marekebisho mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufuta maneno "**Rais wa Tanganyika"**. Aidha, Kamati nyingine zilipendekeza kufuta ibara hii na kuiandika upya ili kuainisha utaratibu mzuri wa kufuata wakati wa kumshtaki Makamu wa Rais Bungeni kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi iliyazingatia mapendekezo ya kuboresha Ibara hii kwa kuongeza maneno "**wa Kwanza"** kila mahali ambapo linajitokeza maneno "Makamu wa Rais". Aidha, pendekezo la kufuta maneno "Rais wa Tanganyika" limekubaliwa kwa kuwa mfumo wa Serikali Mbili unaopendekezwa hauhitaji uwepo wa Rais wa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivyo basi Ibara hii imefanyiwa maboresho na kuandikwa kama ilivyo katika Ibara ya 100 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.26 IBARA YA 96: Upatikanaji wa Makamu wa Rais wakati nafasi hiyo inapokuwa wazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu upatikanaji wa Makamu wa Rais wakati nafasi hiyo inapokuwa wazi. Kamati

sita zilipendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati nyingine kupendekeza kuongeza Ibara mpya zitakazoweka utaratibu wa upatikanaji wa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Tatu wa Rais ili kuainisha kwa ufasaha utaratibu wa upatikanaji wa kila kiongozi kati ya viongozi hao watatu wenye madaraka ya juu na namna watakavyoapishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeifanyia maboresho Ibara hiyo na itasomeka kama ilivyo kwenye Ibara 101 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi pia imezingatia mapendekezo ya kuwepo kwa Ibara mpya mbili zitakazozungumzia masharti ya upatikanaji wa Makamu wa Pili wa Rais na Makamu wa Tatu wa Rais. Hivyo zitasomeka kama Ibara ya 103 na 104 katika Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SEHEMU YA PILI
WAZIRI MKUU NA BARAZA LA MAWAZIRI NA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO
(a) Waziri Mkuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Sura hii inayohusu Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika Rasimu ya Katiba ya Tume hakukuwa na nafasi ya Waziri Mkuu kutokana na mfumo uliokuwa unapendekezwa wa Serikali tatu.

Kamati za Bunge Maalum pamoja na mijadala ndani ya Bunge zilipendekeza kuwepo na nafasi ya Waziri Mkuu, hivyo kupendekeza kuongeza Ibara mpya zitakazomhusu Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeridhia kuanzishwa kwa Ibara mpya za 96A, 96B, 96C na 96D zinazotaja uwepo wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, kazi na mamlaka yake, uwajibikaji katika Serikali na kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu kama zinavyofafanuliwa hapa chini.

9.27 IBARA YA 96A: Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano. Kamati nyingi zimependekeza kuwapo kwa cheo cha Waziri Mkuu kwa kuwa ndiye msimamizi Mkuu wa shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo ya kuitambua nafasi ya Waziri Mkuu Kikatiba na inapendekeza Ibara Mpya inayotamka uwepo wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atateuliwa na Rais miongoni mwa Wabunge kutoka katika jimbo la uchaguzi na anayetokana na chama cha siasa chenye wabunge wengi zaidi Bungeni au anayeungwa mkono na Wabunge wengi zaidi.

Ibara hii itasomeka kama Ibara ya 105 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.28 IBARA YA 96B: Kazi na Mamlaka ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kazi na mamlaka ya Waziri Mkuu na inataja madaraka yake kuwa Waziri Mkuu atakuwa ndiye msimamizi wa shughuli za kila siku za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Ibara hii itasomeka kama Ibara ya 106 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

IBARA YA 96C: Uwajibikaji wa Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uwajibikaji wa Serikali. Masharti ya Ibara hii yanahusu Waziri Mkuu kuwajibika kwa Rais kuhusu utekelezaji wa madaraka yake na Mawaziri chini ya uongozi wa Waziri Mkuu kuwajibika kwa pamoja Bungeni kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Ibara hii itasomeka kama Ibara ya 107 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.29 IBARA YA 96D: Kura ya kutokuwa na Imani na Waziri Mkuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inayohusu kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu. Katika ibara hii Bunge limepewa mamlaka ya kupitisha Azimio la kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu endapo itatolewa hoja Bungeni na kupitishwa kwa

kuungwa Mkono kwa kura za Wabunge walio wengi. Ibara hii itasomeka kama Ibara ya 108 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.30 IBARA YA 97: Kuundwa kwa Baraza la Mawaziri

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Ibara hii inayohusu kuundwa kwa Baraza la Mawaziri Kamati zote za Bunge Maalum zimependekeza marekebisho kwa kupendekeza kuwepo kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Rais wa Zanzibar, Makamu wa Tatu wa Rais ambaye ni Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia Kamati zimependekeza kufanya marekebisho katika ibara ndogo ya (1)(b) na ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "**Waziri Mwandamizi"** na kuweka maneno "**Waziri Mkuu"** ili kuhuisha mfumo wa Serikali mbili unaopendekezwa na Wajumbe walio wengi. Vile vile, Kamati zinapendekeza kurekebisha ibara ndogo ya (2) ili endapo Rais na Makamu wa Kwanza wa Rais hawapo, basi Waziri Mkuu aweze kuongoza Mikutano ya Baraza la Mawaziri. Aidha, kulikuwa na pendekezo la kufanya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mjumbe wa Baraza la Mawaziri isipokuwa asiye na haki ya kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati mbalimbali, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo ya Kamati katika ibara ndogo ya (1)(b) na ibara ndogo ya (2) ya kuondoa maneno "**Waziri Mwandamizi**" na

badala yake kuweka maneno "**Waziri Mkuu**" ili kuendana na mfumo wa Serikali Mbili unaopendekezwa. Pia, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa Baraza la Mawaziri liundwe na Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Rais wa Zanzibar pamoja na Makamu wa Tatu wa Rais ambaye atakuwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo ya kurekebisha ibara ndogo ya (2) ili kumpa mamlaka Waziri Mkuu ya kuongoza Mikutano ya Baraza la Mawaziri ikiwa Rais na Makamu wa Kwanza wa Rais hawapo. Pia Kamati inaafiki pendekezo la Mwanasheria Mkuu kuwa mjumbe katika Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo hayo na kuandika upya Ibara hiyo kama inavyoonekana katika Ibara ya 109 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.31 IBARA YA 98: Uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri

Mheshimiwa Mwenyekiri, Ibara hii inahusu Uteuzi wa Mawaziri. Kamati zote zilipendekeza marekebisho kwa kuweka masharti kwamba Rais ashauriane na Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu wakati wa kuteua Baraza la Mawaziri. Aidha, inapendekezwa kuweka sharti la idadi ya Mawaziri watakaounda Baraza la Mawaziri kutozidi thelathini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inakubaliana na utaratibu wa Katiba kuweka ukomo wa idadi ya Mawaziri ili kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapendekezo ya Kamati na mijadala mbalimbali katika Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imerekebisha Ibara hii na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 110 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.32 IBARA YA 99: Waziri Mwandamizi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Ibara hii inayohusu Waziri Mwandamizi, Kamati nane zilipendekeza ibara hii ifutwe kwa kuwa maudhui yake hayaendani na Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa. Kamati nne zilipendekeza kufutwa kwa maneno "**Waziri Mwandamizi**" na badala yake kuweka maneno "Waziri Mkuu" kila yanapojitokeza katika Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo, imekubaliana na mapendekezo ya kufuta Ibara hii kwa kuwa haiendani na Muundo wa Serikali Mbili unaopendekezwa na Wajumbe walio wengi.

9.33 IBARA YA 100: Kazi na mamlaka ya Waziri Mwandamizi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kazi na mamlaka ya Waziri Mwandamizi. Kamati nane zilipendekeza Ibara hii ifutwe

na Kamati nne zilipendekeza ibara ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kupendekeza kwamba majukumu ya Waziri mwandamizi yawe majukumu ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada kuyatafakari mapendekezo hayo, haikuyazingatia kwa kuwa hayaendani na Muundo wa Serikali Mbili unaopendekezwa na hivyo, Ibara hii imefutwa.

9.34 IBARA YA 101: Sifa za Mawaziri na Naibu Mawaziri

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Sifa za Mawaziri na Manaibu Mawaziri. Kamati zote Kumi na Mbili zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kuongeza aya mpya ya (d) katika ibara ndogo ya (1) itakayosomeka "**Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano**", kufuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya, kufuta maneno "**za Nchi Washirika**" na badala yake kuandika maneno "**ya Mapinduzi ya Zanzibar**" katika ibara ndogo ya (2), kufuta maneno "**Wabunge wa Bunge la Tanganyika**" na "**katika Nchi Washirika**" na kuongeza maneno "**wa pande zote za Jamhuri ya Muungano**" mwishoni mwa ibara ndogo ya (2)(a), na kuongeza maneno "**au ujuzi na uzoefu unaolingana na elimu hiyo**" katika ibara ndogo ya (1)(b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali imekubaliana na pendekezo kuwaongeza **wabunge** kuwa miongoni mwa watu wenye sifa za kuteuliwa kuwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri. Pia, Kamati inakubaliana na pendekezo la kuifuta ibara ndogo ya (2) ili kuiandika upya kwa lengo la kurekebisha lugha na kuondoa dhana ya uwepo wa Muundo wa Serikali tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapendekezo ya Kamati mbalimbali na mijadala katika Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho katika Ibara hii na itasomeka kama inavyooneka kwenye katika Ibara 111 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.35 IBARA YA 102: Kiapo, muda na masharti ya kazi ya Waziri na Naibu Waziri

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kiapo, Muda na masharti ya kazi ya Waziri na Naibu Waziri. Katika Ibara hii Kamati Kumi zilipendekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu Tume, Kamati mbili zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza aya mpya ya (b) katika ibara ndogo ya (4) kwa ajili ya kuongeza sifa itakayomfanya Waziri na Naibu Waziri kuachia nafasi ya madaraka aliyonayo kutokana na kuacha kuwa Mbunge kwa Mujibu wa masharti ya Katiba hii. Aidha, Kamati nyingine ilipendekeza Ibara ya

102(3) ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza maneno **"Naibu Waziri"**.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya mapendekezo hayo imekubaliana na pendekezo la kuongeza aya ndogo ya (b) pamoja na kuongeza maneno Naibu Waziri katika ibara ndogo ya (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapendekezo hayo ya Kamati na mijadala mbalimbali katika Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hiyo kama inavyosomeka katika Ibara 112 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.36 IBARA YA 103: Utekelezaji wa shughuli za Serikali Bungeni

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Utekelezaji wa Shughuli za Serikali Bungeni. Katika Ibara hii, Kamati saba zilipendekeza kuwa Ibara hii ifutwe kwa kuwa sifa za kuteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri zimerekebishwa ili kuruhusu Mawaziri na Manaibu Waziri kuteuliwa kutoka miongoni mwa Wabunge. Kamati nyingine tano zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kwa kufuta maneno '**hawatakuwa na haki ya kuhudhuria'** na badala yake kuweka neno **watahudhuria** katika ibara ndogo ya (1). Aidha, Kamati nyingine zilipendekeza kufuta maneno **hawatakuwa** na badala yake kuweka maneno **watakuwa** katika aya ya (a) na (b) ya ibara ndogo ya (1), kufuta ibara ndogo ya (1) na kuiandika

upya ili kuwezesha Mawaziri na Manaibu Mawaziri kuhudhuria mikutano ya Bunge na kutoa ufafanuzi kuhusu hoja yoyote inayojitokeza Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo, imekubaliana na mapendekezo ya kuifuta Ibara hii kwa kuwa, katika mfumo wa kibungeMawaziri na Naibu Mawaziri wanakuwa ni sehemu ya Bunge. Hivyo, Ibara hii imefutwa.

9.37 IBARA YA 104: Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika Ibara hii Kamati zote zilipendekeza kuongeza sifa za Mtu anayestahili kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuweka sharti kuwa ni lazima awe amewahi kuwa Wakili Mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuongeza maneno mwadilifu katika ibara ndogo ya (2)(f).

Vile vile, Kamati zilipendekeza kufuta maneno "**Mahakama Kuu ya Tanganyika**" katika ibara ndogo ya (2)(c) na badala yake kuweka maneno "**Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano**" Aidha, kulikuwa na mapendekezo ya kuweka sharti la Mwanasheria Mkuu kuhudhuria na kusikilizwa katika Mahakama zote ndani ya Jamhuri ya Muungano na kuweka sharti la Muda wa Mwanasheria Mkuu kukaa madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii pia, Kamati Nane, zimependekeza kuongezwa kwa Ibara mpya mbili zinazohusu kuwepo kwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka. Sababu za mapendekezo haya ni kutokana na ukweli kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ina Majukumu mengi na nyeti hivyo ni vyema nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu ikatambulika kikatiba.

Aidha, Kamati zilipendekeza kuanzishwa kwa Ibara inayohusu Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye atasimamia uendeshaji wa mashauri yote ya Jinai na madai yanayoihusu Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchambua Mapendekezo ya marekebisho kuhusu Ibara hii, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kuongeza sifa za mtu kuweza kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa wakili Mwandamizi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuwa nafasi hii ni nyeti hivyo inahitaji mtu mwenye uzoefu mkubwa. Aidha, Kamati ya uandhishi imekubaliana na pendekezo la kufuta maneno "**Mahakama Kuu ya Tanganyika**" na badala yake kuweka maneno "**Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano**" ili kuendana na Muundo wa Serikali Mbili unaopendekezwa na Wajumbe walio wengi. Ibara hii sasa itasomeka kama Ibara ya 113 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi pia imekubaliana na pendekezo la kuanzishwa kwa nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mkurugenzi wa Mashtaka. Nafasi hizi mbili hazikuwepo katika Rasimu ya Tume. Kamati ya Uandishi inakubaliana na ushauri wa Kamati ili kuwa na Ofisi inayotambulika Kikatiba inayosimamia uendeshaji wa masuala ya jinai kwa niaba ya Serikali. Hivyo, uanzishwaji wa nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa katika Ibara ya 113 na nafasi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeanzishwa katika Ibara ya 114 katika Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na mapendekezo hayo, Ibara hizo zimeongezwa na zitasomeka kama zilivyo kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.38 IBARA YA 105: Katibu Mkuu Kiongozi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Katibu Mkuu Kiongozi. Katika Ibara hii, Kamati mbili zilipendekeza Ibara hiyo ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, na Kamati kumi zilipendekeza marekebisho mbalimbali ikiwemo kufuta maneno **"watumishi waandamizi**" katika ibara ndogo ya (1), na badala yake kuweka maneno **"Maafisa Waandamizi**", kufuta maneno **"na kuthibitishwa na Bunge**" na kuongeza maneno **"na Naibu Katibu Mkuu Kiongozi**" mara baada ya maneno **"Katibu Mkuu**

Kiongozi" yaliyopo katika ibara ndogo ya (1). Vile vile, Kamati zilipendekeza, kuongeza ibara ndogo mpya ya (7) ili kutoa tafsiri ya maneno **"Afisa Mwandamizi".**

Aidha, Kamati nyingine zilipendekeza kufutwa kwa ibara ndogo ya (1) na kuiandika upya ili kuondoa sharti la Katibu Mkuu Kiongozi kuthibitishwa na Bunge mara baada ya kuteuliwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeafiki kwamba Katibu Mkuu Kiongozi asithibitishwe na Bunge. Hii inatokana na ukweli kwamba nafasi ya madaraka ya "**Katibu Mkuu Kiongozi**" ni nafasi ya kiutendaji katika mhimili wa utawala na si nafasi ya kisiasa. Aidha, katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola, nafasi ya madaraka ya Katibu Mkuu Kiongozi ni nafasi ya juu ya madaraka katika Utumishi wa Umma na mtu anayeteuliwa kushika nafasi hiyo hutekeleza majukumu yake kama msaidizi wa karibu wa Rais katika masuala mbalimbali yanayohusu utendaji wa Serikali na utumishi wa umma kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho ili, pamoja na mambo mengine, kuondoa dhana ya "**kuthibitishwa na Bunge**", na kutoa tafsiri ya maneno Afisa Mwandamizi. Hivyo basi, Ibara hii sasa isomeke kama Ibara ya 116 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

9.39 IBARA YA 106: Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu. Katika Ibara hii Kamati Saba zimependekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo. Hata hivyo, Kamati tano zimependekeza marekebisho mbalimbali kwa kuongeza Ibara mpya inayohusu masuala ya kutambua nafasi ya Naibu Katibu Mkuu kisheria, kutaka uteuzi wa nafasi ya Katibu Mkuu kuzingatia jinsia, uwiano wa pande mbili za Muungano, na uwakilishi wa watu wenye ulemavu kwa Wizara za Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa Ibara hii ifutwe kwa kuwa masharti yake yanahusu masuala ya utendaji ambayo hayana ulazima wa kwenye Katiba.

9.40 IBARA YA 107: Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii inahusu Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu. Katika Ibara hii, Kamati zote kumi na mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Hata hivyo, Kamati ya Uandishi haikuafiki mapendekezo ya kuwepo kwa Ibara hii hivyo Kamati inapendekeza kuwa Ibara hii ifutwe.

9.41 IBARA YA 108: Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Kamati zote kumi na mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui ya Ibara hii yanajitosheleza. Ibara hii itasomeka kama inavyoonekana Ibara ya 117 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Aidha, kulikuwa na pendekezo la kuongeza ibara mpya inayohusu Wakuu wa Mikoa ili kuweka masharti ya Kikatiba kuhusu Wakuu wa Mikoa kwa kuwa hawakuainishwa katika Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kuanzisha Wakuu wa Mikoa kama inavyo fafanuliwa katika maelezo yanayofuata. Hivyo basi, ibara hii imeandikwa kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 118 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuchambua kwa kina mapendekezo mbalimbali ya Kamati za Bunge Maalum, inapendekeza kuongeza sehemu mpya katika sura hii. Sehemu inayopendekezwa kuongezwa inahusu Madaraka ya Umma. Sehemu hiyo ina Ibara inayohusu Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na Uongozi katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu mpya iliyoongezwa pamoja na Ibara zake zimeandikwa kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 119, 120 na 121 za Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA NANE

UHUSIANO NA URATIBU WA SERIKALI

10.0 IBARA YA 109: Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali. Kamati tisa zimependekeza kuifuta Ibara hii na kuiandika upya kwa kuboresha ibara ndogo ya (1) inayotamka jina la Tume na ibara ndogo ya (2) inayoainisha muundo wa Wajumbe wa Tume ili ziendane na mfumo wa Serikali mbili. Aidha, Kamati mbili zimependekeza kuiandika upya Ibara hii kwa lengo la kuiondoa Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali na badala yake kuunda Baraza la Taifa la Uhusiano na Uratibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baraza hilo limependekezwa kuwa ni chombo cha kusimamia na kuratibu uhusiano baina ya Serikali hizo mbili. Aidha, Kamati moja imependekeza kuiandika upya Ibara hii kwa lengo la kuiondoa Tume na kuunda Kamati ya kusimamia na Kuratibu Mambo ya Muungano baina ya Serikali hizo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapitia mapendekezo yaliyotolewa pamoja na mijadala Bungeni, Kamati ya Uandishi inaona kwamba maudhui yaliyomo katika Ibara hii ni ya muhimu kwa ajili kujenga mahusiano mazuri na endelevu baina

ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hivyo, Kamati ya Uandishi, inapendekeza kuwa ibara ndogo ya (1) iandikwe upya kwa lengo la kuandika jina la Tume kuwa Tume ya Usimamizi na Uratibu wa Mambo ya Muungano kwani jina hilo linaendana na majukumu ya Tume yaliyoainishwa katika Ibara ya 123 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa. Kamati imeyabadili maelezo ya pembeni ili yaendane na jina la Tume, ambayo sasa yatasomeka "**Tume ya Usimamizi na Uratibu wa Mambo ya Muungano**", na popote litakapojitokeza kwenye Sura hii. Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuyafuta maneno yanayoashiria kuwepo kwa muundo wa Serikali tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ndogo ya (2) Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo ya Kamati mbalimbali za Bunge na mijadala Bungeni, na imeandika upya ibara ndogo ya (2) kwa kuainisha Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

(a) Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano;
(c) Kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi; na
(d) Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha maudhui ya Ibara hii, Kamati ya Uandishi, imeongeza ibara ndogo ya (3) inayoipa mamlaka Mwenyekiti wa Tume ya Mambo ya Muungano kumwalika mtu yeyote atakayeona anafaa kwa ajili ya kutoa ufafanuzi juu ya jambo lolote litakalohitajika kwenye Kamati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 122 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

10.1 IBARA YA 110: Malengo ya Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu malengo ya Tume. Kamati zote kumi na mbili za Bunge Maalum zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho, kwa ajili ya kuboresha maudhui mbalimbali. Mapendekezo ya marekebisho yanalenga kubadili jina la Tume ili liweze kuendana na maudhui ya sura hii pamoja na kufuta maneno "**Serikali za Nchi Washirika**" kwenye aya ya (a) na (c) na badala yake kuandika "**Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**" na kwenye aya ya (b) inapendekezwa kuandika "**Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**". Aidha, inapendekezwa kufuta neno "**Nchi Washirika"** na badala yake kuandika maneno "**baina ya pande mbili za Muungano**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo na mijadala ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi imejiridhisha kwamba upo umuhimu wa kurekebisha jina la "**Tume**" katika Ibara hiyo ili lisomeke kuwa ni "**Tume ya Usimamizi na Uratibu wa Mambo ya Muungano**" ili kuendeleza maudhui ya ibara ndogo ya (1). Aidha, kwa kuwa muundo wa Serikali unaopendekezwa ni wa Serikali mbili, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo ya kufuta maneno "**Nchi Washirika**" kwa kuwa yanaashiria mfumo wa Serikali tatu unaopendekezwa na Rasimu ya Tume.

Vile vile, Kamati ya Uandishi imependekeza kuwa maneno ya pembeni ya Ibara hii yasome "**Majukumu ya Tume ya Mambo ya Muungano**" na kuunganisha masharti ya Ibara ya 111 ya Rasimu ya Tume kwenye Ibara hii kwa kuwa maudhui yake yanafana. Aidha, Kamati ya Uandishi imeunganisha ya masharti ya Ibara ya 112 ya Rasimu ya Tume kwenye Ibara hii kwa kulipa Bunge mamlaka ya kutunga Sheria itakayoainisha masharti kuhusu uanzishwaji, muundo na majukumu ya Sekretarieti ya Tume ya Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii pamoja na maelezo yake pembeni kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 123 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

10.2 IBARA YA 111: Majukumu ya Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inaainisha majukumu ya Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali. Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba chombo kitakachosimamia utekelezaji wa sera, sheria mipango na mikakati katika Jamhuri ya Muungano. Pia Kamati hiyo itakuwa na jukumu la kuweka utaratibu wa mawasiliano na mashauriano endelevu kwa lengo la kuimarisha na kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zote zimependekeza marekebisho mbalimbali kwa nia ya kuboresha maudhui yaliyomo katika Ibara hii. Marekebisho hayo ni kuongeza au kufuta baadhi ya maneno, kufuta Ibara ndogo na kuziandika upya, kufuta aya na kuongeza ibara ndogo mpya, kufuta neno "**Nchi Washirika**" na badala yake kuandika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kubadili jina la Tume liwe "**Baraza la Taifa la Uhusiano na Uratibu wa Jamhuri ya Muungano**" na kuongeza aya ya (c) katika ibara ndogo ya (3) itakayosomeka "**utekelezaji wa masharti yaliyotajwa katika Ibara ya 111(c)**"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali na mijadala ndani ya Bunge na kubaini kwamba kimsingi Kamati zote zinakubaliana na maudhui ya Ibara hii. Hata hivyo, Kamati ya Uandishi, imeifuta ibara hii na kuweka maudhui yake kwenye

Ibara ya 123 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa ambayo inaweka masharti kuhusu majukumu ya Tume.

10.3 IBARA YA 112: Sekretarieti ya Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati nne zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati nane zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali ambayo yalikuwa na lengo la kufuta na kuongeza baadhi ya maneno, kufuta na kuziandika upya Ibara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati mbalimbali, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa Ibara hii ifutwe kwa kuwa maudhui yake yamezingatiwa kwa kueleza kuwa Sekretarieti itaanzishwa na sheria itakayotungwa na Bunge na kuingizwa katika Ibara ya 123 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA TISA
BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

SEHEMU YA KWANZA
KUUNDWA NA MADARAKA YA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

11.0 IBARA YA 113: Kuundwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kuundwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kamati saba zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati nyingine zimependekeza kufanya marekebisho ya kuifuta Ibara yote na kuiandika upya ili Bunge liweze kuwa na sehemu mbili, yaani Rais na Wabunge. Marekebisho mengine yalikusudia kuainisha mfumo wa upatikanaji wa Wabunge ikiwemo Wabunge wanaochaguliwa kutoka majimboni, Wabunge wanawake kutoka kila wilaya nchini, wajumbe wa kuteuliwa na Rais, Wawakilishi wa watu wenye Ulemavu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Kamati mbalimbali za Bunge maalum zilipendekeza kuongeza ibara mpya ambazo zitabeba maudhui ya kuwa na uwakilishi utakaozingatia uwiano wa asilimia hamsini kwa hamsini ya wabunge wanaume na wabunge wanawake. Pia ilipendekezwa kutungwa kwa sheria itakayoainisha utaratibu wa utekelezaji wa masharti hayo ya misingi ya uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapendekezo ya Kamati mbalimbali na mijadala ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara hii iboreshwe ili kumpa mamlaka Rais ya kuteua wabunge wasiozidi kumi kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuwa wabunge tofauti na wabunge watano wanaoteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye ulemavu. Aidha, inapendekezwa Wabunge wanaowakilisha walemavu wawe wanaotoka katika kundi hilo. Kwa maelezo hayo jumla ya idadi ya wabunge wa kuteuliwa na Rais kuwa kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia maoni ya Kamati kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa uwiano wa wabunge wanaume na wanawake. Hivyo, Kamati inapendekeza kuwepo na uwakilishi ulio sawa baina ya Wabunge wanawake na wanaume. Vile vile, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara ndogo mpya iongezwe na itoe ufafanuzi kuhusu idadi ya wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano waliochaguliwa na kuteuliwa kuwa haitazidi mia tatu na sitini. Kamati ya Uandishi inapendekeza maoni kuwa Bunge lipewe mamlaka ya kutunga sheria itakayoainisha utaratibu wa kuwapata wabunge hao. Kamati inapendekeza pia kuwekwa kwa ibara ndogo mpya itakayoainisha jukumu la vyama kusimamisha wagombea kwa kuzingatia usawa kati ya wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo haya Ibara hii imeandikwa upya kama inavyosomeka katika Ibar aya 124 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.1 IBARA YA 114: Muda wa Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu muda wa Bunge. Kamati nane zimependekeza Ibara ibaki kama ilivyo kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza na Kamati nne zimependekeza kufanya marekebisho madogo kwa kuongeza maneno "**na ubunge wa Mbunge aliye madarakani utakoma pale mbunge mwingine mteule atakapochaguliwa**", kwenye ibara ndogo ya (1) na kutoa tafsiri ya neno "**maisha ya Bunge**" katika ibara ndogo ya (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo lililotolewa la kuainisha muda wa maisha ya Bunge kuwa ni kipindi kisichozidi miaka mitano. Sababu ya marekebisho haya ni kuzingatia misingi ya kidemokrasia ya kuwawezesha viongozi kukaa madarakani kwa kipindi fulani na kutoa fursa kwa wananchi kuchagua viongozi wao baada ya kipindi ambacho kilichoainishwa na Katiba kuisha. Aidha, kuhusu tafsiri ya neno "**maisha ya Bunge**" Kamati ya Uandishi imeiboresha Ibara hiyo na kutoa tafsiri ya maisha ya Bunge kuwa ni muda wote unaoanzia tarehe ambayo Bunge jipya

litaitishwa ili kukutana kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi wa wabunge na kuisha tarehe ya uchaguzi mwingine wa wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia mapendekezo haya Ibara hii imeandikwa upya kama inavyosomeka katika Ibara 125 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba inayopendekezwa.

11.2 IBARA YA 115: Madaraka ya Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu madaraka ya Bunge. Kamati Mbili zimependekezalbara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati kumi zimependekeza kufanya marekebisho mbalimbali ikiwemo kuongeza ibara ndogo mpya ya (1) inayompa mamlaka Rais kutekeleza mamlaka yake ya kikatiba kuhusu Bunge akiwa kama sehemu ya Bunge. Aidha, kulikuwa na pendekezo la kutaka kuifuta ibara ndogo ya (2)(h) inayotoa mamlaka kwa Bunge kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusisha rasilimali zinazosimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia kulikuwa na pendekezo la kuweka sharti la ukomo wa maswali kwa Mawaziri ili waweze kuulizwa maswali rasmi tu na kuongeza sharti la Bunge kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imefanya uchambuzi wa mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati na kukubaliana na pendekezo la kuongeza ibara ndogo mpya ya (1) inayompa mamlaka Rais ya kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kuhusu Bunge akiwa kama sehemu ya Bunge. Sababu ya mapendekezo haya ni kumwezesha Rais kama sehemu ya Bunge kutekeleza mamlaka juu ya Bunge.

Aidha, pendekezo la kuifuta ibara ndogo ya (2) aya ya (h) inayohusu kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusisha rasilimali zinazosimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano limekubaliwa ili kuepuka uwezekano wa mhimili mmoja kuingilia majukumu ya mhimili mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kuwepo kwa sharti la kuweka ukomo wa maswali ya kumuliza Waziri Mkuu, limekubaliwa ili kuokoa muda na kutumia vizuri muda huo, kwa kutoa fursa ya kuuliza maswali yaliyo rasmi. Vile vile, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuongeza aya mpya ya (h) katika ibara ndog ya (2) inayoweka masharti ya Bunge kuweza kuthibitisha Viongozi kwa mujibu wa Katiba na sheria. Aidha, ibara ndogo ya (3) inayohusu Bunge kusimamia Serikali imefutwa kwa kuwa maudhui yake yamezingatiwa katika ibara ndogo ya (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia mapendekezo haya Ibara hii imefanyiwa marekebisho kama inavyosomeka katika

Ibara ya 126 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba inayopendekezwa.

11.3 IBARA YA 116: Mipaka ya Bunge katika kutumia madaraka yake

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mipaka ya Bunge katika kutumia madaraka yake. Kamati kumi zimependekezaIbara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza. Hata hivyo, Kamati mbili zimependekeza kufanya marekebisho katika ibara ndogo za (1) na (2) ili kulipa mamlaka Bunge kuwa chombo kikuu cha kuishauri Serikali katika kutekeleza mamlaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa ilibaini kuwa maudhui ya Ibara hii yanajitosheleza hivyo, haikufanya marekebisho yoyote. Ibara hiyo inapendekezwa kubaki kama ilivyo na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 127 ya Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa.

11.4 IBARA YA 117: Madaraka ya Bunge kutunga sheria

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Madaraka ya Bunge kutunga sheria. Kamati mbili zimependekeza kuifuta na kuiandika upya Ibara hii, na Kamati nyingine kumi zimependekeza kufanya marekebisho mbalimbali na maboresho madogo ya kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kuiandika upya Ibara hii ili kuainisha kwa ufasaha mamlaka ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika kutunga Sheria. Bunge la Jamhuri litatunga sheria zinazohusu Mambo ya Muungano na Mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu Tanzania Bara na Baraza la Wawakilishi litatunga sheria kuhusu mambo yasiyo ya Muungano yanayoihusu Zanzibar. Pendekezo hili pia linaenda sambamba na mfumo wa Serikali mbili ambao unapendekezwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii ili kuweka bayana mamlaka hayo ya Bunge ya kutunga sheria zinazohusu Mambo ya Muungano pamoja na mambo yote yasiyo ya Muungano yanayohusu Tanzania Bara na Zanzibar na Ibara hii itasomeka kama ilivyo katika Ibara ya 128 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.5 IBARA YA 118: Utaratibu wa kubadilisha Katiba

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kubadilisha Katiba. Kamati zote kumi na mbili zimependekeza maboresho ya kiuandishi kwa kuondoa neno **"Tanganyika"** na badala yake kuweka maneno "**Tanzania Bara**" ili iendane na Muundo wa Serikali Mbili unaopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyazingatia mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi imeifuta na kuiandika upya Ibara hii kwa lengo la kuweka masharti juu ya utaratibu wa kubadilisha Katiba kuhusu Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii au masharti yanayohusika na Jambo lolote kati ya Mambo yaliyotajwa katika Nyongeza ya Kwanza, Nyongeza ya Pili na Nyongeza ya Tatu zilizoko mwishoni mwa Katiba hii. Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 129 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

11.6 IBARA YA 119: Utaratibu wa kubadilisha Masharti Mahsusi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kubadilisha masharti mahsusi. Kamati nyingi, zimependekeza kufanya marekebisho mbalimbali ili kuweka masharti juu ya utaratibu wa kufuatwa katika kufanya mabadiliko kuhusu mambo ya msingi katika Sura ya kwanza, ya Pili, ya Tatu na ya Nne na katika Ibara ya 69 na 79. Aidha, baadhi ya Kamati zilipendekeza kuwa endapo itaonekana kuna haja ya kufanya marekebisho, marekebisho hayo yafanyike kwa kuungwa mkono kwa wingi wa kura ya theluthi mbili katika kura ya maoni kutoka kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuchambua na kutafakari mapendekezo yaliyotolewa inapendekeza Ibara hii ifutwe kwa kuwa maudhui yake yamezingatiwa katika Ibara 129 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa inayohusu utaratibu wa kubadilisha Katiba.

11.7 IBARA YA 120: Utaratibu wa kutunga sheria

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kutunga sheria. Kamati mbili zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati kumi zilizobaki zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali ili kuboresha Ibara hii, kwa kufuta neno ''**Tanganyika**'' katika ibara ndogo ya (4) na badala yake kuandika neno ''**Tanzania Bara**'' ili kuendana na muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa. Aidha, imependekezwa kufanya marekebisho mengine katika ibara ndogo ya (2) kwa kuongeza maneno ''**au Mbunge**'' ili kutoa nafasi kwa Mbunge yeyote kupata fursa ya kuandaa Muswada wa Sheria na Muswada huo wa Sheria unaweza kupitishwa iwapo utaungwa mkono kwa zaidi ya nusu ya kura za Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada kutafakari mapendekezo hayo, imekubaliana na pendekezo la kuruhusu muswada wa sheria uweze kuandikwa na Serikali, Kamati ya Bunge, Kikundi cha Wabunge au Mbunge kama

ilivyopendekezwa kwenye ibara ndogo ya (2). Aidha, ibara ndogo ya (4) imerekebishwa kwa kuondoa sharti la muswada wa sheria, kuhesabiwa kuwa umepitishwa kwa kuungwa mkono kwa wingi wa theluthi mbili ya kura za Wabunge kutoka pande zote mbili za Muungano na badala yake muswada huo uweze kuungwa mkono kwa wingi wa kura za wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na hoja hizo, Ibara hii imefanyiwa marekebisho na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 130 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.8 IBARA YA 121: Utaratibu wa kutunga Sheria kuhusu mambo ya Fedha

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Utaratibu wakutunga sheria kuhusu mambo ya fedha. Kamati zote zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Aidha, Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo hayo na inapendekeza ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 131 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.9 IBARA YA 122: Madaraka ya Rais kuhusu Muswada wa Sheria

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Madaraka ya Rais kuhusu Muswada wa Sheria. Kamati tano zimependekeza Ibara

hii ibaki Kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati saba zimependekeza marekebisho mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika Ibara hii upya ili kuweza kuainisha utaratibu mzuri wa kufuatwa wakati wa kutunga Muswada wa sheria. Endapo, Bunge litapitisha Muswada wa Sheria, Muswada huo hautakuwa sheria mpaka uwe umekubaliwa na kutiwa saini na Rais ndani ya siku thelathini. Iwapo Rais ataukataa Muswada huo, utarudishwa Bungeni pamoja na maelezo ya sababu za kuukataa. Muswada huo utajadiliwa tena Bungeni na utatakiwa uungwe mkono na wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Muswada utarudishwa kwa mara ya pili kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake, basi Rais atatakiwa kuukubali na iwapo hataukubali Muswada huo itabidi alivunje Bunge na aitishe Uchaguzi Mkuu. Sababu ya mapendekezo haya ni kumwezesha Rais kuwa na mamlaka juu ya Muswada wowote wa Sheria unaotungwa na Bunge kwa kuwa yeye ni sehemu ya Bunge. Mapendekezo haya ni tofauti na yaliyoko katika Rasimu ya Tume ambayo yalikuwa yanalipa mamlaka Bunge ya kupitisha Muswada wa Sheria ambao umekwishakataliwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi kwa kuzingatia mapendekezo hayo, imefanya marekebisho ibara ndogo ya (1) ili kutambua madaraka ya Bunge ya Kutunga Sheria kwa kuupeleka Muswada kwa Rais kwa ajili ya kutiwa saini kabla ya kuwa Sheria. Pia, Kamati ilifanya marekebisho katika ibara ndogo ya (4) na (6) ili ziweze kuongeza muda ambao Muswada utapelekwa kwa Rais kupata kibali chake kutoka siku sitini hadi miezi sita na kuweka masharti kwa Rais kuweza kulivunja Bunge pale ambapo Muswada huo utakuwa haujakubalika tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 132 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

11.10IBARA YA 123: Kupitishwa kwa hoja za Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kupitishwa kwa hoja za Serikali, Kamati tatu zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati tisa zimependekeza marekebisho ya kuiandika upya. Mapendekezo hayo yamelenga kuweka masharti yatakayomwezesha Rais kulivunja Bunge pale ambapo Bunge litakataa, kwa mara ya pili, kupitisha hoja ya Bajeti ya Serikali. Sababu ya marekebisho haya ni kumpa mamlaka Rais ya kulivunja Bunge na kuitisha Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi wa hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hiyo isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 133 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.11 IBARA YA 124: Uchaguzi wa Wabunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uchaguzi wa Wabunge. Kamati kumi na mbili zimependekeza marekebisho kwa kufuta baadhi ya maneno katika ibara ndogo ya (4) na (5) ili kuondoa sharti la kufanya uchaguzi mdogo wa kuwapata Wabunge kutokana na wabunge waliokuwepo kupoteza nafasi zao. Kwa kuwa masharti yaliyokuwa yamewekwa katika ibara ndogo za (4) na (5) yalikuwa yanataka Tume Huru ya Uchaguzi kumtangaza kuwa Mbunge mtu mwingine kutoka katika orodha ya majina ya wagombea yaliyowasilishwa na chama chake cha siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na pendekezo jingine la kufanyia marekebisho katika ibara ndogo ya (3). Pendekezo hilo lililenga kuzuiakufanyika kwa uchaguzi mdogo endapo uchaguzi huo unapangwa kufanyika ndani ya kipindi cha miezi kumi na miwili kabla ya uchaguzi mkuu. Sababu za kutaka kufanya marekebisho haya ni kuondokana na matumizi makubwa ya fedha kwa ajili ya kuendesha uchaguzi kwa kuwa kipindi kinachokuwa kimebaki ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilikuwepo pia pendekezo la kufuta ibara ndogo za (4), (5) na (6) ambalo Kamati ya Uandishi ilikubaliana nalo ili wananchi waweze kupata haki yao ya msingi ya kuchaguliwa au kuchagua viongozi ambao wanawataka badala ya kuhamishia majukumu hayo kwa Tume Huru ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo hayo, inapendekeza ibara hiyo isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 134 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.12IBARA YA 125: Sifa za Kuchaguliwa kuwa Mbunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu sifa za kuchaguliwa kuwa mbunge. Kamati zote zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali. Aidha, miongoni mwa maboresho hayo ni kuondoa sifa za kumtaka mtu yeyote anayetaka kugombea nafasi ya kuwa mbunge sharti awe na elimu ya kidato cha nne, pia kuondoa dhana ya uwepo wa Nchi Washirika na kuweza kulifuta neno hilo kila linapojitokeza ili kuendana na Mfumo wa Serikali mbili unaopendekezwa kwa sasa. Vile vile, kulikuwa na mapendekezo ya kuboresha ibara ndogo ya (5) ili kuwaongeza Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu kuwa miongoni mwa watumishi wa umma ambao hawatakiwi kugombea nafasi ya ubunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo hayo imekubaliana na maoni ya Kamati nyingi ya kutaka sifa ya elimu kwa mtu anayegombea nafasi ya ubunge awe ni mtu ambaye anajua kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza ili kuweza kutoa fursa kwa watu wenye uwezo wa kugombea kuweza kugombea. Aidha, Kamati ya Uandishi imeridhia pendekezo la kuwepo mgombea huru katika nafasi ya ubunge.

Aidha, pendekezo la kumzuia mtu mwenye madaraka kugombea nafasi ya ubunge limezingatiwa na Kamati ya Uandishi kwa kufuta sharti hilo, ili lizingatiwe katika Ibara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo hayo imerekebisha Ibara hiyo na itasomeka kama ilivyo katika Ibara ya 135 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.13IBARA YA 126: Utaratibu wa Uchaguzi wa Wabunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge. Kamati kumi na moja zimependekeza ibara hii Ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati moja imependekeza kuifanyia marekebisho ibara ndogo ya (2) kwa kuweka sharti la kuwasilisha majina ya wagombea uchaguzi katika majimbo ya uchaguzi kwenye Tume Huru ya

Uchaguzi, kwa mujibu wa utaratibu utakaoainishwa katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kupitia mapendekezo hayo imeirekebisha ibara hii kwa kuainisha utaratibu wa kuwapata wabunge ambao watapatikana kwa njia ya kuchaguliwa, kupitia majimbo ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara hii isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 136 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.14IBARA YA 127: Kiapo na masharti ya kazi ya Ubunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kiapo na masharti ya kazi ya ubunge. Kamati nane zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati tatu zimependekeza kuifanyia marekebisho mbalimbali ya maboresho ya kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho madogo katika ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "**kama yatakavyopangwa na Tume ya Utumishi wa Umma**" na maneno na "**za nchi**". Sababu ya mapendekezo haya ni kuweza kulitoa jukumu hilo la kuwalipa posho, mishahara na

marupurupu wabunge kutoka kwenye Tume ili litekelezwe kwa mujibu wa Sheria itakayotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo Kamati ya Uandishi imeboresha Ibara hii na inapendekeza isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 137 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.15IBARA YA 128: Kupoteza sifa za Ubunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kupoteza sifa za Ubunge. Kamati saba zimependekeza aya ya (d) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe na Kamati tano zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho madogo yakiwemo kuongeza ibara ndogo ya (1)(g) ili kutoa fursa kwa Rais kutengua uteuzi wa mbunge wa kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo hayo imeongeza aya mpya ya (h) inayoweka sharti la Mbunge aliyetokana na mgombea huru kupoteza sifa za kuwa mbunge kutokana na kujiunga na chama chochote cha siasa. Aidha, Kamati imefanya marekebisho madogo ya kiuandishi kwa kufuta neno "**rufaa**" na badala yake kuweka neno "**rufani**". Vile vile, Kamati inapendekeza kuongezwa kwa maneno "**sheria inayohusu**" katika aya ya (c) ili Mbunge anayevunja sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma apoteze sifa ya kuwa mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 138 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.16IBARA YA 129: Haki ya wapiga kura kumwajibisha Mbunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu haki ya wapiga kura kumwajibisha Mbunge. Kamati moja imependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati saba zimependekeza Ibara hii ifutwe, na Kamati Nne zimependekeza marekebisho madogo ikiwemo kuwepo kwa haki ya wapiga kura kumwajibisha mbunge ambaye ameshindwa kuwasilisha au kutetea kero za wapiga kura wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari maoni hayo inapendekeza ibara hii ifutwe kwa kuwa, haki inayopendekezwa inaweza kutumika vibaya ikiwemo kumwekea vikwazo vya kiutendaji Mbunge aliyeko madarakani. Aidha, wapiga kura wanayo haki ya kumwajibisha kwa kutompigia kura Mbunge katika kipindi cha miaka mitano endapo wananchi wataona Mbunge anayewawakilisha hafai, wanaweza kumwajibisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ifutwe.

11.17. IBARA YA 130: Uamuzi wa suala kama mtu ni Mbunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inaweka utaratibu wa chombo cha Mahakama kupokea malalamiko juu ya uhalali wa uchaguzi au kukoma kwa mtu kuwa na nafasi ya madaraka ya Ubunge na pia kutungwa kwa sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusiana na utaratibu wa kupeleka malalamiko hayo mahakamani. Kamati kumi na moja zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati moja imependekeza ifanyiwe marekebisho kwa kulitaka Bunge kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu watu wanaoweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa ajili ya kupata uamuzi wa suala kama mtu ni Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari pendekezo hili na kuona kuwa halibadilishi maudhui ya Ibara hii kwa kuwa ibara ndogo ya (2) imeweka masharti kuwa Bunge linaweza kutunga sheria kuhusu masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na pendekezo hili na mjadala ndani ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 139 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

11.18. IBARA YA 131: Tamko Rasmi la Wabunge kuhusu Maadili ya Uongozi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Tamko Rasmi la Wabunge kuhusu Maadili ya Uongozi ambapo, Kamati kumi na moja zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati moja imependekeza marekebisho katika ibara ndogo ya (1) kwa kumtaka mtu anayetoa Tamko Rasmi la Mali kwenye Tume ya Maadili ya uongozi kufanya hivyo ndani ya siku tisini badala ya siku thelathini inayotamkwa kwenye Rasimu ya Tume ili kumpa Mbunge muda wa kutosha kuwasilisha Tamko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kuchambua na kuzingatia mapendekezo ya Kamati hii, imefanya marekebisho madogo ya kiuandishi kwa kufuta maneno "**Uongozi na uwajibikaji**" na kuweka maneno "**Maadili ya Viongozi wa Umma**" na maneno "**kwamba hajapoteza sifa za kuwa Mbunge**" na badala yake kuweka maneno "**kuhusu mali na madeni**" katika ibara ndogo ya (1). Aidha, mapendekezo ya kuongeza muda wa mtu kutoa Tamko Rasmi la mali kwenye Tume ya Maadili ya Uongozi kutoka siku thelathini hadi tisini halijazingatiwa na Kamati ya Uandishi kwa sababu mapendekezo ya Kamati nyingi ilikuwa zibaki siku thelathini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika Ibara hii kama inavyoonekana katika Ibara ya 140 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.19IBARA YA 132: Spika na mamlaka ya Spika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Spika na Mamlaka ya Spika. Kamati tano zimependekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza. Aidha, Kamati saba zimetoa mapendekezo ya maboresho kwa kufuta neno "**na"** baada ya neno **"wabunge"** na kuongeza maneno **"kutoka miongoni mwa watu ambao ni wabunge au wenye sifa za kuwa wabunge"** kwenye ibara ndogo ya (1), kufuta neno **"mbunge"** kabla ya maneno **"au mtu mwenye"** katika ibara ndogo ya (2), kufuta maneno **"za nchi"** baada ya maneno **"na Sheria"** na badala yake kuweka maneno **"iliyotungwa na Bunge"** katika ibara ndogo ya (3) na kupendekeza kuwa Mbunge awe miongoni mwa watu wanaoruhusiwa kushika madaraka ya Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchambua na kuzingatia mapendekezo ya Kamati za Bunge na mijadala Bungeni, Kamati ya Uandishi imeifuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (1) ili kumuwezesha Spika wa Bunge kuchaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge au watu wenye sifa za kuwa

Wabunge. Aidha, imekubaliana na pendekezo la kufuta neno "**Mbunge**" katika ibara ndogo ya (2) ili kumwondoa Mbunge katika orodha ya watu wanaokosa sifa za kugombea nafasi ya Spika.

Aidha, Kamati ya Uandishi, imepunguza siku za mtu aliyechaguliwa kuwa Spika kuwasilisha Fomu za Tamko Rasmi la Mali kwa Rais kutoka siku thelathini zilizowekwa awali kuwa siku kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika Ibara hii upya kama inavyoonekana katika Ibara ya 141 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.20IBARA YA 133: Ukomo wa Spika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu ukomo wa Spika kushika nafasi ya madaraka ya Spika. Kamati saba zimependekeza aya (a) ya ibara ndogo ya (1) ifutwe kwa kuwa inawanyima wabunge fursa ya kugombea nafasi ya Spika na Kamati tano zimependekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kuyatafakari mapendekezo ya Kamati zote kwa umakini, imeifuta aya ya (a) kwenye ibara ndogo ya (1) na imeongeza

aya mpya ya (g) inayoweka sharti la Spika kukoma kuwa Spika kwa kujiuzulu.

Aidha, Kamati imefanya maboresho madogo ya kiuandishi katika ibara ndogo ya (2) ili kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya ibara hii na inasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 142 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.21 IBARA YA 134: Naibu Spika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inamhusu Naibu Spika. Kamati moja imependekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati kumi na moja zimependekeza kuifanyia Ibara hii marekebisho mbalimbali kwa, kufuta Ibara ndogo ya (2) kwa kuwa ni ya kibaguzi, kufuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya, kufuta aya za (a) na (d) ya ibara ndogo ya (3) na Kamati saba zimependekeza kuwa neno "**Mbunge**" lifutwe miongoni mwa watu wanaokosa sifa za kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kuyapitia na kuyatafakari mapendekezo ya Kamati zote imekubaliana na pendekezo kuwa Naibu Spika atoke miongoni mwa wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati na mijadala mbalimbali ndani ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kiuandishi ili iweze kusomeka vizuri kama inavyoonekana katika Ibara ya 143 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.22IBARA YA 135: Sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika. Katika Ibara hii Kamati mbili zimependekeza kuwa Ibara hii ifutwe na kuandikwa upya, wakati Kamati mbili zimependekeza ibara ibaki kama ilivyo, Kamati nane zimependekeza kuwa ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kuweka kigezo kuwa mtu anayetaka kuwa Spika au Naibu Spika, sharti awe na elimu ya shahada ya Chuo Kikuu katika fani za uongozi, sheria au utawala. Kamati moja ilipendekeza umri wa juu wa mgombea kuwa miaka sabini na nyingine zimependekeza kufuta sharti linalomtaka mtu anayegombea nafasi hii kuwa na shahada na viongozi wanaogombea wasiwe viongozi wa juu wa vyama vya siasa na katika kipindi ambacho ni Spika pia asiwe kiongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kupitia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali imekubaliana na pendekezo la kuweka kigezo cha umri wa juu kwa mgombea nafasi ya Spika kuwa umri usiozidi miaka sabini. Aidha, mapendekezo mengine hayakuzingatiwa kwa kuwa mtu akishachaguliwa kuwa mbunge anakuwa na sifa pia za kuchaguliwa kuwa Spika na Naibu Spika bila ya kujali kigezo cha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Kamati ya Uandishi imeifuta na kuiandika tena Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 144 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

11.23IBARA YA 136: Utaratibu wa uchaguzi na kiapo cha Spika na Naibu Spika

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara hii, Kamati moja imependekeza maboresho madogo ya kiuandishi, Kamati tano zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati saba zimependekeza kufanyia marekebisho mengine madogo kwa kuongeza kigezo cha jinsia katika uteuzi wa Spika na Naibu Spika na kupendekeza watu wasio wabunge pia waweze kupewa nafasi ya kugombea nafasi ya Spika au Naibu Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyazingatia mapendekezo yaliyotolewa ya kutaka Spika na Naibu Spika kuchaguliwa kwa msingi kwamba, endapo Spika atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Naibu Spika atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano ili kuimarisha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzingatia maboresho hayo Kamati ya Uandishi imeifuta na kuiandika upya ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 145 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.24IBARA YA 137: Katibu wa Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Katibu wa Bunge. Kamati sita hazikuwa na maboresho katika ibara hii, na Kamati sita zilizobakia zimefanya marekebisho mbalimbali kwa kuondoa kigezo cha kushika madaraka ya juu katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na badala yake uteuzi uzingatie watu wenye weledi na uzoefu katika utumishi wa umma ambao watashindanishwa kwa njia ya usaili. Aidha, kulikuwa na mapendekezo ya kubadilisha Tume ya Uteuzi kutoka Tume ya Utumishi wa Umma na badala yake Tume hiyo iitwe Tume ya Utumishi wa Bunge na pia kulikuwa na pendekezo la kutaka Katibu wa Bunge athibitishwe na Bunge baada ya kuteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati ya Uandishi imeona haja ya Katibu wa Bunge kuteuliwa kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Bunge. Kwa kuwa utumishi wa Jamhuri ya Muungano uko mikononi mwa Tume ya Utumishi wa Umma. Hivyo, ni bora mtu huyo akapatikana kwa mujibu wa utaratibu ambao umewekwa katika Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba inayopendekezwa. Aidha, suala la kutaka Katibu wa Bunge kuthibitishwa na Bunge halikuzingatiwa kwa sababu Katibu wa Bunge atakuwa amependekezwa na Tume ya Utumishi wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo haya Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara hii isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 146 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekeza.

11.25IBARA YA 138: Sekretariati ya Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii inayohusu Sekretarieti ya Bunge, Kamati tisa zilipendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba na Kamati tatu zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kwa kufuta maneno "**kutoka pande mbili za Jamhuri ya Muungano**" katika ibara ndogo ili kuondoa dhana ya watumishi wa Bunge kutoka pande zote za Jamhuri ya Muungano na kuongeza maneno "**sifa za kitaaluma**" ili

Bunge liwe na watumishi watakaopatikana baada ya kuwa na sifa za kitaaluma zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia mapendekezo haya Kamati ya Uandishi imeona kuwa kuondoa maneno **"kutoka pande mbili za Jamhuri ya Muungano"** katika ibara ndogo ya (1) haitakuwa ni jambo jema kwa kuwa inaweza kuleta mgogoro na manung'uniko ya kero za Muungano katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano. Aidha, pendekezo la kuongeza sifa za kitaaluma limekubaliwa ili kuweza kuteua watumishi ambao wana sifa zinazostahili za kushika nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia marekebisho hayo Ibara hii imerekebishwa na itasomeka kama ilivyo katika Ibara ya 147 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.26IBARA YA 139: Kanuni za Kudumu za Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii inahusu Utaratibu wa Shughuli za Bunge. Kamati tisa zilipendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba na Kamati nne zilipendekeza marekebisho mbalimbali kwa kufuta maneno "**zinaweza kuweka**" na badala yake kuweka maneno "**itaweka**"yaliyopo katika ibara ndogo ya (2) na kurekebisha ibara ndogo ya (2) ili iweze kuwa na mtiririko mzuri wa kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo ya Kamati imeona kuwa ipo haja ya kurekebisha ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "**zinaweza kuweka**" na badala yake kuweka maneno "**zitaweka**". Sababu ya kuyakubali mapendekezo haya ni kuziwezesha Kanuni za Bunge zinazotungwa ziweze kuweka utaratibu wa namna ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za Kamati ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika ibara hii kama inavyoonekana katika Ibara ya 148 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.27IBARA YA 140: Rais kulihutubia Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii inahusu Rais kulihutubia Bunge. Kamati mbili zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati Kumi zilipendekeza marekebisho mbalimbali katika ibara ndogo ya (2) kwa kufuta neno "**mwandamizi**" na kuweka maneno "**Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais**" na kufuta maneno "**Waziri Mwandamizi**" na kuweka maneno "**Waziri Mkuu na Makamu wa Tatu wa Rais**" na vile vile, kufuta maneno "**Waziri Mwandamizi**" na kuweka maneno **"Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo ya Kamati zote imekubaliana na pendekezo la kufuta maneno "Waziri Mwandamizi" kwa kuwa mfumo ambao unapendekezwa sasa hautakuwa na "Waziri Mwandamizi na badala yake kutakuwa na **"Waziri Mkuu" ambaye atakuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia mapendekezo hayo Ibara hiyo imerekebishwa na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 149 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.28IBARA YA 141: Mikutano ya Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu mikutano ya Bunge. Kamati saba zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, Kamati mbili hazikupendekeza chochote, na Kamati tatu zimependekeza marekebisho mbalimbali kwa kupendekeza Mikutano ya Bunge iwe ya aina mbili, Mikutano ya kujadili Mambo ya Muungano ambayo wajumbe wake watakuwa ni Wabunge wote wa Tanzania Bara na Wabunge wote wa Baraza la Wawakilishi na Mikutano ya kujadili mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu Tanzania Bara ambayo wajumbe wake watakuwa ni Wabunge wote wa Tanzania Bara. Vile vile, kulikuwa na pendekezo la kutaka kuweka muda maalum kwa Rais kuitisha Bunge Jipya na kutaja mahali ambapo Bunge kwa kawaida hufanyia mikutano yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati zote na mijadala katika Bunge, Kamati ya Uandishi inapendekeza kwamba pendekezo la kuwa na mikutano ya aina mbili liachwe kwa sababu ya ugumu katika utekelezaji wake, na katika Ibara inayohusu muundo wa Bunge la Jamhuri ya Muungano hakukuwa na pendekezo la kuwa na mabunge mawili ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, pendekezo la kuweka muda maalum kwa Rais kuitisha Bunge Jipya, Kamati ya Uandishi iliona kuwa halina ulazima, na kwamba hakuna haja ya kutaja ndani ya Katiba mahali Bunge linapofanyia Mikutano yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Ibara ya 150 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

11.29IBARA YA 142: Uongozi na vikao vya Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii inahusu Uongozi na vikao vya Bunge, Kamati kumi na moja zimependekeza ibara ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati moja imependekeza aya ya (c) iandikwe upya ili kuweka utaratibu wa kuendesha vikao vya Bunge kwa kutoa fursa kwa Wabunge kumteua Mbunge mmoja wapo kuendesha vikao, pale ambapo Spika na Naibu Spika wanapokuwa hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali, Kamati ya Uandishi inakubali kwamba, upo uwezekano wa Spika na Naibu Spika kutokuwapo kwa wakati mmoja hivyo umuhimu wa kutoa fursa kwa Mbunge atakayeteuliwa na Wabunge wenzake aweze kuendesha vikao ili kuondokana na uwezekano wa kusitisha shughuli za Bunge pindi itakapotokea kuwa Spika na Naibu Spika hawapo wakati wa vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara ifanyiwe marekebisho na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 151 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

11.30 IBARA YA 143: Akidi ya Vikao vya Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Akidi ya Vikao vya Bunge. Kamati kumi na moja zilipendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati moja imependekeza kufanya marekebisho katika ibara ndogo ya (1) kwa kuongeza maneno "**wakati wa kufanya maamuzi itakuwa**" baada ya neno "**Bunge**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi haikukubaliana na pendekezo hilo kwa kuwa halitabadilisha maudhui ambayo yamekusudiwa na hivyo kupendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na itasomeka kama ilivyo katika

Ibara ya 152 Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.31 IBARA YA 144: Kamati za Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kamati za Bunge. Kamati zote kumi na mbili zilipendekeza Ibara ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo hayo na Ibara hii itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 153 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.32 IBARA YA 145: Uhuru wa Majadiliano Bungeni

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uhuru wa majadiliano Bungeni. Kamati nane zimependekeza Ibara ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu na Kamati nne zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kuboresha ibara ndogo ya (4) itakayolipa Bunge mamlaka ya kutunga Sheria kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo ya Kamati zote, imeona hakuna haja ya kuboresha ibara ndogo ya (4) kwa kuwa maudhui yaliyopo yanajitosheleza. Hata hivyo, Kamati ya Uandishi imeboresha ibara ndogo ya (3) ili kuweza kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 154 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.33 IBARA YA 146: Mipaka ya majadiliano Bungeni

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mipaka ya majadiliano Bungeni. Kamati Kumi zimependekeza Ibara ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati mbili zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo hayo inapendekeza Ibara hii ifutwe kwa vile maudhui yake yamezingatiwa katika ibara inayohusu uhuru wa majadiliano Bungeni. Aidha, Kamati ya Uandishi ina maoni kuwa endapo Mbunge atapewa fursa ya kuthibitisha hoja yake kwa kutumia vyombo vya habari upo uwezekano wa kutoa taarifa ambazo si sahihi Bungeni.

11.34 IBARA YA 147: Tume ya Utumishi wa Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Tume ya Utumishi wa Bunge. Kamati tano zilipendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo na Kamati saba zilipendekeza kuwaongeza Waziri Mkuu na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge.

Vile vile, ilipendekezwa kuongeza idadi ya Wabunge wataokuwa wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge kwa kuwajumuisha wabunge sita wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia uwiano wa pande mbili za Muungano, jinsia na vyama vyenye uwakilishi Bungeni na wabunge watano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano watakaochaguliwa na wabunge. Pia, imependekezwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi ya Bunge ateuliwe na Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano awe Mwenyekiti wa Tume hii kwa kuwa ndiye kiongozi mkuu wa mhimili huu.

Aidha, Naibu Spika wa Bunge wawili wabaki kuwa Makamu Mwenyekiti kwa kuwa ni wasaidizi wakuu wa Spika.

Vile vile, kutamtambua Waziri anayehusika na masuala ya Bunge kuwa mjumbe wa Tume hii. Sambamba na hilo, idadi ya Wabunge watakaokuwa wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge iongezwe na kufikia idadi ya wajumbe watano badala ya wawili kama ilivyo hivi sasa ili kuwa na uwakilishi mzuri katika uwiano kwa pande mbili za Muungano, vyama vyenye uwakilishi Bungeni, jinsia na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi ilikubaliana na pendekezo la kumuongeza Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ili kuweka uwakilishi wa wapinzani katika Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 155 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.35 IBARA YA 148: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge. Kamati sita zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo. Kamati moja ilipendekeza Ibara hii ifutwe na Kamati tano zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza baadhi ya maneno "**kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na Utumishi wa Umma:"** mwishoni mwa ibara ndogo (2)(c) na kufuta Ibara ndogo ya (2) inayohusu majukumu ya Tume. Vile vile, kulikuwa na pendekezo la kuongeza aya mpya ya (2)(c) itakayohusu uandaaji na usimamiaji wa utekelezaji wa mipango na Bajeti ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapitia mapendekezo ya Kamati, Kamati ya Uandishi imeona kuwa ibara ndogo ya (2)(c) ibaki kama ilivyo isipokuwa iongezwe maneno "**kwa kuzingatia muongozo uliotolewa na utumishi wa umma**" kwa

kuwa maneno yanayopendekezwa kuongezwa hayatabadili maudhui ambayo yamekusudiwa. Aidha, mapendekezo ya kuongeza aya mpya itakayohusu uandaaji na usimamiaji wa utekelezaji wa mipango na Bajeti ya Bunge, Kamati ya Uandishi imependekeza Ibara hii ibaki kwa sababu imeshatoa fursa ya kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria mahsusi ambayo pamoja na mambo mengine itazungumzia masuala ya Utumishi wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imerekebisha ibara hii na itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 156 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

11.36 IBARA YA 149: Mfuko wa Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mfuko wa Bunge. Kamati kumi na moja zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati moja imependekeza kufanya marekebisho ibara ndogo ya (3) ili kuwezesha kiwango kitakachotengwa na Bunge kizingatie jinsi hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo haya Kamati ya Uandishi, imeandika upya Ibara hiyo kama inavyosomeka katika Ibara ya 157 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA MPYA YA KUMI NA MOJA

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, BARAZA LA MAPINDUZI LA ZANZIBAR NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mapendekezo ya mfumo wa Serikali mbili uliopendekezwa na Wajumbe walio wengi, Kamati ya Uandishi imependekeza kuwepo kwa Sura mpya itakayotambua Kuwepo Kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za mapendekezo haya ni kuitambua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo itatekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na Katiba ya Zanzibar ya 1984. Aidha, mapendekezo haya yanalenga kumtambua Rais wa Zanzibar kama Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atakayechaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984. Ibara hii inatambua Baraza la Mapinduzi la Zanzibar ambalo litakuwa ndicho chombo kikuu cha kumsaidia na kumshauri Rais wa Zanzibar kuhusu masuala ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii imetambua kuwepo kwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambalo litatunga sheria katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza masharti ya Sura hii yasomeke kama inavyopendekezwa katika Ibara ya 158

hadi 161 inayohusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mamlaka yake. Kwa ufupi Ibara ya 159 inahusu Rais wa Zanzibar na mamlaka yake, Ibara ya 160 inahusu Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na kazi zake, na Ibara ya 161 inahusu Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara za 158, 159, 160 na 161 za Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA KUMI
MAHAKAMA YA JAMHURI YA MUUNGANO

SEHEMU YA KWANZA
MISINGI YA UTOAJI HAKI NA UHURU WA MAHAKAMA

12.0 IBARA YA 150: Kuanzishwa kwa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tisa zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, Kamati moja imependekeza kuongeza ibara ndogo mpya inayoongelea Mahakama ya Kadhi, Kamati mbili zimetoa mapendekezo ya kufuta na kuongeza maneno kwa ajili ya kuleta mtiririko wa kiuandishi na kuboresha maudhui yanayolenga kubadili muundo wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyachambua mapendekezo ya Kamati zote na mijadala ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi imeboresha ibara ndogo ya (2) ya Rasimu ya Tume kwa kufuta maneno "**itakuwa na mamlaka kutoka kwa wananchi na**" badala yake yasomeke "**mujibu wa katiba hii na sheria nyingine yoyote**" ili Mahakama iweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa katiba na sheria, kwa lengo la kuzingatia dhana ya uhuru wa Mahakama kama inavyosomeka katika Ibara ya 162 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.1 IBARA YA 151: Misingi ya utoaji haki

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu misingi ya utoaji haki. Kamati tisa zimependekeza kwamba maudhui ya ibara hii yamejitosheleza hivyo ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati moja imependekeza Ibara hii ifutwe na kuandikwa upya. Aidha, Kamati mbili zimependekeza kuongeza neno "**kidini**" baada ya neno "**kisiasa"** lililopo katika aya ndogo ya (a) ili kuongeza vigezo vinavyokataza mtu kunyimwa haki. Kamati mbili zimetoa mapendekezo ya kufuta na kuiandika upya Ibara hii ili kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeifuta na kuiandika upya aya ya (a) ili kuweka muktadha utakaozuia ubaguzi wa aina yoyote. Hivyo, inapendekezwa Ibara hii iandikwe upya kama inavyosomeka katika Ibara ya 163 ya Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa.

12.2 IBARA YA 152: Uhuru wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii, Kamati tisa zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo. Kamati moja imependekeza kufanya marekebisho katika ibara ndogo ya (1) kwa kuondoa maneno **"ya Jamhuri ya Muungano"** na badala yake kuweka maneno "**zote"** na kufuta ibara ndogo ya (2)

mpaka (6) na Kamati mbili zimependekeza kutenganisha masharti ya ibara ndogo ya (1) na (2) zinazohusu "**Uhuru wa Mahakama**" kwa upande mmoja, na ibara ndogo ya (3), (4), (5) na (6) zinazohusu "**Maslahi ya Majaji**" na kuzijumuisha kwa pamoja katika Ibara mpya**.** Aidha, pendekezo lingine lililotolewa ni kuongeza maneno **"Jaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano"** katika ibara ndogo ya (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo yaliyotolewa hivyo, Kamati imefanya marekebisho katika ibara ndogo ya (1) kwa kuongeza maneno **"Uhuru wa Mahakama"** ambao haupaswi kuishia kwenye Mahakama za Juu pekee, bali kwenye Mahakama zote ikiwa ni pamoja na Mahakama za chini.

Aidha, Kamati inapendekeza ibara ndogo za (2) hadi (6) zibaki kama ilivyopendekezwa kwa sababu, zimenyambulisha masharti yanayohusu dhana ya Uhuru wa Mahakama. Dhana hii inahusisha uhakika wa kulipwa mshahara na malipo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia pendekezo la kuongeza neno "**Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano"** katika ibara ndogo ya (2), (3) na (4) kwa sababu ya kuridhiwa kwa pendekezo la kuwepo kwa Mahakama Kuu

ya Jamhuri ya Muungano, na hivyo kuiongeza nafasi ya Jaji wa Mahakama Kuu kwenye ibara hizi ndogo ili waweze pia kunufaika na masharti yaliyoainishwa katika ibara ndogo hizo.

Baada ya ufafanuzi huo, Kamati ya Uandishi, imeiandika upya Ibara hii na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 164 ya Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa.

12.3 IBARA YA 153: Muundo wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu muundo wa Mahakama. Kamati za Bunge Maalum zimetoa mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha ibara hii kama ifuatavyo:

(a) Ibara ndogo ya (1):

(i) Kamati sita zimependekeza ibara ibaki kama ilivyo;

(ii) Kamati moja imependekeza kufuta Ibara nzima na kuiandika upya ili kuanzisha Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977;

(iii) Kamati moja imependekeza kufuta neno "**na**" kwenye ibara ndogo ya (i) mwishoni mwa aya ya (a); ili kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi;

(iv) Kamati mbili zimependekeza kuongeza aya mpya ya (c) kwenye ibara ndogo ya (1) itakayoanzisha Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na

Mahakama Kuu ya Zanzibar kwenye muundo wa Mahakama za Jamhuri ya Muungano;

(v) Kamati moja imependekeza kuongeza aya mpya ya (c) itakayoanzisha Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na kuongeza aya mpya ya (d) itakayotaja Mahakama za Mahakimu zitakazoanzishwa na sheria ya Bunge; na

(vi) Kufuta neno "**Juu"** kwenye aya ya (a) na badala yake kuweka neno "**Kuu"** ili kufuta Mahakama ya Juu na kuanzisha Mahakama Kuu.

(b) Ibara ndogo ya (2):

(i) Kamati moja imependekeza kufuta ibara nzima na kuiandika upya ili kuanzisha Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na mamlaka yake kama ilivyo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

(ii) Kamati moja ilipendekeza kufuta ibara ndogo ya (2);

(iii) Kamati tisa zimependekeza kufuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (2) ili iendane na maudhui au muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa na wajumbe walio wengi. Aidha, Kamati hizo zimependekeza kufuta maneno **"Nchi Washirika",** "**Tanganyika**" na badala yake kuweka maneno "**Tanzania Bara",** au **"Tanzania Bara na Zanzibar",**

au"Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar";

(iv) Kamati moja imependekeza kuongeza maneno **"na yasiyo ya Muungano"** ili kuzipa mamlaka sawa Mahakama Kuu za pande zote mbili kusikiliza katika ngazi za awali, mashauri ya madai na jinai kuhusu Mambo yasiyo ya Muungano kwenye maeneo yao ya utawala;

(v) Kuongeza neno "**yao**" baada ya maneno "**maeneo**"; na

(vi) Kuongeza ibara ndogo mpya itakayosomeka:

"(3) Bunge litatunga sheria itakayosimamia Mahakama za chini na vyombo vya utoaji haki."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imetafakari mapendekezo ya Kamati mbalimbali na inaona ni muhimu kuwa na Mahakama ya Juu kwa sababu, inapanua wigo wa ngazi za Mahakama ya Jamhuri ya Muungano na kutoa fursa na haki ya kukata rufaa kwa wananchi katika Mahakama ya Juu ambayo, inapendekezwa kuwa ni chombo cha mwisho cha utoaji haki. Vilevile, muundo wa Mahakama unaopendekezwa unaenda sambamba na utaratibu uliopo katika nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imejiridhisha kwamba upo umuhimu wa kuongeza aya mpya ya (c) itakayoitaja Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa ni moja ya Mahakama zitakazoanzishwa chini ya Ibara hii kwa sababu katiba hii pia itatumika kwa mambo yasiyo ya Muungano kwa Tanzania Bara. Aidha, pendekezo hili linaenda sambamba na maoni mbalimbali yaliyotolewa na Kamati za Bunge na mijadala ndani ya Bunge Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kuyachambua mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali za Bunge na mijadala ndani ya Bunge kuhusu ibara ndogo ya (2), imeona ni muhimu kuwekwa kwa masharti yatakayowezesha Mahakama Kuu ya Zanzibar kutekeleza mamlaka yake kwa kiasi kile kile kinachoweza kutekelezwa na Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa kuzingatia hoja zilizoelezwa hapo juu, Kamati ya Uandishi, imeandika upya Ibara hii na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 165 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.4 IBARA YA 154: Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano. Kamati zilikuwa na mapendekezo kama ifuatavyo:

(a) Kamati tisa zimependekeza ibara ndogo ya (1) ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume;

(b) Kamati moja ilipendekeza kufuta ibara nzima ya 154 inayoanzisha Mahakama ya Juu na kuiandika upya ili kuweka muktadha wa kuanzisha Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano pamoja na mamlaka yake;

(c) Kamati moja ilipendekeza kufuta neno **"Juu"** kwenye maelezo ya pembeni ya ibara hii, na mstari wa mwisho wa ibara ndogo ya (1) na badala yake kuweka neno **"Kuu";** ili kufuta Mahakama ya Juu na kuweka Mahakama Kuu;

(d) Kamati moja imependekeza kufuta na kuandika upya aya za (a),(b) na (c) za ibara ndogo ya (2) na kuongeza aya mpya ya (d) ili zisomeke kwa muktadha ambao utamtaja **"Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano"**, **Naibu Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano", "Jaji Kiongozi"** na **"Majaji wengine kama itakavyoonekana inafaa"**;

(e) Kamati moja ilipendekeza kufuta maneno **"wasiopungua saba"** kwenye ibara ndogo ya (1) aya ya (c) na badala yake kuweka maneno **"wasiopungua watano na wasiozidi saba";** ili kuweka ukomo wa chini na juu wa idadi ya Majaji; na

(f) Kamati moja imependekeza kufuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya kwa kuweka utaratibu wa uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imeyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali kuhusu Ibara hii yakiwemo kuibakiza Ibara hii na mapendekezo ya kuifuta Mahakama ya Juu na badala yake kuweka Mahakama Kuu na kumtaja Jaji Kiongozi. Kamati ya Uandishi imezingatia kuwa kwa sababu upo umuhimu wa kuanzisha Mahakama ya Juu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watu wanapata fursa zaidi na haki ya kukata Rufaa katika Mahakama ya Juu kama inavyopendekezwa kuwa ni kwa ajili ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pendekezo la kuiandika upya ibara ndogo ya (1) aya (c) kwa madhumuni ya kuweka idadi ya majaji wengine wa Mahakama ya Juu kuwa ni majaji wasiopungua watano (5) na wasiozidi saba, badala ya majaji wasiopungua saba, kama inavyopendekezwa kwenye Rasimu ya Tume, lina msingi kwa sababu, linalenga kuweka ukomo wa idadi ya chini na ukomo wa idadi ya juu kwa majaji wengine wa Mahakama ya Juu watakaoteuliwa kwa mujibu wa Katiba.

Vilevile, pendekezo hilo linazingatia kuwepo kwa idadi sahihi ya namba ya majaji inayoendana na akidi ya vikao vya

Mahakama ya Juu, ya majaji watano inayopendekezwa kwenye Ibara ya 155(1) ya Rasimu ya Tume. Aidha, Kamati ya Uandishi, imefuta ibara ndogo ya (2) na maudhui yake yamezingatiwa kwenye ibara inayohusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeandika upya ibara hii na isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 166 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.5 IBARA YA 155: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya juu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu akidi ya vikao vya Mahakama ya Juu. Kamati kumi zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba na Kamati mbili zimetoa mapendekezo ya kuweka umri wa kustaafu wa Majaji, masharti ya kujiuzulu, kuondolewa katika madaraka na utaratibu wa kumuondoa Jaji katika madaraka yake kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi, imeona kuwa, masuala hayo yanapaswa kuzingatiwa kwenye Ibara zinazohusu muda wa majaji kuwa madarakani na Ibara zinazoweka utaratibu wa kushuhulikia nidhamu ya majaji, kwa kuwa maudhui ya Ibara hii yanahusu akidi ya vikao vya Mahakama ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 167 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.6 IBARA YA 156: Mamlaka ya Mahakama ya Juu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mamlaka ya Mahakama ya Juu. Kamati moja imependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo na Kamati kumi na moja zimetoa mapendekezo mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kufuta maneno **"Nchi Washirika"** na badala yake kuweka **"Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar"** kwenye ibara ndogo ya 1 aya ya (b) (c) na (d) na kila linapojitokeza neno hilo katika Ibara hii;

(b) kuongeza majukumu ya Mahakama kwenye ibara ndogo ya (1) aya ya (b) kwa kuipa mamlaka ya kusikiliza, kusuluhisha na kuamua migogoro baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(c) kufuta na kuandika upya ibara ndogo ya (1) na ya (2) pamoja na kuboresha mpangilio wa namba za ibara ndogo kwa ajili kuweka matumizi ya lugha fasaha na mtiririko mzuri wa kiuandishi;

(d) kuipa Mamlaka Mahakama ya Juu kusikiliza mashauri kutoka kwa wananchi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(e) kuifuta Mahakama ya Juu na mamlaka yake kuipa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano; na

(f) kuweka masharti yatakayoweka utaratibu wa mtu anayeshika madaraka ya ujaji kutoshika madaraka hayo mpaka kwanza awe amekula kiapo cha uaminifu na kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo ya Kamati zote pamoja na mjadala ndani ya Bunge na kuona kwamba ni muhimu kufuta maneno "**Nchi Washirika**" katika ibara hii popote yanapoonekana kwa kuwa yanaashiria uwepo wa Serikali tatu na badala yake Kamati imebadilisha kwa kuandika maneno Jamhuri ya Muungano ili kuendana na Muundo unaopendekezwa wa Serikali Mbili.

Vilevile, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kupanga ibara ndogo ya (3) kuwa ya (4) na ya (4) kuwa ya (3) ili kuweka muktadha unaotaja sheria kabla ya Kanuni, kwa kuwa, Sheria ndiyo inayoanza kutungwa kabla ya Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ya Uandishi imezingatia pendekezo lililotolewa la kuweka masharti ya

kumtaka Jaji wa Mahakama Kuu kula kiapo cha uaminifu kwa kuwa ni muhimu kwa ajili ya kumwezesha Jaji kutekeleza majukumu yake kwa uaminifu na uadilifu. Kwa kuwa Ibara hii inazungumzia mamlaka ya Mahakama ya Juu, Kamati ina maoni kwamba suala la Majaji wa Mahakama Kuu kula kiapo lisiingizwe katika Ibara hii kwa kuwa limezingatiwa katika ibara zinazohusu Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 168 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.7 IBARA YA 157: Madaraka ya Jaji wa Mahakama Juu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Juu. Kamati moja imependekeza Ibara hii ifutwe. Kamati kumi na moja zimependekeza kufanya marekebisho mbalimbali kwa ajili ya kuboresha maudhui kwa: kufuta baadhi ya maneno kwenye ibara ndogo ya (2), kufuta maneno **"Mahakama za Nchi Washirika"** na badala yake kuweka maneno **"Mahakama Kuu ya Jamhuri Muungano wa Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar"** au **"Mahakama Kuu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar, Tanzania Bara au Mahakama Kuu ya Zanzibar**", kufuta na kuandika upya ibara ndogo ya (2), kufuta maneno **"Jaji wa Mahakama ya Rufani au Mahakama za Nchi Washirika"** na badala yake kuweka maneno **"Hakimu katika**

Jamhuri ya Muungano" ili kumwezesha hakimu anayeteuliwa kushika nafasi ya Ujaji kuweza kuendelea kufanya kazi zake katika Mahakama aliyotoka hadi aweze kutayarisha na kutoa hukumu ambazo hakukamilisha kabla ya uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia na kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati pamoja na mijadala Bungeni na inaona kuwa maudhui yaliyopendekezwa na Kamati yanafaa kujumuishwa katika Ibara hii. Mapendekezo ya kuondoa maneno "**Nchi Washirika**" na badala yake kuandika maneno "**Mahakama Kuu ya Tanzania Bara au Mahakama Kuu Zanzibar**" kwa kuwa yanaendana na Muundo wa Serikali Mbili unaopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya mahakimu unasimamiwa na sheria za nchi, Kamati ya Uandishi inapendekeza utaratibu huo unafaa na hivyo uendelee. Kwa msingi wa hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 169 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.8 IBARA YA 158: Uteuzi wa Jaji Mkuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uteuzi wa Jaji Mkuu. Kamati tatu zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati tano zimependekeza kufuta

maneno yanayoweka sharti la kutaka jina la Jaji kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge katika Ibara ndogo ya (1), Kamati nyingine zilipendekeza kufuta maneno "**za Nchi Washirika**" na badala yake kuweka maneno **"Tanzania Bara au Zanzibar au Jamhuri ya Muungano"**. Aidha, Kamati moja imependekeza kufuta na kuiandika upya ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kuyachambua mapendekezo ya Kamati imekubaliana na pendekezo la kufuta maneno "Nchi Washirika" na badala yake imeandika "**Mahakama Kuu ya Tanzania Bara na Mahakama Kuu ya Zanzibar**" kwa sababu maneno hayo yanaakisi muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa.

Aidha, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge pamoja na mijadala ndani ya Bunge Maalum kwamba ni muhimu kutoweka masharti yanayomtaka Jaji Mkuu atakayeteuliwa na Rais kuthibitishwa na Bunge kabla ya kuapishwa. Lengo ni kuhakikisha kwamba hakuna muingiliano wa mihimili ya dola na kudumisha dhana ya uhuru wa Mahakama.

Vile vile, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kiuandishi ili kuweka mtiririko mzuri wa kiuandishi na kuzipa namba upya aya ya (c)(i) na (ii) na kuwa aya za (c) na (d).

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya ibara hii kama inavyoonekana katika Ibara ya 170 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.9 IBARA YA 159: Uteuzi wa Naibu Jaji Mkuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati sita zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo. Kamati moja imependekeza Ibara hii ifutwe na Kamati tano zimependekeza kurekebisha Ibara ndogo ya (1) kwa kufuta maneno "**na kabla ya kuapishwa jina lake litawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge"**.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kupitia mapendekezo hayo, ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati tano ya kuifanyia marekebisho madogo Ibara ndogo ya (1) kwa kuondoa masharti ya kumtaka Naibu Jaji Mkuu kabla ya kuapishwa kwake, kuthibitishwa na Bunge. Lengo ni kuhakikisha kwamba hakuna muingiliano wa mihimili ya dola na kudumisha dhana ya uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mantiki hiyo, Kamati, imeiandika upya Ibara hii kama inavyoonekana katika Ibara 171 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.10IBARA YA 160: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu. Kamati sita zilipendekeza Ibara hii ibaki

kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati sita zilitoa mapendekezo mbalimbali ya maboresho kwenye ibara ndogo ya (1) na (2) kwa kufuta maneno **"Majaji wa Mahakama ya Juu"** yaliyopo katika ibara ndogo ya (1) na badala yake yaandikwe **"Jaji Kiongozi na Majaji wa Mahakama Kuu",** kufuta maneno **"Nchi Washirika"** na badala yake kuweka maneno **"ya Jamhuri ya Muungano au Mahakama Kuu ya Zanzibar"** na kufuta maneno **"za Nchi Washirika"** na kuweka maneno **"ya Jamhuri ya Muungano au Zanzibar".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imetafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali pamoja na mijadala ndani ya Bunge na imefuta maneno "**Nchi Washirika**", lengo ni kuendeleza maudhui ya Muundo wa Serikali Mbili unaopendekezwa kwa sasa na neno Mahakama Kuu lililopo kwenye ibara ndogo ya (2) aya ya (a) linajumuisha Mahakama Kuu za pande zote mbili za Muungano.

Aidha, Kamati ya Uandishi imetafakari pendekezo la kumweka Jaji Kiongozi kama mmoja wapo wa watu watakaoteuliwa kushika nafasi ya Jaji wa Mahakama ya Juu na kuona kuwa Ibara hii inatoa fursa ya uteuzi kwa Jaji yeyote wa Mahakama Kuu na siyo Jaji Kiongozi peke yake kama inavyopendekezwa na Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii na isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 172 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.11IBARA YA 161: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Juu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Juu. Kamati kumi zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati mbili zimependekeza marekebisho kwa kuongeza neno "**Jaji Kiongozi**" baada ya neno "**Jaji Mkuu**". Kamati nyingine imependekeza kuifuta na kuiandika Ibara hii "**kiapo cha**" uaminifu baada ya uteuzi utakaokuwa umewekwa kwa kuwaondoa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu kula kiapo cha uaminifu baada ya uteuzi wao na badala yake awekwe jaji wa Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari pendekezo hili, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo ili kuzingatia maoni ya Kamati nyingi yanayohitaji kuwepo kwa Mahakama ya Juu. Kwa mantiki hiyo, Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 173 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.12IBARAYA 162: Muda wa Kuwa Madarakani Kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu

Mheheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu muda wa kuwa madarakani kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu. Kamati saba zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo. Kamati tano, zimependekeza kufuta neno **"kufariki"** na badala yake kuweka neno **"atafariki"** kwenye ibara ndogo ya (1) aya ya (c) kufuta na kufanya marekebisho kwenye ibara ndogo za (3) na (4) ili kuweka sharti kwamba Jaji Mkuu au Naibu Jaji Mkuu ataachia madaraka pindi umri wa kustaafu ukifika bila kujali kuwa hajamaliza mashauri aliyokwishaanza kusikiliza. Pendekezo lingine lililotolewa ni kufuta maneno "**Mahakama ya Juu"** kila yanapojitokeza na badala yake kuweka maneno "**Mahakama Kuu".** Kamati moja ilipendekeza kufutwa kwa ibara hii na kuandikwa upya kuakisi mfumo unaopendekezwa kwa sasa. Aidha, Kamati moja imependekeza kuongeza ibara ndogo mpya za (5) na (6) zitakazoweka utaratibu wa kumuondoa Jaji wa Mahakama ya Rufani katika Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia mapendekezo haya pamoja na mijadala ya ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi imekubaliana na marekebisho ya kiuandishi yaliyopendekezwa na Kamati mbalimbali ili kuleta mtiririko mzuri wa lugha fasaha na matumizi ya maneno.

Aidha, Kamati ya Uandishi imetafakari pendekezo na kutoweka ukomo kwa Majaji wanaostaafu kukamilisha shughuli

ambazo hawakuzikamilisha kwa kipindi cha muda maalum, kwa sababu Kamati imeona maudhui ya Ibara kama yalivyo, yanajitosheleza. Vile vile, Kamati ya Uandishi, inashauri kuwa pendekezo la kuweka utaratibu wa kumuondoa Jaji wa Mahakama ya Rufani lisiwekwe katika ibara hii kwa kuwa maudhui ya Ibara hii yanahusu muda wa kuwa madarakani Majaji wa Mahakama ya Juu. Aidha, utaratibu wa kumuwondoa madarakani Jaji wa Mahakama ya Rufani umeainishwa katika Ibara ya inayohusu kumwondoa Jaji madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii kama inavyoonekana katika Ibara ya 174 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.13IBARA YA 163: Utaratibu wa Kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu. Kamati saba zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yamejitosheleza. Kamati moja imependekeza Ibara hii ifutwe.

Aidha, Kamati mbili zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kufuta ibara ndogo ya (3) na (4) ili kuwawajibisha Majaji waweze kumaliza majukumu yao yote wakiwa katika nafasi zao za madaraka, kufuta maneno

"**Mahakama ya Juu"** na kuweka maneno "**Mahakama Kuu"** kwa lengo la kuiondoa Mahakama ya Juu na Majukumu ya Mahakama ya Juu yatekelezwe na Mahakama Kuu. Kufuta maneno "**Kaimu Jaji"** na kuweka maneno "**Jaji wa Nyongeza"** katika ibara ndogo ya (2), kwa kuwa ibara ndogo hiyo haitoi dhana ya kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu bali ina maudhui ya kuongeza Jaji mwingine na kurekebisha ibara ndogo ya (5) kwa kuweka dhana ya Jaji Mwandamizi wa Mahakama ya Juu kuweza kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu badala ya nafasi hiyo kushikiliwa na Kaimu Jaji kama ilivyopendekezwa na Rasimu .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kutafakari mapendekezo ya kutoka kwenye Kamati mbalimbali na mijadala ndani ya Bunge, imeona maudhui ya Ibara hii yanajitosheleza na Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 175 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.14IBARA YA 164: Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii inahusu utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu. Kamati nane zimependekeza maudhui ya Ibara hii yabaki kama yalivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati nne

zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kwa kufuta aya ya (a) ya Ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya ili kumpa mamlaka Rais ya kumsimamisha kazi Jaji baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama;

(b) Kufuta maneno "**ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote"** kwenye aya ya (c) ya Ibara ndogo ya (2) ili kuondoa sharti la kumwondoa Jaji madarakani kutokana na maradhi;

(c) Kuongeza maneno "**kwa kipindi kisichozidi siku mia moja na themanini"** baada ya neno "lote" kwenye Ibara ndogo ya 2 aya ya (c) ili kuweka kipindi maalum cha Tume ya kumwondoa Jaji madarakani kukamilisha uchunguzi wake;

(d) Kufuta neno "**mbaya"** kwenye ibara ndogo ya (4) na badala yake kuweka maneno **"inayoweza kuathiri maadili ya kazi"** baada ya maneno **"tabia mbaya",** ili kuweka sharti la tabia mbaya ambazo zinaathiri utendaji wa kazi kuwa iwe ndio kigezo cha Jaji kuondolewa madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati zote na imeona maudhui ya Ibara hii yanajitosheleza kwa sababu mwenendo

wa majaji unatakiwa kuwa ni mzuri muda wote na hivyo tabia mbaya inafaa kuwa ni kigezo cha kumuondoa jaji madarakani itakapothibitika Aidha, pale itakapothibitika kwamba Jaji ameshindwa kumudu majukumu yake kutokana na maradhi, basi Jaji huyo ataondolewa madarakani kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa misingi hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 176 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.15IBARA YA 165: Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mahakama ya Rufani. Kamati nane zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati nne zimependekeza marekebisho katika ibara ndogo kwa kufuta maneno "**za Nchi Washirika"** na badala yake kuweka maneno "**ya Jamhuri ya Muungano na ya Zanzibar",** kufuta maneno "**za Nchi Washirika**" na badala yake kuweka maneno "**ya Jamhuri ya Muungano**" na kufuta na kuandika upya ibara ndogo ya (3) ili kuweza kulipa Bunge la Jamhuri ya Muungano mamlaka ya kutunga sheria kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kuwasilisha rufani mbele ya Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia ibara hii imekubaliana na hoja ya kuifuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (3) kwa sababu Mahakama ya Rufani ni mojawapo ya chombo cha Muungano kitachokuwa kinapokea na kusikiliza rufaa kutoka pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara ndogo ya (3) iandikwe upya katika muktadha huo na inasomeka kama Ibara ya 177 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa**.**

12.16IBARA YA 166: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Rufaa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu akidi ya vikao vya Mahakama ya Rufaa ambayo ni Majaji watatu. Kamati kumi na moja zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati moja imependekeza akidi iwe ni Jaji mmoja kwa masuala yasiyohusu rufaa. Kamati moja imependekeza kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) itakayoweka masharti yatakayompa mamlaka Jaji wa Mahakama ya Rufaa kutekeleza mamlaka ambayo hayahusiki na uamuzi juu ya rufani kama vile kutoa maamuzi juu ya maombi mbalimbali yanayohusu rufaa kwa mashauri ya madai na jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuna umuhimu wa kuongeza ibara ndogo ya (3) ili kumwezesha Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani kutekeleza madaraka yoyote ya Mahakama ya Rufani ambayo hayahusiki na kusikiliza au kutoa uamuzi juu ya rufani, ikiwemo kusikiliza maombi mbalimbali ya jinai na madai. Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi, imeiandika upya Ibara hii kama ilivyo katika Ibara ya 178 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.17IBARA YA 167: Mamlaka ya Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara inahusu mamlaka ya Mahakama ya Rufani. Kamati nne zimependekeza ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati nane zimependekeza kufuta maneno **"za Nchi Washirika"** popote yanapoonekana, na badala yake kuweka moja wapo kati ya maneno yafuatayo" **"Jamhuri ya Muungano na Mahakama Kuu ya Zanzibar"** au **"ya Tanzania na Mahakamu Kuu ya Zanzibar" au "Jamhuri ya Muungano",** Kamati moja imependekeza maboresho ya muundo wa Mahakama ili ujumuishe Mahakama ya Juu, Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo mbalimbali ya Kamati na imekubaliana kufuta maneno "**za Nchi Washirika**" na badala yake imeandika maneno "**ya Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama yoyote ya chini**" kwenye ibara ndogo ya (1) aya za (a) na (b). Lengo la marekebisho hayo ni kuakisi muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa kwa sasa. Aidha, Kamati ya Uandishi, imeongeza maneno "**zilizotungwa na Bunge**" katika ibara ndogo ya (1) aya ya (c) ili kulipa mamlaka Bunge kutunga sheria itakayoainisha mamlaka mengine ya Mahakama ya Rufani.

Aidha, Kamati ya Uandishi imelitafakari pendekezo la kuweka muundo mpya wa Mahakama katika Ibara hii na kuona muundo huu uzingatiwe kwenye sehemu inayohusu Mahakama za Jamhuri ya Muungano.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii ili isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 179 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.18IBARA YA 168: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani. Kamati tano zimependekeza bara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati saba zimependekeza ibara hii irekebishwe katika Ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno **"Nchi Washirika"** na badala yake kuweka maneno **"Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati zote, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo hilo kwa kuwa maneno **"Nchi Washirika"** yanaashiria muundo wa Serikali tatu tofauti na muundo wa Serikali unaopendekezwa kwa sasa. Kwa kuzingatia hoja hiyo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 180 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.19IBARA YA 169: Uteuzi wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani

Ibara ya 169 inahusiana na uteuzi wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. Kamati nne zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati nne zimependekeza kufuta neno "**Nchi Washirika**" na Kamati nane zimependekeza kufutwa kwa maneno "**za Nchi Washirika**" na badala yake kuandika moja wapo kati ya maneno **"Mahakama za Jamhuri ya Muungano", "Jamhuri ya Muungano na Mahakama Kuu ya Zanzibar", Mahakama Kuu**

ya Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar". Aidha, Kamati moja imependekeza kuifuta ibara ndogo ya (1) na kuaindika upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge na mijadala yake, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kurekebisha ibara ndogo ya (1) kwa kuiandika upya kwa madhumuni ya kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi. Aidha, Kamati ya Uandishi imefuta maneno "**Nchi Washirika**" na badala yake imeweka maneno "**ya Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar**" ili kuendana na Muundo wa Serikali Mbili unaopendekezwa na wajumbe walio wengi kwa sasa pamoja na kuweka mojawapo ya sifa za mtu anayeteuliwa kutumikia Mahakama ya Rufani ni kuwa amefanya kazi katika Mahakama Kuu ya Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Kwa sababu hizo Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 181 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa .

12.20IBARA YA 170: Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. Kamati zote kumi na

mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwa sababu maudhui yake yanajitosheleza.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 182 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.21 IBARA YA 171: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu, uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani. Kamati kumi na moja zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwa sababu maudhui yake yanajitosheleza na Kamati moja imependekeza Ibara hii ifutwe.

Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo hayo, imeridhika kuwa maudhui ya Ibara hii kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume inajitosheleza kwa kuwa inaweka masharti ya kumpa mamlaka Rais kuteua Majaji kutoka miongoni mwa majina yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyosomeka katika Ibara ya 183 ya

Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.22IBARA YA 172: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani. Kamati kumi na moja zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati moja imependekeza Ibara hii ifutwe na iandikwe upya kama ilivyo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inaona kuwa ni muhimu kuendelea kuwepo kwa kiapo cha majaji wa Mahakama ya Rufani ili Majaji waweze kutekeleza majukumu yao kwa uaminifu, uadilifu, na kwa kutenda haki. Hivyo, Kamati inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 184 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.23IBARA YA 173: Muda wa kuwa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Majaji wa Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu, muda wa kuwa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Majaji wa Mahakama ya Rufani. Kamati nne zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, Kamati moja

imependekeza ibara hii ifutwe na Kamati saba zimependekeza marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kwenye ibara ndogo ya (1), kwa kufuta maneno **"umri wa miaka sabini**", na badala yake kuweka maneno **"umri wa miaka sabini na tano**";

(b) kwenye ibara ndogo ya (2), kwa kufuta aya ya (a) hadi aya ya (d), kufuta maneno **"umri wa miaka sabini**", na badala yake kuweka maneno **"umri wa miaka sabini na tano**", na pia kuongeza maneno "**ilivyotajwa katika ibara ndogo ya (1) ya Ibara hii"** mwishoni mwa maneno ya utangulizi ya ibara hii ndogo;

(c) kwenye ibara ndogo ya (3), kwa kuongeza maneno "**katika kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili**" mwishoni mwa ibara hii ndogo, kufuta maneno **"au hadi akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla hajatimiza umri wa kustaafu",** na kuifuta na kuiandika upya ili isomeke "**Jaji aliyetimiza umri wa kustaafu atalazimika kustaafu kwa mujibu wa sheria na atakamilisha kazi zake kabla ya kufikia umri huo"**

(d) kuifuta ibara ndogo ya (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na mijadala ndani ya Bunge na kujiridhisha kwamba, ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali na mijadala ndani ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi inapendekeza Jaji aliyetimiza umri wa kustaafu aendelee kusikiliza mashauri aliyokwishaanza kuyasikiliza kabla ya muda wake wa kustaafu hadi atakapoyamaliza. Endapo utaratibu huu hautawekwa, mwenendo mzima wa usikilizaji wa mashauri husika na utoaji maamuzi yanaweza kuathiriwa kwa sababu Jaji mwingine akipewa mashauri hayo ili ayamalizie hataweza kuwa na historia nzuri ya shauri hilo. Hivyo, hawezi kuwa kwenye nafasi nzuri ya kutenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Kamati ya Uandishi haiafiki pendekezo la kuongeza umri wa kustaafu kutoka miaka 70 hadi miaka 75 kutokana na ukweli kwamba hata Kamati zilizopendekeza suala hili hazikutoa sababu za msingi za ongezeko hilo la umri.

Kutokana ufafanuzi huo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama inavyosomeka kwenye Rasimu ya Tume na

isomeke kama ilivyo katika Ibara ya 185 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.24IBARA YA 174: Utaratibu wa kukaimu nafasi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kukaimu nafasi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. Kamati tisa zilipendekeza ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati moja ilipendekeza Ibara hii ifutwe na Kamati mbili zimependekeza marekebisho yafuatayo:

(a) kuifanyia marekebisho ibara ndogo ya (1) kwa kuongeza aya mpya ya (d) inayoweka masharti ya kumtaja Jaji Mwandamizi wa Mahakama ya Rufani kukaimu nafasi ya mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wanapokuwa hawapo kwenye kituo cha kazi;

(b) kwenye ibara ndogo ya (2) kuna mapendekezo mawili, moja la kuitaka Tume ya Utumishi wa Mahakama kumshauri Rais wakati wa kuteua Jaji wa Mahakama ya Rufani badala ya kushauriwa na Jaji Mkuu na pendekezo la pili ni kuifuta ibara ndogo hii na kuiandika upya ili kuwepo na sharti la Jaji Mkuu kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama endapo itahitajika ateuliwe Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani;

(c) kwenye ibara ndogo ya (3), kwa kufuta maneno **"Jaji Mkuu"**, na badala yake kuweka maneno **"Tume ya Utumishi wa Mahakama**";

(d) kuifanyia marekebisho ibara ndogo ya (4), ili itafsiriwe kuwa Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani atapewa muda maalum wa kuwa na madaraka hayo ya kukaimu; na

(e) kwenye ibara ndogo ya (5), kwa kuifuta ibara hiyo ndogo na kuiandika upya ili itafsiriwe kumwezesha Kaimu Jaji kutoendelea na madaraka yake baada ya muda wake wa kukaimu kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, mapendekezo yaliyoainishwa hapo juu yana lengo la kuondoa dhana ya Jaji Mkuu kumshauri Rais kuteua Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani, na badala yake inapendekezwa Tume ya Utumishi wa Mahakama ibebe jukumu la kumshauri Rais kufanya uteuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yote kama yalivyoainishwa hapo juu, Kamati ya Uandishi, imeridhika kwamba ibara hii inahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuhakikisha kwamba uteuzi wa Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani unafanywa na Rais baada ya kushauriwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na si Jaji Mkuu peke yake. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa Ibara ya 180 ya Rasimu ya Tume, Tume ya Utumishi wa Mahakama ni chombo chenye mamlaka ya

kupendekeza majina ya watu wanaoweza kushika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani.

Aidha, Kamati ya Uandishi imeona pia si vyema kwa Jaji Mkuu peke yake kuanzisha mchakato huo wa uteuzi wa nafasi hiyo nyeti katika Mahakama kwa vile kuna uwezekano wa kuyatumia mamlaka hayo vibaya. Hivyo, inapendekezwa Tume ya Utumishi wa Mahakama, ambayo Jaji Mkuu ni Mwenyekiti, ihusike katika mchakato huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ya Uandishi, inapendekeza ibara ndogo za (4) na (5) zibaki kama zilivyo kwenye Rasimu ili kumwezesha Kaimu Jaji aendelee kushika nafasi hiyo mpaka muda wa uteuzi wake utakapokwisha au uteuzi huo kufutwa na Rais, na inapotokea kwamba muda wa uteuzi umekwisha lakini Kaimu Jaji huyo hajamaliza kusikiliza au kutoa hukumu za mashauri husika, basi ni vyema akaendelea na kazi yake hadi akamilishe majukumu aliyopangiwa.

Kutokana na ufafanuzi huo,Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 186 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.25IBARA YA 175: Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani. Kamati kumi na moja zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati moja imependekeza Ibara hii iunganishwe na Ibara ya 164 ya Rasimu ya Tume.

Kamati ya Uandishi, baada ya kuyatafakari mapendekezo ya Kamati zote imekubaliana na pendekezo la Kamati la kuchukua maudhui ya Ibara ya 164 yanayohusu utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu kwenye Ibara ya 175 ili utaratibu huo pia utumike kwa Majaji wa Mahakama ya Rufani.

Hivyo, Kamati ya Uandishi, inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 187 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.26 Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati nyingi za Bunge Maalum zilipendekeza kuanzishwa kwa Ibara mpya zinazoweka masharti kuhusu Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rasimu ya Tume haikutaja uwepo wa Mahakama Kuu kwenye muundo wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano kwa kuwa, Muundo wa Serikali Tatu uliopendekezwa na Tume ilitegemewa kwamba Mahakama Kuu zingeanzishwa na Nchi Washirika. Kutokana na Kamati za Bunge Maalum kupendekeza muundo wa Serikali mbili kuendelea kutumika, Kamati ya Uandishi imekubaliana na

mapendekezo hayo na imeongeza Ibara mpya za 175A, 175B, 175C, 175D, 175E, 175F, na 175G. Ufafanuzi kuhusu Ibara hizo ni kama ifuatavyo:

12.27 IBARA MPYA YA 175A: Kuhusu Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mbalimbali za Bunge zimependekeza kuongezwa kwa Ibara mpya inayoanzisha Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano, kama ilivyopendekezwa katika Ibara ya 153 inayohusu Muundo wa Mahakama.

Baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati na mijadala ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi, imeona kuna umuhimu wa kuanzisha Ibara mpya inayohusu Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na Mamlaka yake kama ilivyo katika muundo wa sasa wa Mahakama za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Rasimu ya Tume inahusu Mambo ya Muungano na Mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu Tanzania Bara. Hivyo, Kamati ya Uandishi imeongeza ibara mpya ya 175A na isomeke kama Ibara ya 188 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.28IBARA MPYA YA 175B: Majaji wa Mahakama Kuu na Uteuzi wao

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mbalimbali za Bunge zimependekeza kuongezwa kwa ibara mpya inayohusu Majaji

wa Mahakama Kuu na uteuzi wao, akiwemo Jaji Kiongozi ambaye ndiye atakayekuwa Msaidizi Mkuu wa Jaji Mkuu katika utendaji wa kazi katika Mahakama Kuu na Mahakama nyingine za ngazi ya chini yake.

Baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati na mijadala ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi, imeona kuna umuhimu wa kuanzisha Ibara mpya ya 175B ili kuainisha utaratibu wa kikatiba wa kuwapata Majaji wa Mahakama Kuu akiwemo Jaji Kiongozi kama inavyosomeka katika Ibara ya 189 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.29IBARA MPYA YA 175C: Muda wa Majaji wa Mahakama Kuu kushika madaraka

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mbalimbali za Bunge zimependekeza kuongezwa kwa Ibara mpya inayohusu muda wa Majaji wa Mahakama Kuu kushika madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuna umuhimu wa kuongeza Ibara mpya itakayoainisha masharti kuhusu muda wa majaji wa Kuu kushika madaraka ambao ni umri wa miaka sitini na tano, masharti ya Jaji kuweza kustaafu kwa hiari pindi

anapotimiza umri wa miaka sitini, isipokuwa kama Rais ataagiza kwamba asistaafu katika kipindi chochote kabla ya kufikisha umri wa miaka sitini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii mpya pia inaweka masharti ya Rais kuweza kuruhusu Jaji kuendelea kufanya kazi baada ya kufikisha umri wa miaka sitini na tano iwapo Jaji husika anakubali mwenyewe kwa maandishi kuendelea kufanya kazi. Vile vile, kwa mujibu wa Ibara hii inayopendekezwa, Jaji yoyote wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano anaweza kuendelea kufanya kazi ya Ujaji baada ya kutimiza umri wa kustaafu mpaka amalize kutayarisha na kutoa hukumu au shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri aliyokwisha anza kuyasikiliza.

Kwa msingi wa hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara mpya ya 175C kama inavyosomeka katika Ibara mpya ya 190 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ya Katiba Inayopendekezwa.

12.30 IBARA MPYA YA 175D: Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama Kuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mbalimbali za Bunge zimependekeza kuongezwa kwa Ibara mpya inayohusu utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama Kuu na masharti yahusuyo kuondolewa katika madaraka kwa

Jaji wa Mahakama Kuu kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na maradhi au tabia mbaya inayoathiri maadili ya uongozi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuna umuhimu wa kuongeza Ibara mpya ya 175D itakayoainisha masharti kuhusu utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama Kuu, kwa lengo la kuhakikisha kwamba majaji wanaondolewa madarakani kwa utaratibu ulioainishwa kikatiba badala ya kuondolewa bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara mpya hiyo isomeke kama Ibara ya 191 ya Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa.

12.31 IBARA MPYA YA 175E: Kiapo cha Majaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mbalimbali za Bunge zimependekeza kuongezwa kwa ibara mpya inayohusu kiapo cha Majaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano mara baada ya kuteuliwa.

Baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuna umuhimu wa kuongeza Ibara mpya ya 175E itakayoainisha masharti kuhusu utaratibu wa kiapo cha majaji ili kuhakikisha kwamba, Majaji wa Mahakama Kuu wanatekeleza

majukumu yao ya usimamiaji na utoaji haki kwa uaminifu na uadilifu.

Hivyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara mpya itakayosomeka kama Ibara ya 192 ya Rasimu ya Tume Inayopendekezwa.

12.32IBARA MPYA YA 175F: Mahakama Kuu ya Zanzibar

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mbalimbali za Bunge zimependekeza kuongezwa kwa Ibara mpya ya 175F itakayoainisha masharti yatakayotamka bayana kuwa, masharti ya Katiba hii hayazuii kuendelea kuwepo au kuanzishwa kwa mujibu wa sheria zinazotumika Zanzibar, kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuna umuhimu wa kuongeza Ibara mpya inayoainisha masharti kuhusu kuanzishwa kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama zilizopo chini yake, kwa mujibu wa sheria zinazotumika Zanzibar.

Hivyo, Kamati ya Uandishi imeandika Ibara mpya ya 175F kwa lengo la kuitambua Mahakama Kuu ya Zanzibar na Mahakama zilizo chini yake, kama chombo katika Jamhuri ya Muungano kitakachoshughulikia mashauri ya madai na jinai kuhusu Mambo yasiyo ya Muungano kwa upande wa

Zanzibar. Aidha, Mahakama hiyo itaanzishwa kwa mujibu wa Katiba na sheria zinazotumika Zanzibar. Hivyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara mpya hiyo ya 175F isomeke kama Ibara ya 193 ya Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa.

12.33IBARA MPYA YA 175G: Mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mbalimbali za Bunge Maalum zimependekeza kuongezwa kwa Ibara mpya ya itakayotambua mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeongeza Ibara mpya ya 175G inayoainisha masharti ya kutambua mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar. Lengo la kuongeza Ibara hii ni kuweka sharti kuwa mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar itaainishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar isipokuwa kwa mamlaka ambazo zitakuwa zimetajwa kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa. Pia, kutoa ufafanuzi kwamba endapo Bunge litatunga sheria inayotumika katika pande zote mbili za Muungano na kukabidhi madaraka kwa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano, basi Mahakama Kuu ya Zanzibar yaweza kutekeleza madaraka hayo kwa kiasi kilekile inavyoweza kuteleza Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa misingi hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara mpya kama inavyosomeka katika Ibara ya 194 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.34IBARA YA 176: Msajili Mkuu wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu nafasi ya Msajili Mkuu wa Mahakama. Kamati nne zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza. Kamati moja imependekeza kuifuta Ibara hii kwa msingi kwamba nafasi hii si lazima iwe ni ya kikatiba na inafaa iwekwe katika Sheria itakayotungwa na Bunge. Aidha, Kamati saba zimependekeza kurekebisha Ibara hii kwa kufuta kwenye ibara ndogo ya (2)(b) maneno "**za Nchi Washirika**" na badala yake kuweka moja wapo ya maneno "**Jamhuri ya Muungano**", au **"upande wowote wa Jamhuri ya Muungano**", au "**ya Tanzania Bara au Zanzibar**" au **"ya Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar"** au "**Mahakama za Tanzania au Mahakama za Zanzibar"** au **"Mahakama Kuu ya Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapitia mapendekezo ya Kamati zote kumi na mbili, Kamati ya Uandishi, imekubaliana na mapendekezo ya kufuta maneno **"Nchi Washirika"** na badala yake kuweka maneno **"Jamhuri ya Muungano au Mahakama za Zanzibar"** kwa msingi kwamba mapendekezo

hayo yanazingatia muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa na Wajumbe walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, inaona ni muhimu nafasi ya Msajili wa Mahakama Kuu ikawekwa kikatiba kwa sababu Msajili ndiye anayesimamia na kuratibu utekelezaji na utendaji wa shughuli za kimahakama kama mhimili unaojitegemea.

Hivyo, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 195 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.35IBARA YA 177: Majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama. Kamati kumi na moja zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, Kamati moja imependekeza Ibara ifutwe kwa kuwa majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama yanaweza kutungiwa sheria na Bunge badala ya kuyaweka katika Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati zote za Bunge, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza na hivyo Kamati inapendekeza kuwa Ibara hii isomeke kama

inavyoonekana katika Ibara ya 196 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.36IBARA YA 178: Mtendaji Mkuu wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mtendaji Mkuu wa Mahakama. Kamati saba zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu na Tume. Kamati tano zimetoa mapendekezo ya marekebisho kwa kufuta maneno **"na kuidhinishwa na Bunge"** kwenye ibara ndogo ya (1), kufuta ibara ndogo ya (1) na kuiandika upya kwa kuondoa sharti la Mtendaji Mkuu wa Mahakama atakayeteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge, kufuta maneno ya pembeni **"Mtendaji Mkuu"** na badala yake kuandika maneno **"Mkuu wa Utawala"** kwenye maelezo ya pembeni na popote yanapojitokeza kwenye Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge pamoja na mijadala ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi, kwa kuzingatia uhuru wa Mahakama na watendaji wake, inaona kuwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama asithibitishwe na Bunge baada ya kuteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kubadili jina la Mtendaji Mkuu wa Mahakama, kuwa Mkuu wa Utawala, halijazingatiwa na Kamati ya Uandishi kwa sababu haliendani na majukumu

ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama kama yalivyoainishwa kwenye Rasimu ya Tume. Hivyo, Kamati inapendekeza nafasi hiyo ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume.

Kwa msingi wa hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke kama ilivyoandikwa katika Ibara ya 197 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.37IBARA YA 179: Majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama. Kamati kumi na moja zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati moja imetoa mapendekezo ya kuboresha maelezo ya pembeni na kuyaandika upya ili yasomeke "**Majukumu ya Mkuu wa Utawala wa Mahakama".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari pendekezo hili, na kwa kuzingatia mfumo wa sasa wa uendeshaji wa shughuli za Mahakama nchini, Kamati ya Uandishi haijazingatia pendekezo la kufuta maneno "**Mtendaji Mkuu wa Mahakama"** na badala yake kuweka maneno "**Mkuu wa Utawala wa Mahakama"**. Kwa utaratibu wa sasa wa Mahakama, Mtendaji Mkuu wa *Mahakama (**Chief Court Administrator**)* ndiye mtendaji mkuu wa shughuli za kila siku za kiutawala za Mahakama. Hivyo ni vizuri akatambulika kwa cheo cha

"Mtendaji Mkuu wa Mahakama" na si **"Mkuu wa Utawala wa Mahakama"** kama inavyopendekezwa.

Kutokana na sababu hizi, Kamati ya Uandishi, inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 198 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.38IBARA YA 180: Tume ya Utumishi wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Tume ya Utumishi wa Mahakama. Kamati moja imependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati kumi na moja zimependekeza marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kwenye ibara ndogo ya (1), kwa kuifuta aya yote ya (c), na pia kufuta neno **"Tanganyika"** linalojitokeza kwenye aya ya (e) na (g) na kuweka badala yake maneno **"Tanzania Bara"**;

(b) kuongeza aya mpya ya (b) inayosomeka "**Jaji Mkuu Kiongozi"**, aya mpya ya (c) inayosomeka "**Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufaa"**, aya mpya ya (e) inayosomeka "**Jaji Mkuu wa Zanzibar"**, aya mpya ya (h) inayosomeka "**Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar"**, na aya mpya ya (i) inayosomeka "**Mwakilishi wa Mahakimu wa Tanzania Bara";** na

(c) kuongeza ibara ndogo mpya ya (4) inayosomeka "**Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti ya utekelezaji wa majukumu ya Tume".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari pendekezo lililotolewa na kila Kamati ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi, imeona kuna umuhimu wa kufanya marekebisho kwa kuongeza idadi ya Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Mahakama kutoka Wajumbe wanane mpaka kumi na moja. Kwa mantiki hiyo, Kamati imeongeza aya mpya ya (c) ili kumtaja Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufaa kuwa Mjumbe katika utumishi wa Mahakama, Jaji Mkuu wa Zanzibar na Jaji Kiongozi. Lengo la maboresho haya ni kuongeza uwakilishi wa Majaji wa Mahakama ya Rufaa na Majaji wa Mahakama Kuu kwenye Tume hiyo. Vile vile, pendekezo la kumwongeza Jaji Mkuu wa Zanzibar kwenye Tume hiyo ni kutokana na ukweli kwamba shughuli za msingi za Tume hiyo zinagusa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano, hivyo ni vyema Jaji Mkuu wa Zanzibar akawa miongoni mwa Wajumbe wa Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kufanya marekebisho kwenye ibara ndogo ya (1)(g) kwa kufuta neno **"Tanganyika**" na kuweka badala yake maneno **"Tanzania Bara**" ili kuzingatia muundo wa Serikali mbili ambao unapendekezwa kwa sasa.

Kamati ya Uandishi, haikubaliani na mapendekezo ya kumjumuisha **Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**, na **Mwakilishi wa Mahakimu wa Tanzania Bara** kutokana na sababu kwamba Tume hiyo haina jukumu lolote la msingi linalohitaji uwepo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, kwa kuwa ibara ndogo ya (2) imetoa fursa kwa Tume hiyo kumwalika mtu yeyote ambaye Tume inahitaji utaalamu wake, Tume inaweza kumwalika Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wataalamu wengine kwa kadri Tume itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakimu na watumishi wengine wote wa Mahakama watawakilishwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ambaye kimsingi anasimamia masuala mbalimbali yanayowahusu. Kutokana na sababu hizi, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii kwa kuzingatia mapendekezo yote ya Kamati na sasa isomeke kama Ibara ya 199 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.39 IBARA YA 181: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati saba zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, na Kamati nne zimependekeza kufanya marekebisho kwa kuwajumuisha Majaji wa Mahakama Kuu kuwa miongoni mwa watu watakaopendekezwa na Tume na kuwa miongoni mwa watu

watakaoteuliwa na Rais kuwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti neno **"Mahakimu"** katika aya ya (b), (c) na (d) kwenye ibara ndogo ya (2), kuongeza masharti ya kuzingatia **uwakilishi wa jinsia na watu wenye ulemavu** katika utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ibara ndogo ya (3)(c) na kuongeza Majaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano ili wajumuishwe kwenye majina yanayopendekezwa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi wa nafasi za uongozi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapitia mapendekezo hayo na kwa kuzingatia Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa na Wajumbe walio wengi, Kamati ya Uandishi imeyaafiki mapendekezo kwamba masharti kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama yaongezwe kwa ajili ya kushughulikia masuala yanayohusu Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakimu pamoja na maadili na nidhamu ya Majaji. Aidha, Kamati ya Uandishi imeona suala la uzingatiaji wa maadili kwa watu wanaoweza kushika nafasi za uongozi katika Mahakama ni la muhimu, na hivyo liongezwe kwenye ibara ndogo ya (2)(b) ili kuipa mamlaka Tume kupitia na kupendekeza masharti pamoja na mambo mengine kuhusu maadili ya viongozi hawa.

Kutokana na mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 200 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.40 IBARA YA 182: Uanachama katika vyama vya siasa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uanachama katika vyama vya siasa. Kamati saba zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Kamati nne zimependekeza marekebisho ya kuongeza masharti kwamba Jaji Kiongozi, Jaji wa Mahakama Kuu, Mahakimu na Wasaidizi wa Sheria wa Majaji wasiwe wanachama katika vyama vya siasa na Kamati moja imependekeza kufutwa kwa Ibara hii na kuandikwa upya ili kuweka sharti kwa Viongozi wa Mahakama kutokufanya upendeleo wa aina yoyote wa kisiasa, kidini na kijinsia katika utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia mapendekezo ya Kamati na mijadala ndani ya Bunge na kwa kuzingatia mfumo wa Serikali unaopendekezwa, Kamati ya Uandishi inaafiki kuwa Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakimu wawe ni miongoni mwa watumishi wanaopaswa kuzingatia masharti ya kutokuwa wanachama wa chama chochote cha siasa. Hata hivyo, mapendekezo ya kuweka sharti kwa ajili ya kuzuia viongozi wa Mahakama kufanya upendeleo kutokana na sababu za kisiasa, kidini na kijinsia hayajazingatiwa kwa kuwa

masharti kuhusu misingi ya utoaji haki kwa viongozi hao yamezingatiwa katika Sura hii.

Kutokana na maoni hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 201 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

12.41 IBARA YA 183: Mfuko wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mfuko wa Mahakama, Kamati nane zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati nne zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno **"Mtendaji Mkuu wa Mahakama"** na badala yake kuandika maneno **"Jaji Kiongozi",** kufuta neno **"Kinachotosha"** na maneno **"kwa kiwango kinachojitosheleza"** katika ibara ndogo ya (3) na badala yake kuandika **"kinachoridhisha kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti"** ili kuhakikisha kuwa mfuko wa Mahakama unapatiwa fedha za kutosha kuwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake ipasavyo**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kuyapitia na kuyatafakari mapendekezo ya Kamati inatambua kuwa upo umuhimu kwa Serikali kutenga kiwango cha fedha zitakazoingizwa kwenye Mfuko wa Mahakama ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Kamati ya Uandishi inapendekeza jambo hilo lifanyike kwa kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Msingi wa pendekezo hilo ni kuiwezesha Mahakama kutengewa fedha za kutosha kwenye Bajeti ya kila mwaka kulingana na hali ya uchumi.

Kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hiyo kama inavyosomeka katika Ibara ya 202 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA KUMI NAMOJA
UTUMISHI WA UMMA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

13.0 IBARAYA 184: Misingi mikuu ya Utumishi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu misingi mikuu ya Utumishi wa Umma. Kamati moja imependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati kumi na moja zimependekeza Ibara ifanyiwe marekebisho kwa:

(a) kuongeza Ibara mpya ya 184A ambayo itachukua maudhui ya Ibara ya 22, inayohusu marufuku kwa baadhi ya vitendo kwa Watumishi wa Umma;

(b) kuifuta na kuaindika upya kwa lengo la kuboresha maudhui yake ikiwemo kuongeza maneno **"kwa wakati"** katika aya ya (d) ya ibara ndogo ya (1), kuongeza maneno **"ina mipango"** katika aya ya (e), neno **"kuwajibika"** katika aya ya (g), kuongeza maneno

"viongozi" na "**na kuchukuliwa hatua stahili**" katika aya ya (h);

(c) kuongeza maneno **"unazingatia"**, "**usawa wa kijinsia**" na "**na fursa kwa watu wenye ulemavu**" katika aya ya (j);

(d) kuifuta na kuiandika upya aya ya (f) ili kuweka mazingira bora ya kuajiriwa kwa watu wenye ulemavu; na

(e) kuongeza aya mpya ya (k) kwa lengo la kuweka misingi kwa Serikali kuzingatia nafasi mpya za ajira na ajira mbadala kwa watu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati pamoja na mijadala Bungeni, Kamati ya Uandishi imeona kuna umuhimu wa kuboresha Ibara hii ili iweze kuleta maudhui ya misingi ya utumishi wa Umma, Kamati imeongeza maneno "**Mikuu**" ili misingi inayozungumziwa kwenye ibara ndogo ya (1) iwe ni "**misingi mikuu**" kama ambavyo imeelezwa kwenye maelezo ya pembeni. Aidha, Kamati imefuta aya ya (b), (c), (e), (d), (f), (g), (h) na (i) katika Ibara ndogo ya (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo ya Kamati za Bunge kwa kuongeza maneno **"kwa wakati"** katika aya mpya ya (b) kwa nia ya kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma. Maneno mengine yaliyoongezwa ni pamoja na **"unazingatia**", **"usawa wa kijinsia" "na fursa kwa watu wenye ulemavu"** kwenye aya

mpya ya (c) kwa lengo la kuhakikisha kwamba ajira katika nafasi mbalimbali za umma zinazingatia masuala ya jinsia na fursa kwa watu wenye ulemavu.

Kuhusu pendekezo la kuongeza Ibara mpya Kamati ya Uandishi haijazingatia pendekezo hilo, kwa kuwa maudhui yake yameainishwa katika Ibara ya 22 ya Rasimu ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii kama inavyosomeka katika Ibara ya 203 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

13.1 IBARA YA 185: Ajira na Uteuzi wa Viongozi na Watumishi wa Taasisi katika Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu ajira na uteuzi wa Viongozi wa Taasisi katika Serikali. Kamati tatu zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati tisa zimetoa mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuiboresha ibara hii ikiwa ni pamoja na kutilia mkazo Taasisi au Wizara za Muungano kuzingatia ushiriki na uwiano katika pande zote mbili za Muungano. Mapendekezo hayo ni pamoja na:

(a) kuongeza neno **"uadilifu"** katika aya ya (a), ya ibara ndogo ya (1);
(b) kuongeza maneno **"Jamhuri ya Muungano"** mwishoni mwa aya ya (b);

(c) kuongeza aya mpya ya (c) itakayozingatia masuala ya jinsia, ulemavu, na uwiano wa pande mbili za Muungano wakati wa kuajiri; na

(d) kufuta ibara ndogo ya (1) na ya (2) na kuiandika upya kwa lengo la kuiboresha;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imetafakari mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na Kamati za Bunge na mijadala Bungeni, na imeona ipo haja ya kuiandika upya Ibara hii kwa madhumuni ya kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi na kimaudhui. Hivyo, Kamati imeyaboresha maelezo ya pembeni ya Ibara hii ili yasomeke **"Ajira na Uteuzi wa Viongozi na Watumishi wa Taasisi katika Serikali"** na imefuta aya za (a) na (b) na maudhui yake yamejumuishwa kwenye ibara ndogo ya (1) na ya (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imeyazingatia mapendekezo ya Kamati za Bunge kwa kuongeza neno **"uadilifu"** kama moja ya sifa zinazopaswa kuzingatiwa kwenye ajira na teuzi wa Viongozi na watumishi wa Taasisi katika Serikali.

Pia, Kamati imeiandika upya ibara ndogo ya (2) ili kuweka vigezo kwamba uteuzi wa viongozi na watumishi katika Taasisi au Wizara za Muungano uzingatie uwakilishi wa pande mbili za Muungano, jinsia na watu wenye ulemavu.

Kutokana na sababu hizo, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii na inasomeka kama ilivyo katika Ibara ya 204 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

13.2 IBARA YA 186: Tume ya Utumishi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Tume ya Utumishi wa Umma. Kamati zote kumi na mbili zimependekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali ili kuleta mtiririko mzuri wa kimaudhui kama ifuatavyo:

(a) kuiandika upya Ibara hii kwa lengo la kuboresha Ukuu wa Tume;

(b) kuongeza maneno "**kwa kuzingatia pande mbili za Muungano"** mwishoni mwa ibara ndogo ya (1) ili kuweka uwiano kwa pande mbili za Jamhuri ya Muungano katika uteuzi wa Wajumbe wa Tume;

(c) kufuta neno "**sita**" na badala yake kuweka neno "**tano**" katika ibara ndogo ya (1) pamoja na kufuta maneno **"kwa kuzingatia pande mbili za Muungano"** ili kufanya idadi ya Wajumbe wa Tume watakaoteuliwa na Rais kuwa watano;

(d) kufuta maneno **"kuidhinishwa na "Bunge"**, ili kuondoa sharti la Bunge kuidhinisha uteuzi wa Mwenyekiti wa Tume kwa kuwa nafasi hiyo ni ya kiutendaji na kwamba Mwenyekiti hawajibiki moja kwa moja kwa Bunge;

(e) kuongeza neno **"sheria"** katika ibara ndogo ya (2);

(f) kuongeza nafasi ya Makamu Mwenyekiti ambaye sifa zake za uteuzi ziwe sawa na za Mwenyekiti;

(g) kuongeza maneno "**wa kuzaliwa**" katika ibara ndogo ya (3)(a) ili kufanya sharti la uraia uwe ni wa kuzaliwa;

(h) kufuta maneno **"miaka kumi"** na badala yake kuandika **"miaka mitano"** au **"miaka mitatu au zaidi"** kwa mtu kuwa Mwenyekiti na **"miaka mitano"** kuwa miaka **"mitatu"** kwa Mjumbe wa Tume katika ibara ndogo ya (3)(c);

(i) kuongeza sifa kwamba Mwenyekiti na Mjumbe wawe ni raia wasio na uraia wa nchi nyingine; na

(j) kufuta neno **"Mjumbe"** na badala yake kuandika "**Makamu Mwenyekiti**" ili kuweka sifa zake ziwe ni sawa na zinazotumika kumpata Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia na kutafakari mapendekezo ya Kamati na mijadala Bungeni na inaona kuwa maudhui yake yanajitosheleza na kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi imeongeza nafasi ya Makamu Mwenyekiti, imefuta neno "**sita"** na kuandika **"tano"** ili kubadilisha idadi ya Wajumbe wa Tume wanaopaswa kuteuliwa na Rais katika ibara ndogo ya (1). Vilevile, Kamati imefuta maneno **"na kuidhinishwa na Bunge"** ili kuondoa sharti la uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu na Wajumbe kuidhinishwa na Bunge baada ya kuteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imefanya maboresho katika ibara ndogo ya (3), kwa kuongeza maneno **"wa kuzaliwa"** ili Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume wawe na sifa ya uraia wa kuzaliwa kabla ya kuteuliwa.

Aidha, Kamati ya Uandishi haijazingatia hoja ya kuongeza maneno "kwa mjumbe" kwa sababu maudhui yaliyopo kwenye ibara ndogo ya (3)(c) tayari yamejumuisha kipindi cha uzoefu wa miaka kumi kwa Mjumbe na kipindi cha miaka kumi na tano kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii kama inavyoonekana katika Ibara ya 205 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

13.3 IBARAYA 187: Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma. Kamati moja imependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo na Kamati kumi na moja zimependekeza marekebisho mbalimbali kwa:

(a) kufuta maneno **"au Serikali za Nchi Washirika**", au **"Serikali za Nchi Washirika baada ya kuidhinishwa na Bunge"** na badala yake kuweka **"ya Mapinduzi ya**

Zanzibar" au "**Serikali ya Jamhuri ya Muungano"** ili kuendana na Muundo wa Serikali mbili katika ibara ndogo ya (1);

(b) kuifuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (1) kwa lengo la kuweka sharti la Rais kushauriana na Rais wa Zanzibar katika uteuzi wa Katibu wa Tume;

(c) kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) inayohusu uteuzi wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma na kuzingatia pande mbili za Muungano katika uteuzi wa nafasi ya Katibu; na

(d) kuainisha sifa za Katibu wa Tume ili ziwe kama sifa za kuwapata Wajumbe wa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia na kutafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge na imeona kuna umuhimu wa kufuta maneno **"za Nchi Washirika"** ili kuendana na Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa. Aidha, Kamati imeona Katibu wa Tume asithibitishwe na Bunge kwa sababu Katibu wa Tume hiyo hawajibiki moja kwa moja kwa Bunge na kuheshimu dhana ya msingi wa mgawanyo wa madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haijazingatia pendekezo la Rais wa Jamhuri ya Muungano kushauriana na Rais wa Zanzibar wakati wa kumteua Katibu wa Tume kwa sababu Katibu anayepaswa kuteuliwa anapaswa kuwa ni mtumishi wa Umma katika Jamhuri ya Muungano.

Vile vile, Kamati ya Uandishi haijazingatia pendekezo la kuainisha masharti ya sifa za Katibu wa Tume kwa sababu sifa ya kuwa Mtumishi wa Umma zinajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeandika upya Ibara hii kama inavyoonekana katika Ibara ya 206 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

13.4 IBARAYA 188: Mamlaka na Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu mamlaka na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma. Kamati tatu zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati tisa zimetoa mapendekezo ya kuifanyia Ibara hii marekebisho kwa:

(a) kuongeza maneno **"ya Muungano na yasiyo ya Muungano"** ili kufafanua kuhusu masuala yanayopaswa kufanyiwa kazi na Tume;

(b) kufuta neno **"kuwaondoa"** kwenye ibara ndogo ya (2)(c) na badala yake kuandika maneno **"kazini na kuwachukulia hatua";**

(c) kuongeza maneno **"na kuzitolea uamuzi"** katika ibara ndogo ya (2)(e);

(d) kufuta aya (b), (f), (g) na (h) katika ibara ndogo ya (2);

(e) kuongeza neno "**wasiofaa**" katika ibara ndogo ya (2);

(f) kufuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (1);

(g) kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) inayotaka Tume ya Utumishi kusimamia Idara za Utumishi katika Wizara na Taasisi mbalimbali zilizoundwa kwa mujibu wa sheria;

(h) kuongeza ibara ndogo ya (3) inayolipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Tume;

(i) kuongeza Ibara mpya kwa ajili ya kuanzisha Bodi ya Mishahara na Maslahi ya Watumishi wa Umma; na

(j) kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) itakayoweka masharti yatakayoeleza kuwa Tume zote za Utumishi wa Umma za kisekta ambazo zimeainishwa katika Katiba hii na sheria nyingine, zitawajibika kwa Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge pamoja na maoni yaliyotolewa wakati wa mjadala na imeifuta na kuiandika upya Ibara hii kwa madhumuni ya kufanya maboresho ya kiuandishi na kimaudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ibara ndogo ya (2), Kamati imeifanyia marekebisho kwa kuipa Tume jukumu la kupendekeza kwa Rais, majina ya Viongozi kwa ajili ya uteuzi katika nafasi mbalimbali badala ya kumshauri, kuhamasisha utekelezaji wa misingi ya Umma, kushughulikia rufaa za Watumishi wa Umma pamoja na nidhamu katika utumishi wa umma na kutekeleza majukumu mengine yatakayoainishwa na sheria.

Vile vile, Kamati ya Uandishi, imezingatia pendekezo la kuongeza ibara ndogo ya (3) ili kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara ya 188 kama inavyoonekana katika Ibara ya 207 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kuongeza Ibara mpya inayohusu Tume ya Mishahara na Maslahi kwa ajlii ya kuunda na kupanga ngazi za mishahara ya Watumishi wa Umma na maslahi yao. Aidha, ibara ndogo ya (2) ya Ibara hii mpya imetoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria itakayoweka masharti kuhusu muundo, majukumu na mambo mengine kuhusu utekelezaji wa Tume ya

Mishahara na Maslahi kama inavyoonekana katika Ibara ya 208 ya Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA KUMI NA MBILI
UCHAGUZI KATIKA VYOMBO VYA UWAKILISHI NA VYAMA VYA SIASA

14.0 IBARA YA 189: Ushiriki katika Uchaguzi na Kura ya Maoni

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Ushiriki wa Wananchi katika Uchaguzi na Kura ya Maoni**.** Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu na Kamati mbili zinapendekeza maboresho kwa kufuta neno "**walemavu"** na badala yake kuandika maneno **"watu wenye ulemavu"** katika ibara ndogo ya 2(d)(iii), kufuta maneno **"wa sheria"** katika Ibara ndogo ya (3), kufuta maneno **"mpiga kura"** katika ibara ndogo ya (4) na badala yake kuandika maneno "**mgombea urais",** na kuweka "**Ibara ndogo mpya ya (5)"** kwa ajili ya kuweka masharti ya kisheria kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Wajumbe wa Kamati za Bunge na mijadala ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kiuandishi kwa kufuta neno "**walemavu"** na badala yake kuweka maneno **"watu wenye ulemavu"** kwenye ibara ndogo ya (2)(d)(iii) ili kuweza kuweka dhana ambayo imekusudiwa.

Aidha, Kamati ya Uandishi, imefuta haki ya kila mpiga kura kuweza kufungua shauri Mahakamani kupinga matokeo ya uchaguzi na kutoa fursa hiyo kwa mgombea urais pekee aliyeshiriki katika uchaguzi wa Rais.

Pia, Kamati ya Uandishi imeongeza ibara ndogo ya (3) inayotoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria kuhusu utekelezaji wa masharti ya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeona umuhimu wa kuongeza Ibara mpya inayotoa haki ya mtu kuwa mgombea huru katika uchaguzi unaosimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi. Aidha, kwenye ibara ndogo ya (2), imetoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria itakayoweka masharti kuhusu utekelezaji wa Ibara hii.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uandishi imeifanyia marekebisho Ibara hii na kuongeza Ibara Mpya ya 209 kama inavyoonekana kwenye Rasimu hii ya Katiba inayopendekezwa.

SEHEMU YA PILI
TUME HURU YA UCHAGUZI

14.1 IBARA YA 190: Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kuundwa kwa Tume huru ya Uchaguzi. Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati mbili zimetoa mapendekezo kwa ajili ya kuiboresha ibara ndogo za (5)(a) na (6)(a), ili kumwezesha Mwenyekiti na Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi awe ni raia wa kuzaliwa na kutomlazimu mmoja wa wazazi wake kuwa ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano, kufuta maneno "**Mbunge wa Tanganyika**" na "**Serikali ya Tanganyika**" na badala yake iandikwe "**Tanzania Bara**" kwenye ibara ndogo ya (7)(a), kuongeza maneno **"uwiano wa**" baada ya neno "**utazingatia**", kuongeza maneno "**na jinsi**" baada ya neno "**Muungano**" katika ibara ndogo ya (8), na kuongeza maneno **"uraia pacha**" baada ya neno "**kuzaliwa**" katika ibara ndogo ya (5)(a). Aidha, kufuta maneno **"linalohusiana na uaminifu"** katika ibara ndogo za (5)(e) na (6)(e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi, imefuta maneno **"kuthibitishwa na Bunge"** kwenye ibara ndogo ya (3) na badala yake kuweka maneno **"kuapishwa na Rais"** ili Mwenyekiti, Makamu na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi waapishwe na Rais mara baada ya kuteuliwa na wasithibitishwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeongeza maneno "**ya juu**" kwenye ibara ndogo ya (5)(d) ili kuweka sifa

ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama cha siasa kwenye ibara ndogo ya 5(d) na 6(c). Vilevile, Kamati imefuta maneno **"linalohusiana na uaminifu"** katika ibara ndogo ya (5)(e) na (6)(e) ili kuweka sharti la kuzuia mtu ambaye ametiwa hatiani kwa kosa la jinai kutokuwa na sifa ya kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe.

Aidha, Kamati ya Uandishi imeifuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (7)(a) ili kuwatambua watu ambao hawatakuwa na sifa ya kuwa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi ambao ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani.

Vilevile, Kamati ya Uandishi imeona kwamba ibara ndogo za 5(a) na (6)(a) zibaki kama zilivyo ili kuhakikisha nafasi hizi zinashikwa na raia ambao ni wazawa na wazalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dhana ya kuwepo kwa uraia pacha, Kamati ya Uandishi iliikataa hoja hii kutokana na unyeti wa nafasi hii. Hivyo, ni vyema mtu ambaye atachaguliwa aweze kuwa raia wa Tanzania na asiwe na uraia wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii iandikwe upya na isomeke

kama Ibara ya 211 kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

14.2 IBARA YA 191: Kamati ya Uteuzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kamati ya Uteuzi. Kamati zote kumi na mbili zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa ajili ya kuendana na maudhui yaliyokusudiwa. Baadhi ya mapendekezo hayo ni kufuta neno **"Tanganyika"** kila mahali linapojitokeza katika Ibara hii, kufuta aya za (d) na (e) za ibara ndogo ya (1) kwa kuwaondoa Spika wa Bunge wa Tanganyika na Jaji Mkuu wa Tanganyika kutokuwa Wajumbe wa Kamati ya Uteuzi, kubadilisha jina la Kamati hii ili iwe Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi, kumweka Jaji Mkuu wa Zanzibar kuwa Makamu Mwenyekiti, kuondoa sharti la Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kuthibitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kufanya uchambuzi wa kina kuhusu mapendekezo ya Kamati mbalimbali za Bunge imekubaliana na hoja ya kumjumuisha Jaji Mkuu wa Zanzibar kuwa Makamu Mwenyekiti kwenye ibara ndogo ya (1) na kumwongeza Jaji Kiongozi kuwa Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imefuta na kuandika upya aya za (d) na (e) kwenye ibara ndogo ya (1)

kwa ajili ya kuendeleza maudhui ya Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa.

Aidha, Kamati ya Uandishi, inapendekeza kuondoa sharti la Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kuthibitishwa na Bunge ili kuwezesha kila mhimili wa dola kufanya kazi yake kwa uhuru zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho haya Ibara hii sasa isomeke kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 212 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

14.3 IBARA YA 192: Ukomo wa kushika nafasi ya madaraka ya Tume Huru ya Uchaguzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Ukomo wa kushika nafasi ya madaraka ya Tume Huru ya Uchaguzi. Kamati kumi zilipendekeza marekebisho mbalimbali kwa kuondoa maneno "**kutoka Tanganyika**" na kuweka maneno **"kutoka Tanzania Bara"** katika ibara ndogo ya (5)(d), na kufuta ibara ndogo ya (1) na kuiandika upya kwa lengo la kuliwezesha Bunge kutunga sheria itakayoweka ukomo wa kushika madaraka katika Tume Huru ya Uchaguzi, kwa lengo la kuendana na maudhui ya Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa na kufuta na kuiandika upya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kimaudhui kwa kufuta maneno **"kutoka Tanganyika"** na kuweka maneno **"kutoka Tanzania Bara",** kwa lengo la kuweka Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa.

Aidha, Kamati imeifuta ibara ndogo ya (4) inayohusu Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kupoteza sifa ya kuwa Mjumbe endapo atakiuka Kanuni za Maadili. Kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi imeipanga upya ibara ndogo ya (5) kuwa ya (4) na ibara ndogo zinazoendelea zitafuata mtiririko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii iandikwe upya na itasomeka kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 213 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

14.4 IBARA YA 193: Wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi. Kamati kumi zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo Katika Rasimu ya Tume na Kamati mbili zinapendekeza marekebisho mbalimbali kwa kuongeza maneno **"na Serikali za Mitaa"** katika ibara ndogo ya (1)(a), kuongeza aya mpya ya **"(e)"** kwenye ibara ndogo (1) ili kuipa Tume wajibu wa kutangaza matokeo ya uchaguzi, kuongeza maneno **"kwa kuzingatia ukubwa wa eneo na wingi wa watu**

ndani yake" mwishoni mwa ibara ndogo ya (1)(d), kufuta neno **"huru"** na badala yake liwekwe neno **"binafsi"** katika Ibara ndogo ya (3)(a), na kufuta neno "**Tanganyika**" na badala yake kuweka "**Tanzania Bara"** katika ibara ndogo ya (6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada kutafakari mapendekezo haya, Kamati ya Uandishi imeona kuwa hakuna haja ya kubadilisha jina la mgombea huru ili awe mgombea binafsi kwani jina la mgombea huru ndilo ambalo linaleta tafsiri na dhana ambayo imekusudiwa.

Aidha, Kamati ya Uandishi imefuta maneno **"na Tume Huru ya Tanganyika"** kwenye ibara ndogo ya (6) ili kuendana na dhana ya muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi haijazingatia pendekezo la kuongeza maneno **"Serikali za Mitaa"** katika ibara ndogo ya (1)(a) na (e) ili kuwezesha Tume Huru kushughulikia uchaguzi wa Rais na Wabunge na kuacha uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la kuongeza maneno "**kwa kuzingatia ukubwa wa eneo na wingi wa watu ndani yake**" Kamati ya Uandishi haikulizingatia kwa kuwa

ugawaji wa majimbo ni jukumu la Tume Huru ya Uchaguzi hivyo hakuna ulazima wa kulitaja, bali Tume yenyewe itaweka vigezo vya kugawa majimbo.

Aidha, Kamati ya Uandishi imeongeza aya mpya ya (e) kwenye ibara ndogo ya (1) ili kuwezesha Tume Huru ya Uchaguzi kutangaza matokeo ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge au matokeo ya kura ya maoni, jukumu ambalo halikuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii na isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 214 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

14.5 IBARA YA 194: Malalamiko kuhusu Uchaguzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Malalamiko kuhusu Uchaguzi. Kamati sita zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba na Kamati sita zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kuipa mamlaka Mahakama ya Wilaya na Hakimu Mkazi kuweza kusimamia malalamiko ya uchaguzi yanayotokana na Serikali za Mitaa na malalamiko ya uchaguzi ya Wabunge yaweze kufunguliwa katika Mahakama Kuu.

Aidha, imependekezwa kufuta Ibara hii yote na kuiandika upya ili kufafanua masuala yanayohusu malalamiko ya uchaguzi ili yaweze kuainishwa katika sheria itakayotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuwa, kwa kuwa uchaguzi wa Madiwani hautasimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi, inapendekezwa malalamiko kuhusu uchaguzi wa Madiwani yafunguliwe katika Mahakama za Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii na itasomeka kama ilivyo kwenye Ibara ya 215 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

14.6 IBARA 195: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi. Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati mbili zinapendekeza Ibara hii irekebishwe kwa kufuta maneno "**na angalau mmoja wa wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano**" katika ibara ndogo (2)(a), kufuta kigezo cha kuthibitishwa na Bunge katika ibara ndogo ya (1)(c)

na kufuta maneno "linalohusu kukosa uaminifu" katika ibara ndogo ya (2)(e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyachambua mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuwa pendekezo la kuondoa sifa ya "angalau mmoja wa wazazi awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano" na inapendekeza kuwa sifa hiyo iendelee kuainishwa katika Ibara hii.

Aidha, pendekezo la Mkurugenzi wa Uchaguzi kutothibitishwa na Bunge limezingatiwa ili kutoa fursa kwa kila mhimili kuweza kufanya kazi bila ya kuingiliwa na mhimili mwingine.

Vile vile, pendekezo la kufuta maneno **"linalohusu kukosa uaminifu"** nalo limezingatiwa ili kuwezesha watu wanaogombea nafasi hii wasiwe ni watu ambao hawajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai. Kamati pia imeainisha sifa ya Mkurugenzi kuwa ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama cha siasa ili kuzuia mgongano wa maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii iandikwe upya na isomeke kama ilivyo kwenye Ibara ya 216 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

14.7 IBARA YA 196: Majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi. Kamati nane zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba na Kamati nne zinapendekeza kufanya marekebisho kwa kuongeza ibara ndogo mpya itakayoliwezesha Bunge kutunga sheria ili kuweka utaratibu wa Uchaguzi, uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa kura ya maoni, kufuta ibara ndogo ya (4) ili maudhui yake yaweze kutungiwa sheria na kurekebisha ibara ndogo ya (3) ili kuwezesha Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi kusaidiana na watendaji watakaoteuliwa kwa mujibu wa sifa zitakazoainishwa katika Sheria. Aidha, kurekebisha ibara ndogo ya (1) kwa lengo la kuwezesha Tume Huru ya Uchaguzi kuboresha Daftari la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imeona kuwa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge hayana sababu ya kuongezwa kwa kuwa maudhui ya Ibara hii yanajitosheleza. Hata hivyo, imefanya maboresho ya kiuandishi ili kuleta mtiririko mzuri wa lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke

kama ilivyo kwenye Ibara ya 217 ya Rasimu hii ya Katiba inayopendekezwa.

14.8 IBARA YA 197: Usajili wa vyama vya siasa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Usajili wa Vyama vya Siasa. Kamati tano zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati saba zimetoa mapendekezo mbalimbali kwa kuongeza aya mpya ya (f) katika ibara ndogo ya (2), kuifanyia marekebisho ibara ndogo ya (2)(d) kwa kuondoa maneno **"sehemu moja tu ya"** na badala yake kuweka maneno **"upande mmoja tu wa"** na kufanya maboresho mbalimbali ya kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho ya kiuandishi na kimaudhui ili Ibara hii iweze kueleweka kwa urahisi zaidi. Kamati ya Uandishi imefuta neno **"pahala**" na badala yake imeweka neno **"mahali"** kwenye ibara ndogo ya (2)(a)(ii) na imefanya maboresho ya kimaudhui kwenye aya ya (e) ya ibara ndogo ya (2) kwa kuweka sharti la kuzuia chama cha siasa ambacho kimesajiliwa kiweze kuruhusu uchaguzi wa uongozi wake kuzingatia jinsia, watu wenye ulemavu na uwakilishi wa pande zote mbili za Muungano kwa njia ya demokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi wa mapendekezo hayo, Ibara hii sasa itasomeka kama inavyoonekana katika Ibara ya 218 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

14.9 IBARA YA 198: Uteuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uteuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa. Kamati sita zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati nyingine sita zinapendekeza kufanya marekebisho kwa:

(a) kufuta maneno **"na kuthibitishwa na Bunge"** ili Msajili wa vyama asithibitishwe na Bunge katika ibara ndogo ya (1);

(b) kuongeza aya ya (2)(c) itakayotamka kuwa Msajili wa vyama awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka yoyote katika chama cha siasa kuanzia ngazi ya Kata au zaidi;

(c) kuongeza maneno **"na Naibu Msajili"** baada ya neno **"Msajili"** katika ibara ndogo ya (1);

(d) kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) itakayomtaka Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa awe Msaidizi Mkuu wa Msajili wa Vyama Vya Siasa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali za Bunge, Kamati ya Uandishi imeifanyia marekebisho ibara ndogo ya (1) kwa kuongeza maneno **"miongoni mwa orodha ya watu watatu"** ili

kumpa mamlaka Rais kumteua Msajili wa Vyama vya Siasa miongoni mwa orodha ya watu watatu watakaopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma. Aidha, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo ya kumtaka Msajili wa Vyama asithibitishwe na Bunge ili kuweza kuwa na fursa ya kila mhimili kuweza kufanya kazi yake bila ya kuingiliwa.

Aidha, kwenye ibara ndogo ya (2), Kamati imeiboresha aya ya (c) kwa kuongeza maneno **"ya juu"** ili kuweka sifa ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama cha siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeongeza Ibara mpya inayomtambua Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma kutoka orodha ya miongoni mwa watu watatu wataopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma. Aidha, Ibara hii imetoa sifa za mtu anayefaa kuteuliwa kuwa Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa na majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hizo kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 219 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

14.10 IBARA YA 199: Wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa. Kamati saba zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati tano zinapendekeza kuifanyia marekebisho Ibara hii kwa kuongeza maneno "**kinachopata ruzuku kutoka Serikalini kama ilivyo kwenye sheria za nchi"** katika ibara ndogo ya (1)(b), aidha kulikuwa na pendekezo la kumpa Msajili mamlaka ya kufuta chama chochote cha siasa na kuongeza maneno **"matumizi ya"** katika ibara ndogo ya (1)(c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inashauri maneno **"kinachopata ruzuku kutoka Serikalini kama ilivyo kwenye Sheria za nchi"** yasiongezwe katika Ibara hii kwa sababu jukumu la Msajili la kukagua ripoti za ukaguzi wa fedha linavihusu vyama vyote vya siasa. Hivyo, Kamati inapendekeza ibara ndogo ya (1)(b) ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu hii ya Katiba inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kutafakari mapendekezo ya Kamati na majadiliano Bungeni inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 219 ya Katiba hii na majukumu yake ni kama yalivyoainishwa katika Ibara 221 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati mbalimbali, Kamati ya Uandishi,

imeongeza Ibara mpya inayomtaja Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na majukumu yake. Ibara zinazomzungumzia Naibu Msajili huyo ni Ibara ya 220 na majukumu yake ni kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 221 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA KUMI NA TATU
TAASISI ZA UWAJIBIKAJI

15.0 IBARAYA 200: Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji**.** Kamati tatu zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, na Kamati tisa zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kufuta maneno **"Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji"** popote yanapojitokeza na badala yake kuweka maneno "**Tume ya Maadili ya Taifa";**

(b) kurekebisha ibara ndogo ya (4) kwa kufuta maneno "**kuthibitishwa na Bunge**" na badala yake kuweka maneno **"baada ya kuapishwa na Rais";**

(c) kurekebisha ibara ndogo ya 5(a) kwa kuongeza maneno **"na pia wazazi wake wote wawili wawe ni Raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano**";

(d) kuongeza ibara ndogo mpya ya (7) ambayo itatambua uwepo wa Katibu wa Tume ambaye ndiye atakayeongoza Sekretarieti ya Tume;

(e) kufuta neno "**itakuwa**" katika ibara ndogo ya (1) na badala yake kuweka neno "**itakayokuwa**";

(f) kurekebisha ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "**baada ya kupendekezwa na Kamati Maalum ya Uteuzi**" na badala yake kuweka maneno "**miongoni mwa majina yatakayopendekezwa na Tume ya Uteuzi**";

(g) kurekebisha ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "**baada ya kupendekezwa na Kamati Maalum ya Uteuzi**" na badala yake kuweka maneno "**baada ya kupendekezwa na Kamati Maalum ya Mapendekezo ya Uteuzi**";

(h) kuongeza sifa za Mwenyekiti katika ibara ndogo ya (5)(e) ili awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai, kukosa uaminifu na kukiuka maadili ya uongozi; na

(i) kufuta maneno "**linahusu kukosa uaminifu**" katika ibara ndogo ya (5)(e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia na kuyatafakari mapendekezo ya Kamati zote kumi na mbili, inapendekeza Tume hii ijulikane kama "**Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**". Lengo ni kulifanya jina la Tume lifanane na majukumu ambayo Tume imepewa kwa mujibu wa Katiba

hii. Hivyo, Kamati ya Uandishi imezifanyia marekebisho Ibara zote zinazotaja jina la Tume hii, ili kuweka maudhui yaliyokusudiwa.

Aidha, Kamati ya Uandishi imeifuta ibara ndogo ya (3) ili kuandika Ibara mpya inayojitegemea kwa ajili ya kuweka masharti ya uteuzi wa viongozi mbalimbali wakiwamo wa Tume ya Maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imeafiki mapendekezo ya kuboresha sifa za Mwenyekiti wa Tume kuwa raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano ambaye angalau mmoja wa wazazi wake awe ni raia wa Jamhuri ya Muungano. Lengo la maboresho hayo ni kuzidi kuthibitisha uraia wa mtu anayepaswa kuteuliwa bila ya kuacha chembe yoyote ya shaka. Kamati pia imefuta sharti la Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume kuthibitishwa na Bunge kwa lengo la kuzingatia uhuru wa Tume na misingi ya mgawanyo wa madaraka. Vilevile, Kamati ya Uandishi imeifuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (5)(e) ili kuweka sharti la kumzuia mtu ambaye amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai asiweze kuwa Mwenyekiti wa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo Kamati ya Uandishi, imeiandika upya Ibara hii kama

inavyosomeka kwenye Ibara ya 222 Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.1 IBARAYA 201: Uteuzi na sifa za Wajumbe

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uteuzi na Sifa za Wajumbe. Kamati tano zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, na Kamati saba zinapendekeza marekebisho kama ifuatavyo:

(a) kubadilisha Jina la **"Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji"** na kuwa **"Tume ya Maadili ya Taifa"**;

(b) kurekebisha ibara ndogo ya (2) ili kuwezesha Wajumbe wa Tume wawe raia wa Tanzania na wazazi wao wote pia wawe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;

(c) kurekebisha ibara ndogo ya (1) kwa kuitaka Kamati Maalum ya Uteuzi izingatie uwiano wa pande mbili za Muungano, jinsia na uwakilishi wa watu wenye ulemavu;

(d) kurekebisha ibara ndogo ya (2)(c) kwa kufuta neno "**Kumi**" na badala yake kuweka maneno "**Kumi na Tano**";

(e) kuongeza ibara mpya ya (1)(e) kwa ajili ya kuongeza sifa inayomtaka Mjumbe wa Tume awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai;

(f) kurekebisha ibara ndogo ya (2)(d) kwa kumtaka Mjumbe awe ni mtu mweledi, mwadilifu na asiwe na tabia zenye kutiliwa shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, baada ya kuyatafakari mapendekezo ya Kamati zote kumi na mbili imeona kuwa pendekezo hili la kuzingatia uwiano wa pande mbili za Muungano, ulemavu na jinsia wakati wa uteuzi wa Wajumbe ni la msingi na kwa kuwa maneno haya yanajirudia rudia hivyo ni bora maudhui yake yakawekwa katika Ibara moja. Aidha, Kamati inaona kuwa kigezo cha mzazi mmoja kuwa raia kinatosha kuthibitisha uraia wa mtu.

Hata hivyo, Kamati imekubaliana na pendekezo la kuweka sharti la kumzuia mtu asiteuliwe kuwa Mjumbe wa Tume endapo mtu huyo ametiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai. Sharti hili ni la msingi kwa kuwa linawianisha masharti ya Ibara hii na Ibara ya 222, na litasaidia kupata kiongozi ambaye ni mfano wa kuigwa katika jamii. Vilevile, Kamati ya Uandishi ina maoni kwamba kipindi cha miaka kumi kinatosha kwa mtu kuweza kuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Mjumbe, na kwa hiyo hakuna haja ya kufanya marekebisho katika ibara ndogo ya (2)(c) kukiongeza kipindi hicho kuwa ni miaka kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizo, Ibara hii imeandikwa upya kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 223 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.2 IBARAYA 202: Kamati Maalum ya Uteuzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kamati Maalum ya Uteuzi. Kamati zote kumi na mbili zilikuwa na marekebisho kama ifuatavyo:

(a) kufuta aya ya (c) na (e);
(b) kufuta maneno **"Kamati Maalum ya Uteuzi**" na badala yake kuweka maneno **"Kamati ya Uteuzi**";
(c) kuongeza Wajumbe wapya katika Kamati Maalum ya Uteuzi ambao ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Jaji Mkuu wa Zanzibar, na Jaji Kiongozi; na
(d) kufuta neno **"Tanganyika**" na badala yake kuweka maneno **"Tanzania Bara**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo haya, imefuta aya ya (b), (c), (e) na (f) na badala yake kumuweka, **Jaji Mkuu wa Zanzibar, Jaji Kiongozi** na **Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar** kuwa Wajumbe ili kuleta taswira ya uwakilishi wa vyombo muhimu vya Serikali kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano katika Kamati ya Uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii na itasomeka kama Ibara ya 224 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.3 IBARAYA 203: Majukumu ya jumla ya Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu majukumu ya jumla ya Tume. Kamati moja inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati kumi na moja zinapendekeza ifanyiwe marekebisho kwa kufuta na kuandika upya Ibara hii kwa kutowajumuisha watumishi wa umma kwenye masharti ya Ibara hii, kuzifuta aya ndogo za (b), (e), (f), (h), (i),(k), (l), (m), (n) na (o) kwenye ibara ndogo ya (1), kuongeza aya mpya ya (p) inayoipa majukumu Tume kufuatilia na kuchunguza tabia na mwenendo wa viongozi na watumishi wa umma na aya mpya ya (q) kwa ajili ya kuipa jukumu Tume kupokea Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa viongozi wa umma, kuongeza ibara ndogo ya (3) itakayoweka masharti yatakayotoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria kuhusiana na majukumu ya Tume na utekelezaji wa majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati zote na imeona umuhimu wa kuifuta na kuaindika upya ibara ndogo ya (2) na kuainisha upya majukumu ya Tume kwa kuwa aya zilipendekezwa kufutwa zinahusu uwezo na utaratibu wa Tume katika kutekeleza

majukumu yake hivyo ni vyema mambo hayo ya yakaainishwa katika sheria itakayotungwa na Bunge.

Aidha, Kamati ya Uandishi, imeifanyia marekebisho aya ya (c) ambayo kwa sasa ni aya ya (b) na itasomeka "**kuchunguza tabia na mwenendo wa kiongozi wa umma na kuchukua hatua pale inapostahili'.** Vilevile, Kamati imeongeza ibara ndogo ya (3) inayotoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hiyo kama Ibara ya 225 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.4 IBARAYA 204: Muda wa kukaa madarakani kwa Mjumbe wa Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu muda wa kukaa madarakani kwa mjumbe wa Tume. Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, Kamati moja inapendekeza Ibara hii ifutwe na Kamati moja inapendekeza ifanyiwe marekebisho katika Ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno **"au vinginevyo vyovyote itakavyokuwa**".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati zote na mijadala ndani ya Bunge na

imeona kuwa maudhui ya Ibara hii yaunganishwe na Ibara ya 205 ya Rasimu ya Tume na Ibara inayohusu kuondolewa madarakani kwa Mjumbe wa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke Ibara ya 226 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.5 IBARAYA 205: Kuondolewa madarakani kwa Mjumbe wa Tume:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kuondolewa madarakani kwa Mjumbe wa Tume. Kamati kumi na moja zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati moja inapendekeza iongezwe aya mpya ya (f) katika Ibara ndogo ya (1). Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza sababu za kuondoshwa madarakani kwa Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume iwapo atatiwa hatiani kwa makosa ya jinai yanayohusiana na kukosa maadili na uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo ya Kamati zote na imeunganisha maudhui ya Ibara hii kwenye Ibara ya 205 ambayo Kamati inapendekeza isomeke kama Ibara 226 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.6 IBARAYA 206: Uhuru wa Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uhuru wa Tume. Kamati kumi na moja zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati moja inapendekeza marekebisho kwa kuongeza aya mpya itakayoweka masharti kuhusu muda ambao Wajumbe watakaa madarakani na utaratibu wa kuwaondoa Wajumbe hao madarakani.

Hata hivyo, baada ya kutafakari pendekezo hilo, Kamati ya Uandishi imeona kuwa aya hiyo isiongezwe kwa kuwa maudhui yake yamezingatiwa katika aya ya (e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, na isomeke kama Ibara ya 227 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.7 IBARAYA 207: Uwezeshaji wa nyenzo na rasilimali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uwezeshaji wa nyenzo na rasilimali. Kamati nane zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, Kamati moja inapendekeza ifutwe na Kamati tatu zinapendekeza ifanyiwe marekebisho kwa kufuta jina la **"Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji"** na badala yake liwekwe "**Tume ya Maadili ya Taifa"** na katika ibara ndogo ya (1) kufuta maneno **"ya kutosha".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati zote na imebadillisha jina la "**Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji**" kuwa "**Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**" kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa ili kuhakikisha kwamba Serikali inaipatia Tume fedha, nyenzo na rasilimali watu ili kutekeleza kazi na wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 228 kama Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SEHEMU YA PILI
TUME YA HAKI ZA BINADAMU

15.8 IBARAYA 208: Tume ya Haki za Binadamu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Tume ya Haki za Binadamu. Kamati moja inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati kumi na moja zilikuwa na mapendekezo mbalimbali ya kurekebisha Ibara hii kama ifuatavyo:

(a) kuongeza maneno **"na Utawala Bora"** baada ya maneno **"Tume ya Haki za Binadamu"** kwenye ibara ndogo ya (1) na popote yanapojitokeza kwenye Ibara na Sehemu ya Pili ya Sura hii;

(b) kuyafuta na kuyaandika upya maelezo ya pembeni na jina la Sehemu hii kwa muktadha huu, ili kuipa Tume mamlaka ya kushughulikia masuala ya haki za binadamu na Utawala Bora;

(c) kuongeza maneno **"kwa kuzingatia uwiano wa pande mbili za Muungano, jinsia na uwakilishi wa watu wenye Ulemavu"** baada ya maneno **"Kamati ya Uteuzi**" kwenye ibara ndogo ya (2);

(d) kufuta maneno "**kuthibitishwa na Bunge"** na badala yake kuweka maneno **"kuapishwa na Rais"** ili kuifanya Tume na watendaji wake kuwa huru na kutowajibika kwa Bunge.

(e) kuongeza Ibara mpya na kuweka maelezo yake pembeni ili yasomeke **"Sifa za Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume"** ili iendane na utaratibu wa uandishi uliotumika kwenye Tume zingine kwa kuweka Ibara inayojitegemea;

(f) kuongeza maneno "**asiye na uraia wa nchi nyingine na angalau mmoja wa wazazi wake ni raia wa Tanzania"** kwenye aya ya (a) ya Ibara ndogo ya (5) ili kuweka sharti la Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kuwa ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania;

(g) kuongeza maneno "**au shahada nyingine yoyote ya Uchumi, Siasa, Sayansi ya Jamii au Utawala"**; kwenye aya ya (a) ya ibara ndogo ya (5) ili kuweka muktadha

utakaoweka sifa za Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Tume kuwa ni mwenye Shahada ya Sheria;

(h) kufuta neno **"Uweledi"** na badala yake kuweka neno **"weledi";**

(i) kuongeza maneno **"wa kuzaliwa"** baada ya neno "**raia**" kwenye aya ya (a) ya ibara ndogo ya (6) ili kuweka sifa ya uraia wa kuzaliwa kwa Makamishna wa Tume;

(j) kuongeza maneno **"moja kati ya**" baina ya neno "**sifa**" na kufuta neno "**na**" lililopo kati ya neno "**siasa**" na "**mambo**" kwenye aya ya (c) ya ibara ndogo ya (6), ili kuongeza wigo wa watu wa kada mbalimbali kuomba nafasi hizo;

(k) kufuta neno "**uweledi**" katika aya ya (d) ya ibara ndogo ya (6) na badala yake kuweka neno "**weledi**";

(l) kuzipanga upya aya za ibara ndogo ya (6) ili aya ya (e) iwe ni (b) na (b) iwe (e) na kuzipanga upya aya zote zilizopo katika Ibara hii, ili kuweka muktadha utakaotanguliza sifa za kitaaluma kabla ya sifa nyingine zilizoorodheshwa kwenye ibara ndogo ya (6); na

(m) kufuta aya za (a) hadi (e) za ibara ndogo ya (6) na badala yake kufanya rejea ya sifa zilizoainishwa kwenye ibara ndogo ya (5) ili sifa za Makamishna wa Tume ziwe ni sawa na sifa za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati mbalimbali za Bunge na mijadala ndani ya Bunge,

Kamati ya Uandishi imeunga mkono hoja ya kuongeza maneno **"na Utawala Bora"** baada ya maneno **"Tume ya Haki za Binadamu"** kwenye jina la Sehemu ya Pili ya Sura ya Kumi na Tatu na maelezo ya pembeni ya Ibara ya 208 ya Rasimu ya Tume na popote yanapojitokeza kwenye Ibara zote za Sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya mapendekezo haya ni kuipa mamlaka Tume ishughulikie masuala yote ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kama yalivyoainishwa kwenye Rasimu ya Tume. Aidha, pendekezo la kuweka sharti la kuzingatia uwiano wa pande mbili za Muungano, jinsia na uwakilishi wa watu wenye ulemavu halijazingatiwa kwa sababu imewekwa kwenye Ibara mahsusi inayozungumzia masuala ya uteuzi wa viongozi. Kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi imeifuta ibara ndogo ya (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho hayo ibara ndogo ya (4) sasa isomeke kuwa ni ya (3) na ibara ndogo zinazoendelea zitafuata mpangilio huo.

Kamati ya Uandishi pia imekubaliana na pendekezo la Kamati za Bunge la kufuta sharti la Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, kuthibitishwa na Bunge na badala yake watashika madaraka baada ya kuapishwa na Rais, ili kuifanya Tume na Watendaji wake, kuwa ni chombo huru na kisichowajibika kwa Bunge,

kwa mujibu wa Misingi ya Paris inayoanzisha vyombo hivi duniani.

Aidha, Kamati ya Uandishi, imekubaliana na pendekezo la kuifanya ibara ndogo ya (5) kuwa ni Ibara mpya itakayoainisha sifa za Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume, ili iendane na utaratibu wa kiuandishi uliotumika kwenye Ibara nyingine za Rasimu zinazoanzisha Tume mbalimbali, ambazo zimeainisha Ibara tofauti zinazozungumzia sifa za wajumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imekubaliana na pendekezo la Kamati za Bunge la kuweka sharti la Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume kuwa ni raia wa kuzaliwa na angalau mmoja kati ya wazazi wao kuwa ni raia wa Tanzania, ili kuhakikisha kwamba nafasi hizi za juu za chombo huru cha Serikali zinashikwa na watu ambao ni raia, bila ya kuacha chembe yoyote ya shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati Uandishi haijazingatia pendekezo la kuongeza sifa ya Shahada nyingine yoyote ya Uchumi, Siasa, Sayansi ya Jamii au Utawala kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na badala yake imeacha sifa ya Shahada ya Sheria peke yake. Hii ni kwa sababu asili ya shughuli za Tume ni za kisheria na zinahitaji Kiongozi au Viongozi wenye elimu na uzoefu wa sheria ili waweze kuzisimamia

kikamilifu kazi za Tume. Aidha, wasaidizi wao wa karibu ambao ni Makamishna watakuwa na sifa tofauti zinazohusisha kada mbalimbali ikiwemo sheria, siasa, haki za binadamu na mambo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, inakubaliana na pendekezo la Kamati za Bunge la kuifanyia marekebisho aya ya (d) ya ibara ndogo mpya za (1) na (2) ili kuweka muktadha wa kuweka sifa mbadala zitakazohitajika kwa mtu anayefaa kushika nafasi hizo.

Aidha, Kamati ya Uandishi imeona kuwa aya ya (a) mpaka (e) za ibara ndogo ya (6) zisifutwe kwa ajili ya kuweka utofauti wa sifa zinazohitajika kwa kiongozi wa Tume na Makamishna wanaofanya kazi chini yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi wa hoja hizo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii igawanywe ili ziwe Ibara mbili zinazojitegemea. Ibara ya 229 itowe ufufanuzi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Ibara ya 229 iweke masharti ya sifa za Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Tume. Ibara hizo ni kama zinavyosomeka kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.9 IBARAYA 209: Kamati ya Uteuzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Kamati ya Uteuzi. Kamati zote kumi na mbili zilikuwa na mapendekezo ya maboresho kama ifuatavyo:

(a) kufuta maneno **"Kamati ya Uteuzi"** yanayojitokeza kwenye maelezo ya pembeni na badala yake kuweka maneno "**Kamati ya Mapendekezo ya Uteuzi"** na popote yanapojitokeza kwenye Ibara hii, ili kuhakikisha kwamba jina la Kamati hii linafanana na majukumu yake ambayo kimsingi ni kupendekeza majina ya uteuzi kwa mamlaka husika na si kuteua;

(b) kufuta na kuandika upya ibara ndogo ya (d) na (e) za ibara ndogo ya (1) ili ziweze kuwajumuisha **Wawakilishi watatu kutoka katika Taasisi za kidini na mwakilishi mmoja kutoka asasi za kiraia;**

(c) kufuta neno **"Tanganyika"** kwenye aya za (d) na (e) na badala yake kuweka maneno **"Jamhuri ya Muungano"** kwa muktadha utakaomtaja Spika wa Bunge na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kuwa ni Wajumbe;

(d) kufuta aya (d) na (e);

(e) kufuta ibara ndogo ya (1) ili kuweka muktadha utakaomtaja **Jaji Kiongozi** kuwa ni mmojawapo wa Wajumbe kwenye aya ya (d);

(f) kufuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (1) na aya zake ili kuwaondoa Spika wa pande mbili za

Muungano kwa madhumuni ya kuweka Wajumbe ambao watakuwa huru na mambo ya siasa, na kuongeza wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kwa kuzingatia jinsia;

(g) kufuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (1) na aya za (a)(b) na (g) kwa nia ya kuwaondoa Jaji Mkuu wa Tanzania, Spika wa Jamhuri ya Muungano pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji na badala yake kuwaweka Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye ni Mkuu wa Utumishi wa Umma;

(h) kufuta aya ya (d) inayomtaja Spika wa Bunge la Tanganyika na aya ya (f) inayomtaja Jaji Mkuu wa Zanzibar, na badala yake kuweka aya ya (d) inayomtaja Jaji Kiongozi; (e) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na kuipa namba mpya aya ya (g) kuwa (h);

(i) kuongeza aya mpya ya (h) itakayomtaja **"Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali**" ambaye atakuwa ni Katibu;

(j) kufuta aya ya (d) na (e) na badala yake kuweka aya mpya ya (e) inayomtaja Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, aya ya (g) mwakilishi wa asasi za kiraia kama Wajumbe;

(k) kufuta neno **"Tanganyika"** na badala yake kuweka neno **"Tanzania"** ili kuzingatia mfumo wa Serikali mbili unaopendekezwa;

(l) kuongeza aya mpya ya (h) inayosomeka:

"(h) Wastaafu wawili mwanaume na mwanamke ambao wametumika Serikalini, wenye sifa ya uadilifu na weledi watakaoteuliwa na Rais, ili kuwaongeza katika orodha ya Wajumbe wa Kamati;

(m) kufuta sharti la Rais kuwasilisha majina ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa uhuru zaidi katika ibara ndogo ya (5);

(n) kufuta ibara ndogo ya (6) na kuiandika upya ili kutoa fursa kwa mtu yeyote kuomba nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Ukamishna wa Tume, badala ya asasi za kiraia tu zilizopendekezwa;

(o) kuongeza neno "Mtendaji" ili Katibu wa Tume awe ni Katibu Mtendaji na atakayeteuliwa kutokana na orodha ya majina matatu yatayopendekezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora baada ya kushauriana na Rais;

(p) Katibu wa Tume apatikane kwa ushindani ili aweze kuwajibika ipasavyo;

(q) kufuta na kuandika upya ibara ndogo ya (8) ili kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria itakayoweka masharti kuhusu majukumu ya Tume na utaratibu wa uombaji nafasi za Tume na mapendekezo ya uteuzi;

(r) kufuta ibara ndogo za (2), (3), (4) na (6) na kuandika upya namba za ibara ndogo za (5), (7) na (8) kuwa ibara ndogo za (3), (4) na (5); na

(s) kuipanga upya ibara ndogo ya (5) kuwa ya (6), na ya (6) kuwa ya (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge na mijadala ndani ya Bunge lakini haijabadilisha jina kwa sababu jina la Kamati halibadilishi majukumu ya msingi ya Kamati ambayo ni kupendekeza majina. Aidha, inapendekezwa kwamba Kamati ya Uteuzi iundwe na Jaji Mkuu wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano ambaye ni Mwenyekiti, Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye ni Makamu Mwenyekiti badala ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kama inavyopendezwa kwenye Rasimu ya Tume, Wajumbe wengine ni Spika wa pande zote mbili za Muungano. Muundo huu unazingatia uwakilishi wa pande zote mbili za Muungano, mihimili ya Bunge na Mahakama kwa pande zote, ikiwemo mhimili wa Serikali unaotumikiwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano

ambaye ni Katibu na anatekeleza majukumu ya Kamati na kuishauri wakati wote wa mchakato. Utaratibu huu ni mzuri na unazingatia misingi ya Kimataifa ya uteuzi wa Tume za aina hii inayozianzisha au kutoa miongozo ya uanzishwaji wa Tume hizi ambazo zinapaswa kuwa ni vyombo huru kiutendaji (Idara huru za Serikali) kwa namna zinavyoundwa au kuanzishwa.

Vilevile, ni maoni ya Kamati kwamba mapendekezo ya kuweka Wajumbe ambao wanatoka kwenye mhimili wa Serikali kama vile Katibu Mkuu Kiongozi au Mwenyekiti wa Tume ya Maadili yanaenda kinyume na Misingi ya Paris, kwa sababu Tume kama chombo huru cha Serikali haipaswi kuundwa na Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo ya Kamati mbalimbali ya kufuta aya za (d) na (e) kwa sababu haziendani na Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa ambao hauna Spika wa Bunge la Tanganyika wala Jaji Mkuu wa Tanganyika kama ulivyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza ibara ndogo ya (2) irekebishwe ili kumuondoa Katibu wa Tume ya Haki za Binadamu kuwa Katibu wa Kamati na badala yake imeongeza aya ya (e) ambayo imemjumuisha Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuwa ni Katibu. Sababu

ya marekebisho haya ni kuendeleza utaratibu unaotumika sasa ambao unaonekana kuwa na ufanisi badala ya Katibu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora anayetajwa kwenye ibara ndogo ya (2) ya Ibara ya 209. Utaratibu huu unazuia mgongano wa kimaslahi, baina ya Katibu Mtendaji wa Tume na Tume inayotarajiwa kuundwa ikiwemo kuzuia shutuma za upendeleo na uonevu. Hivyo ni vyema Katibu Mtendaji wa Tume akawa nje ya Kamati inayomuundia Tume atakayofanya kazi nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi imepanga upya mtiriko wa namba wa ibara ndogo ya (3) kuwa ya (2) na ibara ndogo zinazoendelea zitafuata mpangilio huo. Aidha, Kamati imefuta ibara ndogo ya (4), (5), (6) na (8) za Ibara hii ili yazingatiwe kwenye sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho kwenye ibara ndogo ya (7) ambayo kwa sasa ni ya (3) kwa kuipa mamlaka Tume ya Haki za Binadamu kupendekeza kwa Rais majina matatu ya Katibu Mtendaji badala ya nafasi hiyo kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Hii ni kwa sababu Tume inapaswa kuwa ni chombo huru kiutendaji. Hivyo ili kuzuia mgongano na Tume ya Utumishi wa Umma kuimarisha suala la uwajibikaji wa Katibu Mtendaji wa Tume kwa Tume na kwa

kuzingatia kwamba, nafasi hiyo ni ya Idara huru ya Serikali, ni vyema Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ikapewa mamlaka ya kupendekeza majina hayo. Aidha, inakubaliana na pendekezo la kutaka Katibu wa Tume awe ni Katibu Mtendaji kwa sababu nafasi hiyo inahusika na utekelezaji na utendaji wa shughuli za Tume za kila siku.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inakubaliana na pendekezo la kuiacha ibara ndogo ya (3) ya Rasimu ya Tume ambayo baada ya marekebisho imekuwa ni ibara ndogo ya (2) ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu kwa sababu shughuli za Kamati ya Uteuzi zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria za nchi, kanuni za taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi wa mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 231 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.10 IBARAYA 210: Kazi na Majukumu ya Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu, kazi na majukumu ya Tume. Kamati nne zimependeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume, Kamati moja inapendekeza Ibara hii ifutwe na Kamati saba zimetoa mapendekezo mbalimbali ya kurekebisha Ibara hii kama ifuatavyo:

(a) kufuta maneno **"Katiba za Nchi Washirika"** baada ya maneno **"kwa mujibu wa Katiba hii"** na badala yake kuweka maneno **"Katiba ya Zanzibar"** kwenye aya ya (l) ili kuzingatia Muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa na wajumbe walio wengi;

(b) kuongeza ibara ndogo ya (3) ambayo itaipa Bunge mamlaka ya kutunga Sheria kwa mujibu wa masharti ya Sura hii kuhusu mamlaka ya Tume, utaratibu na uendeshaji wa shughuli za kisheria za Makamishna na Watumishi wa Tume;

(c) kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) itayoweka masharti ya kuizuia Tume kuchunguza masuala yoyote yanashughulikiwa na Mahakama, masuala yanayohusu uhusiano na mashirikiano kati ya Serikali, Serikali yoyote ya nchi ya nje, au Shirika la Kimataifa, jambo lolote linalohusu Madaraka ya Rais, kutoa msamaha na jambo lingine lolote linalotungwa na sheria yoyote;

(d) kufuta ibara ndogo ya (1)(a) hadi aya ya (m);

(e) kuweka masharti ya kuizuia Tume kumtaka mtu kuwasilisha kwake hati au kumbukumbu ambazo kuwasilishwa kwake kunaweza kuathiri usalama wa Taifa, mwishoni mwa Ibara ya 210.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge na imefanya maboresho mbalimbali kwenye Ibara hii kwa kuongeza jukumu la Tume la kutoa mapendekezo yatakayowezesha kurekebisha kasoro mbalimbali baada ya kufanya uchunguzi wa uvunjaji wa haki za binadamu kwenye aya ya (c) ya ibara ndogo ya (1), imefuta aya za (i), (j), (k),(l) na (m) ili majukumu hayo yaainishwe kwenye sheria za nchi badala ya kujumuishwa kwenye Katiba.

Aidha, Kamati imefuta ibara ndogo ya (2) iliyopo kwenye Rasimu ya Katiba ili masharti yake yazingatiwe kwenye sheria za nchi na badala yake kuongeza ibara ndogo mpya ya (2) itakayoipa mamlaka Bunge kutunga sheria kwa ajili ya utekelezaji wa mamlaka yake, utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zake na kinga za kisheria watakazokuwa nazo Makamishna na watumishi wa Tume ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao bila ya kukiuka sheria;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza iongezwe ibara ndogo mpya ya (3)(a), (b), (c) na (d) inayozungumzia ukomo wa Tume katika kutekeleza majukumu yake. Lengo la kuongeza ibara ndogo hiyo ni kuainisha maeneo ambayo Tume haitayachunguza ili kuondoa mgongano baina ya Tume na vyombo vingine vya kimaamuzi

kama vile Mahakama, vyombo vya kiutawala na ushirikiano wa kimataifa.

Aidha, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya kuundwa kwa Tume Maalum kwa ajili ya kuhamasisha, kulinda na kufuatilia utekelezaji wa usawa wa jinsia na ulinganifu kwa ujumla katika maendeleo ya taifa. Kamati imeona kuwa upo umuhimu wa uwepo wa jukumu hilo na hivyo inashauri Tume hii ipewe jukumu hilo badala ya kuunda Tume nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 232 kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.11 IBARAYA 211: Muda wa Kukaa Madarakani kwa Kamishna wa Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu muda wa kukaa madarakani kwa Kamishna wa Tume. Kamati nane zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati moja inapendekeza Ibara hii ifutwe.

Aidha, Kamati tatu zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kufuta neno **"tu"** baada ya neno **"kimoja"** na **"cha"** katika ibara ndogo ya (2), ambalo

lilikuwa linaonyesha msisitizo wa kipindi cha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna kukaa madarakani, kufuta maneno **"au vinginevyo vyovyote itakavyokuwa**" kwenye ibara ndogo ya (2) ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza katika kutafsiri kipindi cha muda kinachotajwa na kufanyia marekebisho kwenye ibara ndogo ya (3) kwa kuifuta na kuiandika upya ili kuweka muktadha utakaozuia mgongano wa kimaslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi imekubaliana na mapendekezo ya kuiboresha ibara ndogo (3) ili kuweka masharti yatakayozuia mgongano ya kimaslahi, kwa mtu yeyote atakayeteuliwa kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Kamishna wa Tume, kuacha madaraka katika chama cha siasa au madaraka ya aina nyingine yoyote yatakayotajwa na sheria baada ya kuteuliwa kuwa Kamishna wa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 233 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.12 IBARAYA 212: Kuondolewa madarakani kwa Kamishna wa Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kuondolewa madarakani kwa Kamishna wa Tume. Kamati nne baada ya majadiliano ya kina zilikubaliana kwamba Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume kwa msingi kwamba maudhui yake yanajitosheleza. Kamati moja inapendekeza Ibara hii ifutwe kwa sababu maudhui yake yanatakiwa kuwekwa katika sheria zitakazotungwa na Bunge. Aidha, Kamati saba zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa:

(a) kufuta maneno **"Tume ya Utumishi wa Umma"** popote yanapojitokeza katika Ibara hii na badala yake kuweka maneno **"Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji";**

(b) kufuta ibara ndogo (5);

(c) kuongeza maneno **"kwa sababu za kiafya"** katika ibara ndogo ya (1)(d) na kuongeza aya mpya ya (f) inayoweka sharti la mtu kutokuteuliwa endapo amewahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai yanayohusiana na kukosa maadili au kukosa uaminifu kwa madhumuni ya kuiboresha;

(d) kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya kwa lengo la kuweka utaratibu wa kikatiba wa kumuondoa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Tume;

(e) kuongeza maneno**"atakavyoona inafaa",** kufuta maneno "**atakavyoshauriana**" na badala yake iandikwe **"baada ya kushauriana";**

(f) kuandika upya maneno ya pembeni ili yasomeke **"Kuondolewa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Tume;**

(g) kufuta aya ya (a) na ya (b) za ibara ndogo ya (2) na kufuta ibara ndogo ya (3) na (4);

(h) Kufuta maneno **"Kamati Maalum"** na badala yake kuweka maneno **"Tume ya Haki za Binadamu na utawala Bora";** na

(i) kuongeza aya mpya ya (f) inayomzuia Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna kutojihusisha na siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapitia mapendekezo ya Kamati zote Kamati ya Uandishi inapendekeza yaandikwe maelezo ya pembeni ya Ibara hii ili yasomeke; **"Kuondolewa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Tume"** kwa lengo la kuyafanya maelezo haya yaakisi maudhui ya Ibara hii kwa sababu yanawahusu pia Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. Aidha, Kamati inapendekeza iongezwe aya mpya ya (f) kwa ajili ya masharti ya kumuondoa madarakani Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Tume endapo atatiwa hatiani kwa makosa ya jinai yanayohusu kukosa maadili au uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti Kamati ya Uandishi, inapendekeza ibara ndogo ya (2) inayosomeka "Tume ya Utumishi wa Umma" ibadilishwe na badala yake iandikwe "Kamati Maalum"

itakayoundwa na Rais kwa madhumuni ya kutoa mapendekezo ya kumuondoa madarakani Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu inapotokea kuna malalamiko yanayohusu mwenendo au tabia isiyoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke Ibara ya 234 ya Rasimu ya Katiba hii Inayopendekezwa.

15.13 IBARAYA 213: Uhuru wa Tume

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uhuru wa Tume. Baada ya majadiliano ya kina, Kamati saba zinapendekeza kwamba Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume kwa msingi kwamba, maudhui yake kama yalivyokusudiwa yanajitosheleza. Aidha, Kamati tano zinapendekeza marekebisho mbalimbali kwa;

(a) kufuta na kuandika upya ibara ndogo ya (2) kwa ajili ya kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria itakayoweka masharti na utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Tume;

(b) kufuta neno **"haitaingiliwa"** na badala yake kuweka neno **"haitoingiliwa";**

(c) kufuta na kuiandika upya Ibara hii ili kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria kuhusu utekelezaji na majukumu ya Tume, uwasilishaji wa taarifa za Tume;
(d) kuifuta ibara ndogo ya (2) kwa msingi kwamba maudhui yake yamezingatiwa; na
(e) kuifuta Ibara hii na kuiandika upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati pamoja na mijadala ndani ya Bunge na imeona maudhui yaliyomo katika Ibara hii yanajitosheleza. Aidha, mapendekezo ya kuifuta na kuiandika upya Ibara hii ili kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume pamoja na masuala mengine, tayari yameshazingatiwa kwenye ibara ndogo ya (2) ya Rasimu ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na isomeke Ibara ya 235 ya Rasimu hii ya Katiba inayopendekezwa.

15.14 IBARAYA 214: Uwezeshaji wa nyenzo na rasilimali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu, uwezeshaji wa nyenzo na rasilimali. Kamati tisa zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume. Kamati tatu zinapendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kwa kufuta maneno **"ya**

kutosha kadri hali itakavyoruhusu" baada ya maneno **"rasilimali watu".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo imekubaliana na mapendekezo ya kufuta maneno **"ya kutosha kadri hali itakavyoruhusu"** na kuiandika upya Ibara hii ili kuipa Serikali jukumu la kuweka utaratibu utakaoiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kupatiwa fedha, nyenzo na rasilimali watu kulingana na uwezo wa kibajeti wa Serikali ili kulinda uhuru wake katika kutekeleza kazi na majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke Ibara ya 236 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SEHEMU YA TATU
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

15.15 IBARAYA 215: Uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati nane zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume wakati Kamati nne zinapendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kufuta maneno **"na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano;"** yaliyopo katika ibara ndogo ya (1) ili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali asithibitishwe na Bunge;

(b) kufuta ibara ndogo ya (2) na masharti yake yazingatiwe katika sheria ili kuleta ufanisi na tija katika kudhibiti na kukagua hesabu za serikali;

(c) kuifuta Ibara hii na kuiandika upya kwa kutenganisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kupata vyombo viwili ambavyo ni **"Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali"** na **"Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na Matumizi ya Serikali";** Sababu za mapendekezo haya ni kuleta ufanisi na tija katika kudhibiti na kukagua hesabu na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo ya Kamati pamoja na mijadala ndani ya Bunge Maalum, Kamati ya Uandishi ina maoni kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali asithibitishwe na Bunge

kama ilivyopendekezwa na Rasimu ya Tume, ili kuondoa muingiliano wa majukumu kati ya mhimili wa Bunge na Serikali.

Aidha, Kamati inaona kwamba kazi na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haipaswi kutenganishwa kwa kuwa mtu anayedhibiti anapaswa kukikagua kile anachokidhibiti. Hivyo, ni vyema majukumu haya yakawa chini ya mtu mmoja.

Aidha, Kamati inapendekeza kuwa iongezwe ibara ndogo mpya ya (2) ili kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuteuliwa kutoka orodha ya majina kama itakavyokuwa imependekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma. Kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi imezipanga upya ibara ndogo za Ibara hii na ili kusomeka Ibara ndogo ya (2) iwe ibara ndogo ya (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 237 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.16 IBARAYA 216: Sifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu sifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati saba

zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati tano zinapendekeza marekebisho mbalimbali ya kimaudhui kama ifuatavyo:-

(a) kuifuta aya ya (a) ya ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya;

(b) kufuta maneno **"katika orodha ya majina matatu ya"** katika ibara ndogo ya (1);

(c) kuongeza maneno "**wa kuzaliwa"** baada ya neno **"raia"** katika ibara ndogo ya (2) ili kuweka sifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa raia wa kuzaliwa wa Tanzania;

(d) kufuta maneno **"linalohusu kukosa uaminifu"** katika aya ya (d) ya ibara ndogo ya (1) ili kuweka sifa ya mtu kutoteuliwa kushika nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali endapo atakuwa na hatia ya kosa la jinai; na

(e) kufuta neno **"heshima"** katika aya ya (e) ya ibara ndogo ya (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara ndogo ya (1) ifutwe kwa kuwa maudhui yake yamezingatiwa kwenye Ibara ya 236 za Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia pendekezo la kufuta neno **"linalohusu kukosa uaminifu"** kwa sababu kosa lolote la jinai linatosha kumthibitisha mtu kukosa uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 238 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.17 IBARAYA 217: Kazi na Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kazi na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati sita zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo na Kamati nyingine sita zilipendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kama ifutavyo:

(a) kuongeza aya ndogo ya (v) katika aya (c) kwenye ibara ndogo ya (1) inayompa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua hesabu za Serikali za Mitaa na Vyama vya Siasa au hesabu za Serikali za Mitaa tu;

(b) kufuta maneno "**linaweza** kutunga" na badala yake kuweka maneno "**litatunga**";

(c) kufuta maneno **"atatosheka"** na badala yake kuweka maneno "**ataridhika**"; na

(d) kufuta na kuandika upya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho ya kiuandishi kwa kufuta na kuongeza maneno ili kuleta mtiririko wa lugha unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika ibara ndogo ya (1)(c) (i), Kamati imeongeza maneno **"hesabu za vyama vya siasa na hesabu za Serikali za Mitaa"** baada neno **"Muungano"** ili kumpa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kudhibiti na kukagua hesabu za Serikali za Mitaa na Vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maboresho hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 239 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.18 IBARA YA 218: Muda wa kukaa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Muda wa kukaa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati tisa zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati tatu zilipendekeza kuifanyia Ibara hii marekebisho mbalimbali kwa: kufuta na kuandika upya Ibara hii; kuondoa maneno **"kimoja cha miaka saba mfululizo"** na badala yake kuweka maneno **"cha miaka mitano na kuweza kuteuliwa tena kwa mara nyingine**

ambayo itakuwa ya mwisho" ili kuweka sharti la muda wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukaa madarakani; na ibara ndogo ya (1) ifutwe na kuandikwa upya ili kuweka sharti la umri wa miaka sitini au umri wowote mwingine utakaotajwa na Bunge kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kukaa madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati na mijadala Bungeni, Kamati ya Uandishi imeona sharti la kutaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuacha kazi yake atakapotimiza umri wa miaka sitini au umri wowote mwingine utakaotajwa na Sheria, kwa kuwa, anateuliwa kutoka orodha ya watumishi wa Umma ambao kwa mujibu wa sheria hustaafu wanapofika umri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii na isomeke Ibara ya 240 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.19 IBARAYA 219: Kuondolewa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabuza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kuondolewa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati tatu zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume. Hata hivyo, Kamati moja

ilipendekeza Ibara hii ifutwe na Kamati nane zilipendekeza marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kufuta maneno **"Mahakama ya Juu";**

(b) kufuta maneno **"Nchi Washirika"** katika ibara ndogo ya (3)(a);

(c) kufuta maneno **"Nchi Washirika"** na badala kuweka **"Jamhuri ya Muungano"** au **"Mahakama Kuu ya Zanzibar"** katika ibara ndogo ya (3)(a);

(d) kuongeza aya mpya ya (f) inayomtia hatiani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa makosa ya jinai yanayohusiana na kukosa maadili na uaminifu;

(e) kufuta na kuandika upya ibara ndogo ya (3)(a);

(f) kuongeza maneno **"kwa sababu za kiafya"** katika ibara ndogo ya (1)(d); na

(g) kufuta maneno **"ya Juu"** na badala yake liwekwe neno **"Kuu"**.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari na kuyazingatia mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imekubaliana na hoja ya kuongeza aya ya (f) katika ibara ndogo ya (1) inayohusu kumuwekea sharti Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa anaweza kuondolewa madarakani endapo atatiwa hatiani kwa makosa ya jinai.

Aidha, Kamati ya Uandishi imefuta maneno **"Nchi Washirika"** ili kuendana na muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara ndogo ya (3)(a) ifutwe na kuandikwa upya. Marekebisho hayo yanalenga kuweka utaratibu kwa Rais kuteua Kamati maalum itakayokuwa na Wajumbe wasiopungua watatu, mmoja kutoka Mamlaka ya Uhasibu nchini, na wawili ambao mmoja atakuwa ni Jaji au ni mtu aliyepata kuwa Jaji. Lengo la kumuongeza mjumbe kutoka Mamlaka ya Uhasibu ni kwa sababu nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendana na fani ya Uhasibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, inapendekeza kuwa sababu ya kiafya inayopendekezwa isiwe miongoni mwa vigezo vya kumwondoa madarakani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii na isomeke kama Ibara ya 241 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

15.20 IBARAYA 220: Uwezeshaji wa nyenzo na rasilimali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uwezeshaji wa

nyenzo na rasilimali. Kamati tisa zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume na Kamati tatu zinapendekeza kufanyia marekebisho mbalimbali katika ibara hii kwa; kufuta maneno "**itahakikisha kuwa"** na badala yake kuweka maneno "**itaweka utaratibu utakaowezesha"** na kufuta maneno "**ya kutosha"** na badala yake kuweka maneno "**kulingana na uwezo wa kibajeti wa serikali".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge na mijadala ndani ya Bunge na inapendekeza Ibara hii iandikwe upya ili kuiwezesha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwezeshwa kwa kupatiwa nyenzo na rasilimali kulingana na uwezo wa kibajeti wa Serikali ili kulinda uhuru wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 242 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA KUMI NA NNE

16.0 MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura hii inahusu masharti kuhusu fedha za Jamhuri ya Muungano. Kamati tisa zinapendekeza kuongeza Ibara mpya kwenye Sura hii kutokana na ukweli kwamba eneo hili limekuwa likilalamikiwa na wananchi kwa muda mrefu na hivyo

kusababisha moja ya kero za Muungano. Hivyo basi, lengo la mapendekezo hayo ni kuweka utaratibu wa kushughulikia migogoro kuhusu:

(a) fedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(b) misingi ya matumizi ya fedha za umma; na

(c) sharti la kuwasilisha taarifa za Akaunti ya Pamoja Bungeni.

16.1 IBARA MPYA

220A: Misingi ya Matumizi ya Fedha za Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii mpya inahusu misingi ya matumizi ya fedha za Umma. Lengo la Ibara hii ni kuainisha misingi itakayoongoza matumizi ya fedha za Umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuongezwa Ibara hii mpya isomeke Ibara ya 243 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.2 IBARA MPYA:

220B: Akaunti ya Fedha ya Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii mpya inaanzisha Akaunti Maalum itakayoitwa "Akaunti ya Fedha ya Pamoja" ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina, ambamo fedha zote zitakazopatikana kwa njia mbalimbali pamoja na fedha

zote zitakazochangwa na Serikali zote mbili kwa kiasi kitachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha, kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge kwa madhumuni ya shughuli za Muungano kwa Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeona umuhimu wa kuongeza Ibara hii kama inavyopendekezwa kwa sababu uanzishwaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja itasaidia kutatua changamoto za mapato na uchangiaji wa gharama za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeongeza Ibara hii mpya na isomeke Ibara ya 244 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.3 IBARA MPYA:

220C: Tume ya Fedha ya Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inaanzisha Tume ya Fedha ya Pamoja, yenye Wajumbe wasiozidi saba watakaoteuliwa na Rais kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Tume ya Fedha ya Pamoja ni kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali za pande zote mbili kuhusu

mchango na mgao wa kila Serikali mojawapo, kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano pamoja na kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeongeza Ibara mpya na itasomeka kama Ibara ya 245 kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.4 IBARA YA 221: Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mfuko Mkuu wa Hazina, Kamati kumi na moja hazikuwa na mapendekezo ya marekebisho yoyote hivyo zinapendekeza kuwa, Mfuko Mkuu wa Hazina uendelee kuwepo kama ilivyopendekezwa kwenye Rasimu ya Tume. Hata hivyo, Kamati moja ilipendekeza kufuta maneno "**ambamo fedha zitakazopatikana kwa njia mbalimbali zitawekwa"** baada ya maneno **"Mfuko Mkuu wa Hazina"** na badala yake kuweka maneno "**ambao utachangiwa na pande zote mbili za Muungano kwa utaratibu utakaopendekezwa na Tume ya Pamoja ya Fedha ili kukidhi Muundo wa Serikali mbili".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyazingatia mapendekezo ya Kamati na ina maoni kuwa pendekezo la

kuongeza sharti la Mfuko Mkuu wa Hazina kuchangiwa na pande zote mbili za Muungano linapelekea Mfuko huu kujumuisha kwa pamoja michango inayohusiana na Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume, ili kutenganisha michango inayotokana na Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa njia ya kuwepo au kuanzishwa kwa Akaunti ya pamoja. Hii pia itafanikisha kuweka utaratibu mzuri wa uchangiaji na ugawaji wa fedha za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii itasomeka kama Ibara ya 246 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.5 IBARA YA 222: Masharti ya kutoa fedha za matumizi katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu masharti ya kutoa fedha za matumizi katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Katiba na Kamati mbili zinapendekeza maboresho machache kwa kuondoa neno **"ama"** baada ya neno **"yameidhinishwa**" katika ibara ndogo ya (1)(b) na kuondoa neno **"au"** kabla ya

neno **"Hazina"** na kuweka maneno "**ya kiuandishi**" katika Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyazingatia mapendekezo hayo na imefanya marekebisho ya kiuandishi ambayo yameboresha maudhui ya Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 247 kama ilivyo kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.6 IBARA YA 223: Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kuidhinisha Matumizi ya fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina, Kamati kumi zinapendekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba. Hata hivyo, Kamati mbili zinapendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kuondoa neno "**wahusika"** na kuweka maneno **"Waziri wa Jamhuri ya Muungano"** katika ibara ndogo ya (1); na

(b) kurekebisha maneno ya kufunga *[closing words]* ya ibara ndogo ya (3) kwa kuweka dhana ya kuondoa utaratibu wa uwasilishwaji wa Makadirio na Matumizi ya nyongeza

ambayo yakikubalika na Bunge ndipo Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha unajadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imefuta neno "**wahusika**" na badala yake imeweka maneno **"watu wanaohusika kwamba watengeneze"** kwenye ibara ndogo (1) ili kuweka matumizi ya lugha fasaha.

Aidha, Kamati ya Uandishi, imeongeza ibara ndogo mpya ya (2) na ya (3) zinazotoa mamlaka kwa Kamati ya Bunge kuyafanyia tathmini na uchambuzi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yanayowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, katika kufanya hivyo, Kamati ya Bunge inaweza kukaribisha na kupokea maoni na ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu Makadirio hayo na kuandaa Taarifa kuhusu Makadirio ya Serikali na kisha kuiwasilisha Bungeni.

Kufuatia marekebisho hayo, Kamati ya Uandishi imepanga upya mtiririko wa ibara ndogo ambapo ibara ndogo ya (2) itasomeka kuwa ibara ndogo ya (4) na zinazoendelea zitafuata mpangilio huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya ibara hii na itasomeka kama Ibara ya 248 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.7 IBARA YA 224: Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha kabla ya Sheria ya Matumizi ya fedha za Serikali kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha za Serikali kabla ya kuanza kutumika. Kamati zote zinapendekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imefanya maboresho madogo ya kiuandshi kwa kuongeza neno "**au**" kabla ya neno "**hadi**" ili kuweka mazingira ambayo fedha ambazo zimeidhinishwa na Rais kutumika kabla ya Sheria ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka huo haijaanza kutumika, fedha hizo zilizoidhinishwa zinatakiwa ziweze kutumika ndani ya miezi minne au hadi sheria ya matumizi ya fedha itakapoanza kutumika kutegemea ni lipi kati ya mambo hayo litatokea mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii itasomeka kama 249 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.8 IBARA YA 225 Mfuko wa Matumizi ya dharura

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Mfuko wa matumizi ya dharura. Kamati Kumi na moja zinapendekeza ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Katiba. Kamati moja inapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno **"**za nchi**"** na badala yake kuweka maneno "itakayotungwa na Bunge".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuzingatia mapendekezo ya Kamati zote imeona kuwa maudhui ya Ibara hii kama ilivyotolewa na Tume yamejitosheleza.

Kwa kuzingatia ufafanuzi huu Kamati ya Uandishi imeiandika kama Ibara ya 250 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.9 IBARA YA 226: Mishahara ya baadhi ya watumishi kudhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tano zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba. Kamati saba zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kuongeza maneno **"malipo ya uzeeni na kiinua mgongo"** katika ibara ndogo ya(1);

(b) kuongeza maneno **"kwa wale wanaostahili malipo hayo miongoni mwa watumishi hao"** baada ya maneno **"kiinua mgongo"** katika ibara ndogo ya (2);

(c) kuandikwa upya ibara ndogo ya (5) ili sharti kuhusu mishahara ya watumishi waliotajwa katika ibara ndogo ya (5) lisiainishwe katika Katiba bali liainishwe katika Sheria itakayotungwa na Bunge;

(d) kuongezwa maneno **"Gavana** na **Naibu Gavana" wa Benki Kuu ya Tanzania"** baada ya maneno **"Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali"** katika ibara ndogo ya (5);

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo ya Kamati zote na imefanya marekebisho ya kimaudhui kwenye ibara ndogo ya (1) na (2) kwa kufafanua kwamba kutakuwa na watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano watakaolipwa mishahara, posho, malipo ya uzeeni na kiinua mgongo kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kama itakavyoelezwa na sheria. Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa matumizi ya fedha za umma kwa ajili ya malipo hayo, kwa baadhi ya watumishi wa Serikali na kuwapa uhakika wa mapato na matunzo yao baada ya kustaafu au kuacha kazi, lakini pia kuepusha watumishi hao kujilipa mishahara na mafao nje ya utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeifanyia marekebisho ibara ndogo ya (5) kwa kupunguza baadhi ya watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambao hawatahusika na masharti ya Ibara hii. Watumishi waliopunguzwa kwa mujibu wa marekebisho hayo, ni pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, Viongozi wengine ambao hawajajumuishwa katika ibara ndogo ya (5) wataainishwa katika sheria itakayotungwa na Bunge kama ibara ndogo ya (5) inavyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii na isomeke kama Ibara ya 251 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.10IBARA YA 227: Deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tisa zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba. Kamati tatu zinapendekeza marekebisho kwenye ibara ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

(a) kuongeza maneno "**na faida inayolipwa juu ya deni hilo**" baada ya maneno **"Serikali ya Jamhuri ya Muungano"**.

(b) kuifuta na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa Ibara hii, deni la Taifa maana yake ni deni lenyewe na pia faida inayolipwa juu ya deni hilo, fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni polepole na gharama zote zinazoambatana na usimamizi wa deni hilo;

(c) kuibadili ibara ndogo ya (2) iwe ya (1) na ibara ndogo ya (1) iwe ya (2), na kufuta maneno **"kwa madhumuni ya ufafanuzi wa Ibara hii"** mwanzoni mwa ibara ndogo ya (2). Sasa Ibara hii itakuwa na mpangilio ufutao:

"(1) Deni la Taifa litajumuisha deni la Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja deni lolote litakalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Deni la Taifa litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina".

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi imeona kwamba, maudhui yaliyomo katika Ibara hii yanajitosheleza na hivyo inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba na isomeke kama Ibara ya 252 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.11 IBARA YA 228: Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kukopa. Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Katiba. Isipokuwa Kamati mbili zinapendekeza maboresho kama ifuatavyo:

(a) kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya kwa lengo la kuondoa sharti la ukomo wa deni la Taifa na madhumuni ya deni hilo;

(b) kufuta ibara ndogo ya (3) na maudhui yake kujumuishwa katika ibara ndogo ya (2); na

(c) kuongeza ibara ndogo mpya ya (4) itakayosomeka kama ifuatavyo:

"(4) Bunge litatunga sheria itakayoweka utaratibu wa kusimamia ustahimilivu wa deni la Taifa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge, Kamati ya Uandishi, inaona kwamba maudhui yaliyoanishwa katika Ibara hii yanajitosheleza kwa kuwa mapendekezo kama yalivyo katika Rasimu ya Tume ni ya msingi na yanalengo la kudhibiti deni la Taifa ili lisivuke uwezo wa Taifa kulipa, pia kuhakikisha kuwa mikopo inayochukuliwa ina tija na manufaa kwa maendeleo ya wananchi. Aidha, maudhui ya ibara ndogo za (2) na (3) yanalenga kuweka utaratibu mzuri wa kusimamia deni la taifa ikiwemo kuhakikisha ustahamilivu wa Deni la Taifa.

Hivyo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba na isomeke kama Ibara ya 253 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.12 IBARA YA 229: Mamlaka za Serikali za Nchi Washirika kukopa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu mamlaka za Serikali za Nchi Washirika kukopa. Kamati mbili zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba. Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho ambayo yataandika upya Ibara hii kwa lengo la kuweka masharti ya mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na imefanyia marekebisho kwenye maelezo ya pembeni ya Ibara hii ili yasomeke **"Mamlaka ya Zanzibar kukopa"** na imeipa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mamlaka ya kukopa fedha ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano, kwa ajili ya kugharamia shughuli zilizo chini ya mamlaka yake kwenye ibara ndogo ya (2). Aidha, inaweka sharti kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kudhamini mkopo, unaoombwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya mashauriano na makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeifanyia marekebisho ibara ndogo ya (3) ili kutoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria inayoweka utaratibu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutoa dhamana ya mikopo ya Serikali ya Mapinduzi. Aidha, Kamati ya Uandishi imeifuta ibara ndogo ya (4) ili maudhui yake yazingatiwe kwenye ibara ndogo (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii na isomeke kama Ibara ya 254 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.13 IBARA YA 230: Masharti ya kutoza kodi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Masharti ya Kutoza Kodi. Kamati tatu zinapendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati nane zinapendekeza kwamba Ibara hii ifutwe na iandikwe upya, ili kuweka bayana mamlaka ya kutoza kodi yawe ni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa yale Mambo ambayo ni ya Muungano na yasiyo kuwa ya Muungano kwa Tanzania Bara.

Aidha, Kamati moja inapendekeza ifanyiwe marekebisho ya kuongeza ibara ndogo ambayo itaweka masharti ya Serikali kupata mkopo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Muungano pamoja na kuweka masharti ambayo kodi zote ni lazima zitozwe kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo ya Kamati zote, Kamati ya Uandishi imeona ipo haja ya kuiandika upya Ibara hii ili kuainisha mamlaka ya Jamhuri ya Muungano kutoza kodi kwa Mambo yote ya Muungano na Mambo yasiyo ya Muungano yanayoihusu Tanzania Bara kwenye ibara ndogo ya (1), na mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoza kodi kwa Mambo yasiyo ya Muungano yanayoihusu Zanzibar kwenye ibara ndogo ya (2). Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji kodi ili kuondoa kero na mgongano katika masuala ya ukusanyaji kodi. Aidha, Kamati imeifanyia marekebisho ibara ndogo ya (3) ili kuboresha maudhui yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na marekebisho hayo maelezo ya pembeni yanayopendekezwa yasomeke **"Mamlaka ya kutoza kodi"** badala ya **"Masharti ya kutoza kodi".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii imeandikwa upya na isomeke kama Ibara ya 255 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.14 IBARA YA 231: Vyanzo vya Mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu vyanzo vya mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kamati nane zinapendekeza Ibara hii ifutwe na kuandikwa upya ili kuainisha vyanzo mbalimbali vya mapato ya Serikali kutokana na kodi na tozo katika taasisi za Muungano, mikopo na misaada kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano pamoja na mapato ya Serikali yatokanayo na shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, Kamati moja imependekeza Ibara hii ifutwe kutokana na sababu kwamba msingi wa maudhui ya Ibara hii unaakisi muundo wa Serikali Tatu na Kamati tatu zinapendekeza kuifanyia marekebisho aya ya (c) ili isomeke "**mapato yasiyo ya kodi yatokanayo na tozo mbalimbali za taasisi za Muungano"** ili kutoa mwanya kwa Serikali kupokea mapato endapo vyanzo vipya vya mapato vitapatikana. Aidha, aya hii imependekezwa kusomeka **"Michango kutoka Tanzania Bara na Zanzibar"** ili aya hiyo ijitosheleze kimaudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi imeifuta na kuiandika Ibara hii kwa lengo la kuainisha vyanzo vya mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na gawio na tozo

mbalimbali zinazotolewa na taasisi za Muungano, mchango kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Mikopo na misaada kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano na mapato mengine ya Serikali yanayotokana na shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuweka mapato mengine kwenye aya ya (e) ni kuzingatia kwamba vyanzo vyote vipya vitakavyojitokeza vinazingatiwa katika Ibara hii. Aidha, kwa kuzingatia kwamba Serikali huwa inapata misaada kutoka ndani na nje ya nchi, Kamati ya Uandishi imeona ni busara kuongeza misaada kwenye aya ya (d) kuwa ni mojawapo ya vyanzo cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imependekeza ibara ndogo ya (2) inayotoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria kwa ajili ya kuweka orodha ya vyanzo vingine vya mapato yatokanayo na shughuli mbalimbali pamoja na utaratibu na masharti ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato katika Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeaindika upya Ibara hii na inapendekeza isomeke kama Ibara ya 255 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.15 IBARA YA 232: Ununuzi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu ununuzi wa umma. Kamati saba zinapendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati tano zinapendekeza kuifanyia marekibisho Ibara hii kama ifuatavyo:

(a) kuongeza maneno **"kwa kuzingatia bei halisi ya soko kwa wakati huo"** mwishoni mwa ibara ndogo ya (1);

(b) kufuta neno **"utazingatia"** lililopo katika ibara ndogo ya (2) na badala yake kuweka maneno **"utatoa kipaumbele";** na

(c) kufuta Ibara hii ili sheria itakayotungwa na Bunge ndio ifafanue jambo hili ambalo kimsingi si la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo yaliyotolewa, Kamati ya Uandishi inapendekeza kufutwa na kuandika upya ibara ndogo ya (2) kwa kutoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria itakayoainisha mfumo wa manunuzi wa Serikali na taasisi zake ambao utazingatia misingi maalum iliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 256 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.16 IBARA YA 233: Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano. Kamati zote kumi na mbili zinapendekeza ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kwenye ibara ndogo ya (1), kwa kuongeza maneno **"ya Tanzania**" baada ya neno **"Benki Kuu",** kufuta maneno **"itakayojulikana kuwa**" na kuweka badala yake neno **"itakayoitwa**" na pia kufuta maneno **"ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo**:";

(b) kuongeza majukumu ya Benki Kuu ya Tanzania yafuatayo:

(i) kutunza Akaunti ya Fedha za Serikali;

(ii) kusimamia sera za kifedha;

(iii) kusimamia Mabenki na vyombo vya fedha nchini;

(iv) kusimamia masoko yote ya fedha isipokuwa soko la mitaji.

(c) kutenganisha katika aya ya (a) jukumu la kutoa sarafu, kudhibiti na kusimamia mzunguko wa sarafu;

(d) kutenganisha masharti ya kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Tanzania na majukumu yake katika ibara ndogo tofauti;

(e) kwenye ibara ndogo ya (3), kwa kufuta neno **"uwakilishi**" na kuweka badala yake neno **"uwiano**", na kuongeza maneno **"jinsia na uwakilishi wa watu wenye ulemavu na**" mara baada ya neno **"utakaozingatia**" na maneno **"ikiwa ni pamoja na sifa za watendaji wakuu**" mara baada ya maneno **"utendaji wa Benki Kuu**";

(f) kuifuta na kuiandika upya ili isomeke: "**kutoa mamlaka kwa Bunge la Jamhuri kutunga sheria itakayoweka kuhusu mamlaka, muundo na shughuli za Benki Kuu ya Tanzania utakaozingatia ushiriki na uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano"**;

(g) kufuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (3) ili kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria itakayoweka masharti kuhusu muundo wa Benki Kuu, mamlaka, shughuli na utendaji wa Benki Kuu**;** na

(h) kuongeza ibara ndogo mpya itakayozungumzia Gavana na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo yote kwa ujumla yana lengo la kupanua wigo wa majukumu na mamlaka ya Benki Kuu. Aidha, baadhi ya marekebisho haya yamelenga kuongeza masuala mbalimbali, kama usawa wa kijinsia, uwakilishi wa watu wenye ulemavu, nafasi ya madaraka ya Gavana na Naibu Gavana, na uwiano na ushiriki wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano katika uendeshaji wa shughuli za Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi imekubaliana na

pendekezo la kuigawa ibara ndogo ya (1) katika ibara ndogo mbili; ibara ndogo ya (1) inahusu kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano, na ibara ndogo ya (2) inayohusu Majukumu ya Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano. Kabla ya marekebisho haya, ibara ndogo ya (1) ilikuwa imejumuisha masula yote mawili kwenye ibara ndogo ya (1). Kwa kuzingatia marekebisho hayo, ibara ndogo ya (2) itasomeka kuwa ibara ndogo ya (3) na ibara ndogo zinazoendelea zitafuata mtiririko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inaafiki wazo la kuziandika upya baadhi ya aya za ibara ndogo ya (1) kwa madhumuni ya kuzifafanua vizuri aya hizo na kuondokana na suala la aya moja kubeba maudhui mengi. Mfano mzuri ni aya ya (a). Kwa mantiki hiyo, Kamati imezifuta aya (a) na (d) na kuanzisha aya mpya ya (a) hadi (f).

Pia, Kamati ya Uandishi inaafiki pendekezo la kuifanyia marekebisho aya ya (d) kwa kufuta maneno "Nchi Washirika" ili kuendana na dhana ya muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hata hivyo, Kamati ya Uandishi inaona kuwa ibara ndogo ya (2) isifutwe kwa sababu kimsingi ibara ndogo hiyo inatoa uhuru wa Kikatiba *(Constitutional*

Autonomy) kwa Benki Kuu kutekeleza shughuli na majukumu yake bila kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote. Kufutwa kwa ibara ndogo hii kunaweza kuleta athari hasi katika utendaji wa chombo hiki nyeti katika nchi yetu na watendaji wake. Hivyo, Kamati ya Uandishi inaona kwamba maudhui ya ibara ndogo ya (2) yabaki kama yalivyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inaafiki pendekezo la kuipa Benki Kuu ya Tanzania jukumu la kutunza akaunti ya fedha za Serikali kwa lengo la kuendeleza utaratibu unaotumika sasa pamoja na kuzingatia usalama wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ya Uandishi inaona suala la kuongeza jukumu la kuandaa na kusimamia sera za kibajeti kwa kuwa kwa kawaida masuala hayo yanasimamiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya Fedha. Endapo Benki Kuu itapewa jukumu hilo, ni dhahiri kwamba Wizara yenye dhamana na masuala ya Fedha itakuwa imeondolewa jukumu kubwa na la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana kwamba suala la kuongezwa kwa ibara ndogo mpya inayohusu nafasi ya madaraka ya Gavana na Naibu Gavana

ni vizuri likashughulikiwa kwenye sheria kama inavyopendekezwa kwenye ibara ndogo ya (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mapendekezo hayo, Ibara hii imeandikwa upya na Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 257 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

16.17IBARA YA 234: Benki za Serikali za Nchi Washirika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Benki Kuu za Serikali za Nchi Washirika. Katika Ibara hii, Kamati kumi na moja zinapendekeza Ibara hii ifutwe, na Kamati moja inapendekeza ifanyiwe marekebisho yafuatayo:

(a) kuifuta Ibara hiyo na kuiandika upya ili kutoa mamlaka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha Benki zitakazokuwa na jukumu la kutunza akaunti na fedha na, kusimamia sera za kifedha na benki za biashara katika mamlaka yao."; na

(b) kuongeza Ibara mpya inayohusu "Tume ya Pamoja ya Fedha", Ibara inayohusu "Majukumu ya Tume" na Ibara inayohusu "Akaunti ya Fedha ya Pamoja".

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inashauri kwamba Ibara ya 234 ifutwe kwa kuwa maudhui yake yamezingatiwa katika Ibara 257 na

imeona kuwa zisianzishwe Benki Kuu mbili kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia mfumo wa Seriakali unaopendekezwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza Ibara mpya inayohusu "Tume ya Pamoja ya Fedha", Ibara inayohusu "Majukumu ya Tume" na Ibara inayohusu "Akaunti ya Fedha ya Pamoja". Kamati ya Uandishi inaafiki mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na ufafanuzi wake umeainishwa kwenye maelezo na uchambuzi wa Ibara zilizotangulia za Sura hii.

SURA YA KUMI NA TANO

ULINZI NA USALAMA WA JAMHURI YA MUUNGANO

17.0 IBARA YA 235: Usalama wa Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu usalama wa Taifa. Kamati mbili zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati kumi zinapendekeza Ibara ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kuongeza maneno "**kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 2 ya Katiba hii"** baada ya maneno "**Jamhuri ya Muungano**" katika ibara ndogo ya (2), kuongeza maneno "**mito, maziwa na visiwa"** baada ya neno "**anga**" katika ibara ndogo ya (2), na kuongeza maneno "**mila, desturi na"** kabla ya neno "utamaduni" katika aya ya (c) ya ibara ndogo ya (3). Aidha, Kamati moja ilipendekeza kuongeza maneno "**kwa mujibu wa Sheria za nchi"** baada ya neno "**jamii"** katika aya ya (c) ya ibara ndogo ya (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyachambua mapendekezo mbalimbali ya Kamati za BungeMaalum na imeaafiki pendekezo la kuongeza maneno "**kama ilivyoainishwa katika Ibara hii"** katika ibara ndogo ya (2), ili kuleta uwiano na Ibara ya 2 ya Rasimu ya Tume ya Katiba inayozungumzia eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Kamati ya Uandishi imeiboresha ibara hii na inapendekeza isomeke kama Ibara ya 258 ya Rasimu hii ya Katiba inayopendekeza.

17.1 IBARA YA 236: Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa, Kamati tatu zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati tisa zilipendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kutaka kujumuisha Jeshi la Magereza ili liweze kuingia katika orodha ya vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa, kwa kuwa chombo hicho kinahusika na masuala ya ulinzi na usalama, kuongeza maneno "**rasilimali za nchi"** katika ibara ndogo ya (2) baada ya maneno "**Jamhuri ya Muungano"**, kufuta neno "**Rais"** katika ibara ndogo ya (5) na badala yake kuweka maneno "**Amiri Jeshi Mkuu",** kuongeza maneno "**kujiunga na chama chochote cha siasa au"** katika aya ya (b) ya ibara ndogo ya (3) na kuongeza aya mpya ya (d) itakayoingiza Idara ya Uhamiaji kama sehemu ya vikosi vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inakubaliana na mapendekezo ya kuongeza maneno **"rasilimali za nchi"** ili rasilimali hizo ziweze kulindwa. Aidha, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la kurekebisha ibara ndogo ya (5) ili kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama viweze kuwa chini ya Amiri Jeshi Mkuu ambaye ndiye mwenye mamlaka ya mwisho kuhusu vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana na hoja ya kutaka mtumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama kutojiunga na chama chochote cha siasa ili asiweze kufanya maamuzi kwa kufuata chama ambacho anakipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiboresha Ibara hii na baada ya marekebisho hayo Ibara hii sasa itasomeka kama Ibara ya 259 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

IBARA YA 237: Kuanzishwa kwa Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kuanzishwa kwa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa. Kamati moja ilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati kumi na moja zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali kwa kufuta na kuandikwa upya ibara ndogo ya (1), kubadili jina la Baraza na kuwa Baraza la Usalama la Taifa, na pia pendekezo la kupunguza idadi ya Wajumbe wa Baraza la Usalama na kumpendekeza Rais awe Mwenyekiti wa Baraza la Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyachambua mapendekezo hayo, inapendeza ibara ndogo ya (1) ifutwe na kuandikwa upya kama ilivyopendekezwa na Kamati mbalimbali. Aidha, Kamati ya Uandishi imetafakari hoja ya kubadili jina la Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa kuwa

Baraza la Usalama la Taifa na kuona hoja hiyo ni ya msingi kwa kuwa jina hilo liweze kuendana na jina la Baraza lililomo kwenye Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia, inakubaliana na hoja kuwa Rais awe Mwenyekiti wa Baraza la Usalama kwa kuzingatia unyeti wa chombo hicho kwa kuwa Rais ndiye Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi Mkuu wa nchi. Aidha, Kamati ya Uandishi inakubaliana na pendekezo la kupunguza idadi ya Wajumbe wa Baraza la Usalama la Taifa kwa lengo la kubakisha Viongozi Wakuu wa Serikali na endapo Baraza litaona kuwa ipo haja ya kuongeza Viongozi wengine katika vikao vyao basi wanaweza kumwalikwa Waziri yeyote ili aweze kuhudhuria katika kikao iwapo hoja inayozungumziwa katika kikao hicho itakuwa inamuhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii iandikwe upya na isomeke kama Ibara ya 260 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.2 IBARA YA 238: Majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa. Kamati mbili zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na

Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho mbalimbali katika ibara ndogo ya (1)(c) kwa kufuta maneno "Serikali za Nchi Washirika" na badala yake kuweka maneno "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar", kufuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya, kufuta Maelezo ya Pembeni ili yasomeke "Majukumu ya Baraza la Usalama la Taifa", kuongeza neno "wa" baada ya neno "usimamizi" katika ibara ndogo ya (1)(d), kufuta maneno "kila mwaka" katika ibara ndogo ya (2) na kuweka maneno "wakati wowote atakapoona inafaa" na kufuta majukumu yaliyoainishwa katika Ibara hii ili yaainishwe katika sheria itakayotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeyachambua na kuyatafakari maoni na kulichukua pendekezo la kubadilisha Maelezo ya Pembeni na jina la Baraza ili lijulikane kama 'Baraza la Usalama la Taifa' badala ya kuitwa 'Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa' na pia kufanya maboresho mengine ya kiuandishi katika Ibara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya ibara hii kama Ibara ya 261 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.3 IBARA YA 239: Kuanzishwa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kuanzishwa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Kamati sita zinapendekeza ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati sita zinapendekeza Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwa kuongezwa maneno "pamoja na mali zao" katika ibara ndogo ya (2), kuboresha ibara ndogo ya (2) kwa kuweka sharti kwamba Rais anapotaka kuanzisha vikosi vingine ashauriane na Baraza la Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia maoni ya Kamati na mijadala ya Bungeni inapendekeza kuwa kuwa Rais ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi la Ulinzi na Usalama basi awe na mamlaka ya kuanzisha vikosi vyingine vya jeshi kama atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba na isomeke kama inavyoonekana katika Ibara ya 262 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.4 IBARA YA 240: Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Kamati nane zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati nne zinapendekeza ibara irekebishwe kwa kuongeza sharti la Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kuwa ni raia wa kuzaliwa wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumtaka Rais kabla ya kumteua Mkuu huyo ashauriane na Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati zote kuhusiana na Ibara hii na kukubaliana na pendekezo la kutaka Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa nafasi hii ni nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kupitia mapendekezo hayo imeirekebisha na kuiandika upya Ibara hii kama Ibara ya 263 ya Rasimu ya Katiba inayopendekezwa.

17.5 IBARA YA 241: Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu. Kamati tisa zilipendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati tatu zilipendekeza ibara zifanyiwe marekebisho kwa kuongeza ibara ndogo mpya ya (4) ili kutoa tafsiri ya neno mwanajeshi; kuongeza mwishoni mwa ibara ndogo ya (2)(a) na (b), maneno **"kwa kuzingatia uwiano wa pande mbili za Muungano"** na kufuta maneno **"utakuwa batili"** katika ibara ndogo ya (3) na badala yake kuandika maneno **"ametenda kosa la uhaini".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyachambua mapendekezo haya, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa ufafanuzi wa neno Mwanajeshi usiwekwe katika Katiba bali ufafanuzi huo utolewe katika sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza kufuta aya (c), (e) na (d) katika ibara ndogo ya (1) kwa sababu majukumu yaliyoainishwa katika aya hizi yanaweza kutekelezwa na kuwekewa utaratibu katika sheria za nchi au kushughulikiwa kiutawala.

Vilevile, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuongeza madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu ya kuwatunuku Kamisheni Maafisa katika majeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke kama Ibara ya 264 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.6 IBARA YA 242: Tume ya Utumishi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Tume ya Utumishi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Kamati nane zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba, Kamati moja inapendekeza Ibara hii ifutwe, na

Kamati tatu zinapendekeza ibara ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza sharti kuwa uteuzi wa watumishi katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania uzingatie uwiano wa pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo ya Kamati zote na ina maoni kuwa maudhui yake yamezingatiwa katika Ibara nyingine ya Katiba hii. Hivyo, inapendekezwa Ibara hii ifutwe.

17.7 IBARA YA 243: Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati kumi na moja zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati moja inapendekeza kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya ili kuliwezesha Bunge kutunga sheria kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Jeshi hilo. Aidha, kutokana na majadiliano ya Wabunge Bungeni Kamati ya Uandishi ilidhihirika kwamba hapa nchini kuna jeshi moja tu ambalo ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi na hivyo inapendekezwa Jeshi la Polisi litambulike kuwa ni Idara ya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Uandishi kutafakari mapendekezo haya, inapendekeza kwamba jina la

Jeshi la Polisi libadilishwe ili itambulike kuwa ni Idara ya Polisi ya Jamhuri ya Muungano.

Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii isomeke Ibara ya 265 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.8 IBARA YA 244: Misingi ya Utendaji wa Jeshi la Polisi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Misingi ya Utendaji wa Jeshi la Polisi, Kamati mbili zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati kumi zinapendekeza marekebisho mbalimbali kwa kuongeza maneno "**askari na**" kabla ya neno **"wafanyakazi"** katika aya (a) ya ibara ndogo ya (1), kufuta maneno **"vya Nchi Washirika"** baada ya neno **"uhalifu",** na badala yake kuweka maneno **"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar"** katika ibara ndogo ya (2) ili iendane na muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa na pia kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuiandika upya ili kuwezesha Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na vyombo vingine vinavyohusika na kupambana na uhalifu katika Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo yaliyotolewa katika Kamati mbalimbali na kukubaliana na hoja ya kufuta maneno **"**vya Nchi Washirika"

baada ya neno "uhalifu", na badala yake kuweka maneno "Jamhuri ya Muungano" katika ibara ndogo ya (2) ili kuendana na muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa kwa sasa. Aidha, ibara ndogo ya (3) imeongezwa ili kulipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria wakati wa kutekeleza kazi na majukumu ya Idara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekezwa Ibara hii ifutwe kwa kuwa maudhui yake yamezingatiwa kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.9 IBARA YA 245: Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati saba zinapendekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati tano zinapendekeza marekebisho mbalimbali kwa kuweka masharti kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi ili awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano, kuondoa sharti la Rais kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa na badala yake ashauriane na Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais, Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wakati wa kumteua Mkuu wa Jeshi la Polisi, kuweka sharti linalotaka Bunge kumthibitisha Mkuu wa Majeshi ili kumpa Rais mamlaka kamili na ya mwisho katika uteuzi, kuongeza Ibara mpya itakayoweka masharti kuhusu sifa za Mkuu wa Jeshi la Polisi na Naibu Mkuu wa Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na uraia wa

kuzaliwa, kuweka ibara ndogo mpya itakayoanzisha cheo cha Naibu Mkuu wa Jeshi la Polisi, kuweka ibara ndogo itakayoweka masharti kuwa iwapo Mkuu wa Jeshi la Polisi atateuliwa kutoka upande mmoja wa Muungano, basi Naibu wake ateuliwe kutoka upande mwingine wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo kutoka katika Kamati mbalimbali kuhusu uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi inapendekeza kufuta maneno "baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa" ili kutoa fursa kwa Rais kuweza kufanya uteuzi bila ya kuingiliwa na chombo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la kuanzishwa kwa nafasi ya Naibu Mkuu Idara ya Polisi na masharti yake ambayo yamependekezwa, Kamati ya Uandishi ina maoni kuwa suala hilo linahusu muundo wa Idara ya Polisi na kwamba itafaa zaidi kama itaekwa katika sheria au kanuni na sio katika Katiba.

Vile vile, Kamati ya Uandishi imeunga mkono pendekezo la Kamati za Bunge la kuweka sharti kuwa Mkuu wa Idara ya Polisi awe raia wa kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwa Ibara hii irekebishwe na isomeke kama Ibara ya 266 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.10 IBARA YA 248: Kuanzishwa kwa Idara ya Usalama ya Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kuanzishwa kwa Idara ya Usalama wa Taifa. Kamati zote zilipendekeza kuwa Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imepitia mapendekezo haya na kufanya marekebisho kwa kufuta maneno "kulinda Katiba hii" na "za Nchi" ili kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi na kimaudhui na itasomeka kama Ibara ya 268 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Vile vile, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuongeza Ibara mpya ya 267 inayohusu uanzishwaji wa huduma nyingine za ulinzi na kutoa mamlaka kwa Bunge kutunga sheria itakayoweka masharti yatakayoruhusu kuanzisha, kudhibiti na kusimamia taasisi nyingine zinazotoa huduma za ulinzi.

17.11 IBARA YA 249: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu uteuzi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa. Kamati nne

zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba na Kamati tisa zinapendekeza marekebisho kwa kuongeza sifa za anayeiongoza idara hii kuwa Mkurugenzi Mkuu na siyo Mkurugenzi kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba. Pia, kulikuwa na mapendekezo la kumtaka Mkurugenzi huyo awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari mapendekezo hayo na kuridhika kuwa Idara ya Usalama wa Taifa kwa sasa iongozwe na Mkurugenzi Mkuu kama ilivyopendekezwa na Kamati mbalimbali. Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza ibara ndogo ya (2) inayoweka sharti kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa awe ni raia wa kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapendekezo mbalimbali ya Kamati na mjadala ndani ya Bunge, Kamati ya Uandishi imefanya marekebisho ya kiuandishi ili maudhui ya Ibara hii yaweze kujitosheleza. Kamati ya Uandishi ilipendekeza Ibara hii igawanywe katika maeneo mawili ambayo ni eneo la kuanziashwa kwa Idara na Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, na inapendekezwa Ibara hizo mbili zisomeke kama Ibara ya 268 na 269 kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

SURA YA KUMI NA SITA

MENGINENYO

17.12 IBARA YA 251: Utaratibu wa kujiuzulu katika Utumishi wa Umma

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu utaratibu wa kujiuzulu katika Utumishi wa Umma. Kamati tisa zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba kwa sababu maudhui yake yanajitosheleza. Kamati tatu zimetoa mapendekezo ya kufanya marekebisho mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) kuifuta na kuaindika upya ibara ndogo ya (1)(c) ili kumjumuisha Makamu wa Kwanza wa Rais katika utaratibu wa kujiuzulu kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi;

(b) kufuta neno "Mbunge" katika ibara ndogo ya (1)(e) na badala yake kuweka "Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais";

(c) kuongeza aya mpya ya (f) inayomtaja Waziri Mkuu kwamba endapo atajiuzulu taarifa yake ataiwasilisha kwa Rais; na

(d) kuongeza maneno "au Waziri Mkuu" kwenye ibara ndogo ya (1)(c) baada ya neno "Rais".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge,

inapendekeza maneno "wa Kwanza" yaongezwe katika ibara ndogo ya (1)(c) ili kuweka utaratibu wa Makamu wa Kwanza wa Rais kujiuzulu kwa kuwasilisha taarifa yake ya kujiuzulu kwa Rais.

Aidha, Kamati imezingatia pendekezo la kuiandika upya ibara ndogo ya (1)(d) kwa madhumuni ya kuweka utaratibu wa Waziri Mkuu kujiuzulu kwa kuwasilisha taarifa yake ya kujiuzulu kwa Rais na nakala kwa Spika kwa sababu nafasi hiyo ilikuwa haikujumuishwa kwenye Rasimu ya Tume ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imetafakari maoni yaliyotolewa na Kamati za Bunge na kuiandika upya kama inavyosomeka katika Ibara ya 270 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.13 IBARAYA 252: Masharti kuhusu kukabidhi Madaraka

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu masharti kuhusu kukabidhi madaraka. Kamati kumi zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza. Aidha, Kamati mbili zinapendekeza kuifanyia marekebisho kama ifuatavyo:

(a) kufuta maneno **"au zaidi"** kwenye ibara ndogo ya (2)(b) na kufuta mistari minne ya mwanzo na kuiandika upya;

(b) kufuta neno "**kukabidhiana"** na badala yake kuandika neno **"kukabidhi"** katika ibara ndogo ya (2) ili kuweka matumizi ya Kiswahili fasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyatafakari mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge na mijadala ndani ya Bunge, imeridhia pendekezo la kufuta neno "kukabidhiana" kwenye ibara ndogo ya (2) na badala yake kuweka neno "kukabidhi".

Aidha, Kamati ya Uandishi, inapendekeza maneno **"au zaidi"** katika ibara ndogo a (2)(b) yasifutwe kwa sababu upo uwezekano watu zaidi ya wawili kushika madaraka kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandisihi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo katika Rasimu ya Tume ya Katiba na isomeke kama Ibara ya 271 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.14 IBARAYA 254: Ufafanuzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu Ufafanuzi. Baada ya majadiliano Kamati moja inapendekeza Ibara hii ibaki kama ililivyo katika Rasimu ya Tume kwa msingi kwamba maudhui

yake yanajitosheleza. Kamati kumi na moja zimependekeza kuirekebisha kama ifuatavyo:

(a) kuongeza maneno "**Mahakama**", **"Serikali za Mitaa"**, **"Mahakama ya Rufani"** na **"Tanzania Bara";**

(b) kufuta maneno **''Nchi Washirika''**, **"Waziri Mwandamizi"** na **"Waziri Mkaazi"** ili kuendana na muundo wa Serikali mbili unaopendekezwa;

(c) kuongeza maneno ya ufafanuzi **"Askari**", **"Baraza la Wawakilishi"**, **"Bunge"**, **"Jaji Mkuu wa Zanzibar"**, **"Kiapo"**, **"Kiapo cha uaminifu"**, **"Mambo ya Muungano"**, **"Tanzania Bara"**, **"Waziri Mkuu";**

(d) kuongeza maneno **"Makundi madogo"**, **"Makundi Maalum" "Mtoto"** , **"Mzee"**, **"Kijana"**, **"Uchaguzi Mkuu"**, **"Raia"**, **"Maslahi ya Taifa"**, **"Jinsia"**, **"Mamlaka ya nchi"**, **"Ujamaa na Kujitegemea"**, **"Amri ya jeshi" "Askari" "Mahakama" na "Raia wa asili";**

(e) kurekebisha taratibu za kiuandishi katika ibara ndogo ya (2)(d) kwa kufuta maneno **"Serikali ya zamani ya Zanzibar"** na badala yake kuweka maneno **"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar";**

(f) kufuta maneno **"zamani"** na **"ya zamani"** katika ibara ndogo ya (2)(d) kwa lengo la kurekebisha makosa ya kiuandishi;

(g) kufuta aya ya (e) na maudhui yake yahamishiwe kwenye aya ya (d);

(h) kufuta "**ya juu"** na kuweka neno **"kuu";**

(i) kufuta neno **"kilichoandikishwa"** kuweka **"kilichosajiliwa";**

(j) kuongeza maneno **"Mkuu wa Nchi", "Kiongozi wa Serikali"** na **"Amiri Jeshi Mkuu"** katika ibara ndogo ya (2)(a) baada ya neno "**Mkuu";**

(k) kupendekeza ufafanuzi wa maneno mbalimbali yaliyotumika katika Katiba kama vile "**Waziri Mkuu", "Makamu wa Kwanza wa Rais", "Makamu wa Pili wa Rais", "Tanzania Bara", "Tanzania Zanzibar", "Serikali za Mitaa", "Raia wa asili", "Mahakama Kuu", "Askari"** na **"Mambo ya Muungano".**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kuyatafakari mapendekezo hayo, imeridhia kuongeza ufafanuzi wa baadhi ya maneno kwenye ibara hii ili kuweka bayana maana halisi ya maneno hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imelikubali pendekezo la kuongeza maneno kwenye baadhi ya tafsiri ili kuweka bayana maudhui yaliyokusudiwa. Vile vile, Kamati ya Uandishi imefuta ufafanuzi wa neno **"Waziri Mwandamizi"** kwa kuwa neno hilo halikutumika kwenye Rasimu ya hii Mapendekezo. Aidha, Kamati ya Uandishi inapendekeza maneno **"kijana"** na **"wazee"** yasifafanuliwe katika Ibara hii

kwa kuwa yanaweza kutolewa ufafanuzi katika sheria mahsusi. Vile vile, tafsiri ya neno **"mtoto"** imeshatafsiriwa katika Ibara ya 50 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, imeiandika upya Ibara hii na inapendekeza isomeke kama Ibara ya 272 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.15 IBARAYA 255: Jina la Katiba na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu jina la Katiba na kuanza kutumika kwake. Kamati kumi na moja zinapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume na Kamati moja inapendekeza kuongeza ibara ndogo mpya ya (3) itakayohusu mipaka ya kutumika kwa Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati za Bunge na mijadala Bungeni, imeridhia kuongeza ibara ndogo ya (3) ambayo inaweka masharti ya kutumika kwa Katiba hii kwa Tanzania Bara na Tanzania na Zanzibar kwa Mambo ya Muungano na pia kutumika Tanzania Bara pekee kwa Mambo yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imeiandika upya Ibara hii na inapendekeza isomeke kama Ibara ya 273 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

17.16 IBARAYA 256: Kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, [Sura ya 2].

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya majadiliano Kamati zote Kumi na mbili zimependekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari mapendekezo hayo, Kamati ya Uandishi inapendekeza Ibara hii ibaki kama ilivyo kwenye Rasimu ya Tume kwa kuwa maudhui yake yanajitosheleza. Hivyo, Ibara hii isomeke kama Ibara ya 274 ya Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

18.0 NYONGEZA YA KWANZA

[Imetajwa katika Ibara ya 71(3)]

Mambo ya Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii inahusu Nyongeza ya Mambo ya Muungano. Kamati zote kumi na mbili zimetoa mapendekezo ya kuboresha Nyongeza ya Mambo ya Muungano kama ifuatavyo:

(a) kufuta na kuandika upya jambo la nne la Muungano linalohusu "**Sarafu na Benki Kuu"** ili lisomeke**: "Mambo yote yanayohusika na Sarafu na Fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti); mabenki (pamoja na mabenki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabenki; fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni;**

(b) kufuta na kuandika upya jambo la sita la Muungano linalohusu **"Usajili wa Vyama vya Siasa"** ili lisomeke: **"Uandikishaji wa Vyama vya Siasa na mambo mengine yanayohusiana; na"**

(c) kufuta na kuandika upya jambo la saba linalohusu **"Ushuru wa Bidhaa na Mapato yasiyo ya Kodi yatokanayo na Mambo ya Muungano"** ili lisomeke: **"Kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha";**

(d) kuongeza Mambo Mapya ya Muungano kama ifuatavyo:

1. **Elimu ya Juu**
2. **Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na Mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo.**
3. **Mawasiliano.**
4. **Usalama wa Usafiri wa Anga.**
5. **Utabiri wa Hali ya Hewa.**
6. **Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano.**
7. **Mahakama ya Rufani.**
8. **Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano.**
9. **Takwimu.**
10. **Mamlaka ya kutangaza Hali ya Hatari.**
11. **Sensa.**
12. **Bunge la Jamhuri ya Muungano.**
13. **Masuala ya Kimataifa yanayohusu Usafirishaji Baharini.**
14. **Mikataba ya Biashara.**
15. **Mikopo inayohitaji Dhamana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano**
16. **Polisi.**
17. **Posta na Simu.**
18. **Utafiti.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati na mjadala Bungeni

inapendekeza mambo yafuatayo yawe ndio mambo ya Muungano:

1. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
2. Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
3. Usalama na Usafiri wa Anga.
4. Uraia na Uhamiaji.
5. Polisi.
6. Sarafu na Benki Kuu.
7. Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na Mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengeneza nchini Tanzania na zinazosimamiwa na Idara ya Forodha.
8. Mambo ya Nje.
9. Usajili wa Vyama vya Siasa.
10. Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani.
11. Elimu ya Juu.
12. Baraza la Taifa la Mitihani na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo.
13. Utarabiri wa Hali ya Hewa.
14. Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu mambo yanayopendekezwa na Kamati ya Uandishi kuwa yawe mambo ya Muungano kama ifuatavyo:

(a) Elimu ya Juu na Baraza la Taifa la Mitihani na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inashauri masuala haya mawili yajumuishwe kwenye orodha ya Mambo ya Muungano kwa kuwa Elimu ya Juu na Baraza la Taifa la Mitihani ni vyombo vinavyohusika katika kutahini wanafunzi na hatimaye kuendelea na masomo katika ngazi za juu ili kupata wataalamu wa fani mbalimbali na kuandaa viongozi watarajiwa katika nchi.

Aidha, kwa kuyatambua masuala haya kuwa ni ya Muungano kutawezesha mambo haya kuratibiwa na kusimamiwa kwa pamoja ili kuwezesha utahini na udahili wa wanafunzi waliofaulu ili waweze kujiunga na elimu ya juu. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kudhibiti ubora wa elimu na hivyo kuwa na viwango vya elimu vinavyofanana kwa pande zote mbili za Muungano na kuleta usawa wa ushindani katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la Elimu ya Juu linajumuisha kupata elimu ndani na nje ya nchi, ni vizuri uratibu wake ukawa chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kulinda utambulisho wa Jamhuri ya Muungano pale ambapo wanafunzi wa pande zote mbili za Muungano wanapokuwa masomoni nje ya nchi.

(b) Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi, inapendekeza jambo hili liongezwe ili kuhakikisha kwamba vyombo, idara na taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zinazotekeleza kazi na shughuli zinazohusiana na mambo ya Muungano, zinakuwa na uwiano na uwakilishi wa watumishi kutoka pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Hii itawezesha vyombo, idara na taasisi za Muungano kuhudumiwa na watumishi kutoka pande zote mbili za Muungano, hivyo, kuakisi uhalisia wa kuwa ni vyombo vya Muungano.

(c) Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza jambo hili liongezwe kutokana na asili ya majukumu ya Mahakama hizi mbili. Aidha, kwa vile kila upande wa Muungano umepewa mamlaka ya kuwa na Mahakama hadi ngazi ya Mahakama Kuu, ni vizuri Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani zikatambuliwa kuwa sehemu ya Mambo ya Muungano. Hii itatoa fursa kwa wananchi ambao hawataridhika na maamuzi ya Mahakama za chini kutoka pande zote mbili za Muungano kukata rufaa ili kutafuta haki katika Mahakama za juu zaidi. Aidha, inapendekezwa Mahakama hizi zipewa mamlaka ya kusikiliza, kusuluhisha na

kuamua mashauri yatakayowasilishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano au na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu tafsiri au utekelezaji wa masharti ya Katiba hii.

(d) Utabiri wa Hali ya Hewa;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza suala hili liongezwe kwenye orodha ya Mambo ya Muungano kwa kuzingatia kwamba Utabiri wa Hali ya Hewa una uhusiano wa moja kwa moja wa maisha ya siku hadi siku ya kila Mtanzania. Kwa kuwa lengo kuu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni kuhakikisha kuna kuwepo na ustawi wa wananchi ni vyema Utabiri wa Hali ya Hewa ukasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(e) Polisi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi imekubaliana na pendekezo la Kamati nyingi la kuongeza suala la Polisi kuwa miongoni mwa Mambo la Muungano. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Idara ya Jeshi la Polisi ndio yenye dhamana ya kulinda watu, mali zao na usalama wao. Hivyo, ni muhimu likaongezwa katika orodha ya Mambo ya Muungano.

(f) Usalama na Usafiri wa Anga;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inaunga mkono kuongezwa kwa suala la Usalama na Usafiri wa Anga kuwa ni miongoni mwa mambo ya Muungano, kwa kuwa, usalama wa nchi unahusu anga pamoja na vyombo vinavyosafiri angani. Endapo usalama wa anga na usafiri utahatarishwa ni dhahiri kuwa usalama wa nchi utakuwa hatarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufafanuzi huo, mambo yaliyopendekezwa na Kamati mbalimbali pamoja na mjadala Bungeni ili yajumuishwe kwenye orodha ya Mambo ya Muungano kuhusu "Posta na Simu", "Mawasiliano", "Utafiti", "Sensa", "Takwimu", "Bunge la Jamhuri ya Muungano", "Mikataba ya Biashara", "Masuala ya Kimataifa yanayohusu usafirishaji wa baharini" na "Mikopo inayohitaji dhamana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano". Kamati ya Uandishi inapendekeza kwamba, kwa kuwa Ibara ya 122 ya Rasimu ya Katiba inapendekeza kuundwa kwa Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali kwa lengo la kuratibu masuala mbalimbali yanayohusu Serikali za pande mbili za Muungano, mambo hayo yaingizwe kwenye orodha ya Mambo ya Muungano yanayoweza kushughulikiwa na Tume hiyo.

Kutokana na sababu hizi, Nyongeza ya Kwanza ya Mambo ya Muungano ya Rasimu ya Tume imeandikwa upya na isomeke

kama inavyoonekana kwenye Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

19.0 NYONGEZA YA PILI

[Imetajwa katika Ibara ya 129(1)(b)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuwepo kwa Nyongeza ya Pili ya Katiba kwa ajili ya kuainisha Sheria ambazo mabadiliko yake ili yakubalike ni sharti kwanza yaungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Zanzibar. Sheria hizi ni kama zifuatazo:

1. Muswada wa Sheria wa kubadili masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano yanayohusu Mambo ya Muungano.
2. Kuongeza au kupunguza jambo lolote la Muungano.

20.0 NYONGEZA YA TATU

[Imetajwa katika Ibara ya 129(1)(c)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uandishi inapendekeza kuongezwa Nyongeza ya Tatu ya Mambo ya Muungano yanayohitaji kuungwa mkono kwa zaidi ya nusu ya kura halali zilizopigwa na wananchi wa Tanzania Bara na zaidi ya nusu ya kura halali zilizopigwa na wananchi wa Zanzibar katika kura ya maoni. Sababu ya mapendekezo haya ni kwa kuwa mabadiliko yake yanahitaji ushirikishwaji wa moja kwa moja wa wananchi kupitisha mabadiliko. Mambo hayo ni:

1. Muundo wa Jamhuri ya Muungano.
2. Kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano.
3. Kubadilisha masharti ya Ibara ya 129(1)(c) ya Katiba hii.

21.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na makini unaozingatia kasi na viwango. Kazi ya kujadili na kuandaa Katiba hii ilikabiliwa na hisia na mitazamo tofauti kutoka ndani na nje ya Bunge. Baadhi ya vikwazo hivyo ni pamoja na kufunguliwa mashauri ya kupinga kuendelea na mchakato huu katika Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano, kutolewa kwa kauli mbalimbali kutoka kwa viongozi wa dini, taasisi zisizo za kiserikali na baadhi ya wananchi. Hata hivyo, busara na hekima yako ilikuongoza ukaweza kuendelea na mchakato huu na hatimaye tunawasilisha taarifa ya kukamilika kwa kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Uandishi naomba kumshukuru Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan (Mb) kwa ushirikiano wake wa dhati kwa Kamati ya Uandishi na kwa Bunge Maalum katika kutoa miongozo na maelekezo ambayo kwa ujumla wake imesaidia kufanikisha shughuli hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Uandishi kwa kufanyakazi kwa kujituma bila ya kuchoka na kwa michango yao madhubuti ambayo ilichangia maboresho makubwa na muhimu ya kimantiki na kimaudhui katika Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama zitomshakuru Katibu wa Bunge Maalum la Katiba Ndugu Yahya Khamis Hamad pamoja na Naibu Katibu wake Ndugu Dkt. Thomas Didimu Kashilillah kwa ushirikiano wao wa karibu waliotupatia wakati Kamati yangu inatekeleza majukumu yake. Sambamba na hilo, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Uandishi kwa kazi ngumu waliyoifanya usiku na mchana ili kuweza kukamilisha kazi ya kuandaa Rasimu inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishukuru Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kututayarishia Rasimu ya Mapendekezo ya Katiba ambayo imetusaidia katika kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Uandishi walioshiriki katika kazi ya kuandaa Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Andrew John Chenge
2. Mhe. Mgeni Hassan Juma
3. Mhe. Dr. Natujwa S. Mvungi
4. Mhe. Ali Ahmed Uki
5. Mhe. Amina Dastan Mweta
6. Mhe. Almas Athuman Maige
7. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
8. Mhe. Magdalena Kamugisha Rwebangira
9. Mhe. Dr. Mahadhi Juma Maalim

10. Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema
11. Mhe. Dr. Tulia Ackson
12. Mhe. Ummy Mwalimu Ally
13. Mhe. Dr. Harrison George Mwakyembe
14. Mhe. Valerie Ndenengo-sya Msoka
15. Mhe. Elizabeth Maro Minde
16. Mhe. Angela Jasmine Kairuki
17. Mhe. Dkt. Pindi Chana
18. Mhe. Dkt. Asha-Rose M. Migiro
19. Mhe. Prof. Costa Ricky Mahalu
20. Mhe. Amon Anastaz Mpanju
21. Mhe. Evod Herman Mmanda
22. Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji
23. Mhe. Khadija Nassor Abdi

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru kwa mara nyingine tena Sekretarieti ambayo kwa kiasi kikubwa iliisaidia Kamati hii kukamilisha kazi ya kuandaa Rasimu hii ya Katiba Inayopendekezwa kwa ufanisi na kwa muda uliopangwa. Majina ya sekretarieti hiyo ni yafuatayo:

1. Ndg. Mussa Kombo Bakari - Mkuu wa Idara ya Uandishi wa Sheria
2. Ndg. Stephen Kagaigai - Naibu Mkuu wa Idara ya Uandishi wa Sheria
3. Ndg. Sarah K. Barahomoka - Mwandishi Mkuu wa

Sheria

4. Ndg. Oscar Godfrey Mtenda - Mwandishi wa Sheria
5. Ndg. Optat J. Mrina - Mwandishi wa Sheria
6. Ndg. Juliana Munisi - Mwandishi wa Sheria
7. Ndg. Bavoo Junus - Mwandishi wa Sheria
8. Ndg. Shabani Kabunga - Mwandishi wa Sheria
9. Ndg. Jacob Sarungi - Mwandishi wa Sheria
10. Ndg. Victor Kahangwa - Mwandishi wa Sheria
11. Ndg. Mark Mulwambo - Mwandishi wa Sheria
12. Ndg. Sarah D. Mwaipopo - Mwandishi wa Sheria
13. Ndg. Ali Ali Hassan - Mwandishi wa Sheria
14. Ndg. Fatma Saleh Amour - Mwandishi wa Sheria
15. Ndg. Mtumwa Said Sandal - Mwandishi wa Sheria
16. Ndg. Thabit Mlangi - Mwandishi wa Sheria
17. Ndg. Agnes Ndumbati - Mwandishi wa Sheria
18. Ndg. Nicodemus Chuwa - Mwandishi wa Sheria
19. Ndg. Pius Mboya - Mwandishi wa Sheria
20. Ndg. Prudence Rweyongeza - Mwandishi wa Sheria
21. Ndg. Matamus Fungo - Mwandishi wa Sheria
22. Ndg. Nesta Kawamala - Mwandishi wa Sheria
23. Ndg. Richard Mbaruku - Mwandishi wa Sheria
24. Ndg. Fatma Mtumweni - Mwandishi wa Sheria
25. Ndg. Ephery Sedekia - Mwandishi wa Sheria
26. Ndg. Angaza Mwipopo - Mwandishi wa Sheria
27. Ndg. Alice Mtulo - Mwandishi wa Sheria

28. Ndg. Paul Thomas Kadushi - Mwandishi wa Sheria
29. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Mwandishi wa Sheria
30. Ndg. Mossy V. Lukuvi - Mwandishi wa Sheria/Katibu Kamati
31. Ndg. Evangelina Manyama - Katibu Muhtasi
32. Ndg. Josephine Chalamila - Katibu Muhtasi
33. Ndg. Maryam Ramadhan Moh'd- Katibu Muhtasi
34. Ndg. Beatrice Mphuru - Katibu Muhtasi
35. Ndg. Salama Mwinyi Khamis - Katibu Muhtasi
36. Ndg. Ramadhan Sijamini Khatib - Katibu Muhtasi
37. Ndg. Kelvin John Chiwangu - Tehama na Mawasiliano
38. Ndg. Silver S. Chindandi - Mwandishi Taarifa Rasmi
39. Ndg. Tumaini A. Fungo - Mwandishi Taarifa Rasmi
40. Ndg. Catherine Kitutu - Mhudumu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba kuwasilisha.

Andrew John Chenge, (MB)

Mwenyekiti,

Kamati ya Uandishi ya Bunge Maalum

22 Septemba, 2014